# Nipashe

Jumatano Septemba 18, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580026

www.ippmedia.com

ww n/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Ufukwe Coco Beach sasa wafungwa kwa miezi sita

UKURASA 2




UKURASA 13

# Diwani amwonyesha jeuri RC Mwanri



• **Katika** operesheni fukuafukua, akataa agizo lake kwa kumweleza kuwa...*Uk. 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**FATMA KARUME AMSHTAKI MUSIBA KORTI KUU ZENJI**

RAIS mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, amemshtaki Cyprian Musiba katika Mahakama...

UKURASA WA 3

**KINA MBOWE KUJITETEA KWA SIKU SABA MFULULIZO**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kusikiliza ushahidi wa upande wa utetezi wa kesi ya...

UKURASA WA 4

**VIONGOZI, WANAHABARI WAMLILIA DILUNGA**

VIONGOZI mbalimbali na wanataaluma ya habari wamemlilia aliyekuwa Mhariri wa Gazeti la Jamhuri, Godfrey Dilunga...




Wananchi wakiangalia basi la mwendokasi namba T 130 DGW, likiondolewa katika makutano ya Barabara ya Bibi Titi Mohamed na Morogoro, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kugongwa na lori namba T410 DEL. Watu wawili walijeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## CCM yaomba msamaha viongozi

UKURASA 2

## Mkuu wa Mkoa adai Bodi Mikopo Elimu inaua vipaji

UK.21


**MICHEZO** **AZAM KUIWAHI MAPEMA TRIANGLE FC** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Diwani amvimbia RC Mwanri

**Na Mwandishi Wetu**

DIWANI wa Kata ya Mabama wilayani Uyui, Renatus Byagala, amemtunishia misuli Mkuu wa Mkoa wa Tabora , Agrey Mwanri, baada ya kutajwa katika kura za siri zilizopigwa na wananchi akidaiwa kujihusisha na utapeli.

Kura tisa zilimwangukia diwani huyo pamoja na mtu aliyedaiwa kuwa Mchungaji wa Kanisa wa FPTC, wote wakituhumiwa kujihusisha na utapeli wakati wa mkutano wa hadhara wa Mwanri na wananchi uliofanyika katika Kata ya Mabama wilayani Uyui.

Mkutano huo ulianza kwa mkuu wa mkoa huyo kuzungumza na wananchi juu ya operesheni fukuafukua aliyoianzisha kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ujambazi na uhalifu mkoani mwake.

Baada ya kutangaza kuanza kwa operesheni hiyo, Mwanri aligawa karatasi na kalamu kwa wananchi ili waandike majina ya watu wanaohisi kujihusisha na ujambazi na uhalifu mwingine.

Baada ya kura hizo, Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, alitangaza matokeo na kumtaja aliyeongoza kwa kutajwa na wananchi wengi kuwa ni mtu aliyetajwa kwa jina la Mchungaji Abel, aliyetajwa na wananchi 19.

Msuya alisoma jina moja moja kwa waliopigiwa kura na idadi ya kura, akibanisha kuwa waliotajwa ni 32 na wote watahojiwa na Jeshi la Polisi.

"Tutafanya kwa kata zote, tupate idadi ya watu wanaotusumbua, Jeshi la Polisi wana utaalamu wa kumuhoji mtu na kujua ukweli na uhalisia wa maisha yake na nini anafanya. Ninyi kutuandikia hivi inatupa ufahamu wapi tuanzie," Msuya alisema.

Baada ya tangazo hilo, Mwanri alisema wote waliotajwa wanatakiwa kwenda kuripoti kituo cha polisi, vinginevyo wangesakwa "kama panya" kama ingefika saa 12 jioni hawajatii agizo hilo.

Kutokana na agizo hilo la Mwanri, Byagala alisimama na kusema: "Nimetajwa kwa kura tisa kwa umaarufu wa utapeli, nashukuru sana lakini naamini zoezi hili na majukumu makubwa niliyonayo na afya yangu, uwezekano wa leo kufika kituo cha polisi kujitetea na kujieleza hilo suala la kura tisa utanisamehe kwa kuwa wewe ndiye kamanda wa polisi ngazi ya mkoa."

Jana, Nipashe ilimtafuta Katibu wa Mwanri kujua hatma ya diwani huyo na kuelezwa kuwa alikwenda kuripoti kituo cha polisi asubuhi ya siku iliyofuata.

Alisema diwani huyo aliomba aende siku iliyofuata kutokana na matatizo ya kiafya na umbali wa kutoka nyumbani kwake hadi kituoni, ikidaiwa ni takriban km 40.

"Nguvu ya umma ni nguvu inayotokana na Mungu, safari tuliyosafiri na majambazi imefika mwisho, leo tumekuja na operesheni fukuafukua," Mwanri alisema wakati anatangaza operesheni hiyo.

Alisema alitembelea Hospitali ya Kitete na wengi wa wagonjwa aliozungumza nao walidai kukatwa panga na majambazi jioni na wengine alfajiri wakati wakiwa kwenye kwenye biashara zao.

"Hakuna aliyesema saa sita usiku au saa nane, wote ni saa 12, saa moja na saa mbili usiku, hakuna atakayekuja kuiba hapa bila kumshirikisha mwenyeji," alisema.

INAENDELEA UK.8



Mabaki ya boti inayojulikana kwa jina Lulimbe, ikiwa imetia nanga baada ya kupata ajali ya moto juzi, wakati ikiwa safarini kutoka Kemondo wilayani Bukoba kuelekea Rushonga Bumbire wilayani Muleba Mkoa wa Kagera juzi, ambapo abiria 56 walinusurika kifo. **PICHA: RESTITUTA DAMIAN**

# Coco Beach yafungwa miezi sita

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli kueleza kukerwa na baadhi viongozi ambao hawasimamii na kuchukua uamuzi katika utekelezaji wa miradi jijini Dar es Salaam, uongozi wa Manispaa ya Kinondoni umetangaza kuufunga Ufukwe wa Coco ili kupisha ujenzi.

Juzi Rais Magufuli wakati akizindua kiwanda cha kutengeneza mabomba Vingunguti jijini Dar es Salaam, alisema baadhi ya miradi inayocheleweshwa ni pamoja na Kiwanda cha Machinjio Vingunguti na ufukwe huo ulioko Oysterbay jijini.

Jana, Meya wa Kinondoni, Benjamin Sitta, akiwa na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Aron Kagurumjuli, walifika kwenye ufukwe huo na kutangaza rasmi unafungwa kwa muda kupisha ujenzi uliolenga kuuendeleza ili uwe wa kisasa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Sitta alisema ufukwe huo umefungwa kwa muda kupisha ujenzi ambao utachukua muda wa miezi sita kuanzia sasa na utagharimu Sh. bilioni 13.6.

"Tutafunga mpaka kule wanakouza mihogo, wanaouza mihogo wameshapewa notisi ili watafute sehemu nyingine, tutafunga eneo hili lote kwa mabati ili wakandarasi wafanye kazi bila kuleta matatizo, mkiona ufukwe umefungwa ni kwa maslahi mapana ya manispaa na mkoa wetu," alisema.

Alibainisha kuwa awali waliomba Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi huo lakini baada ya mazungumzo na mkandarasi, imeshuka hadi Sh. bilioni 13.6.

"Ninaishukuru timu ya watalaamu na wakandarasi wameonyesha uzalendo, tutahakikisha tunapata ufukwe wa kimataifa ili watu wakija kupumzika, wapate mandhari kama ya Afrika Kusini au Uingereza na kwingine," alisema.

Aliongeza kuwa manispaa pia inaendelea na mchakato wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa soko la Tandale ambao taratibu za kisheria zimeendelea kufuatwa.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo (Kagurumjuli) alisema kwa upande wa ununuzi katika mradi wa Coco Beach hawakuruka hata kipengele kimoja hivyo kwenye eneo hilo wapo salama.

# CCM sasa yawaombea msamaha waliopotoka

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hamprey Polepole, ameomba radhi kutokana na waziri, wakuu wa mikoa na wilaya kutoa kauli za ukiukwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria.

Amesema msahama huo ni kwa niaba ya Mwenyekiti wa chama hicho kwa kuwa walitoa kauli hizo wakiulizwa kwa sasa hawawezi kuzifafanua kwa kuwa walizungumza kwa hisia.

Viongozi hao kwa nyakati tofauti walitoa kauli za kuelekeza majambazi, vibaka, majangili na watenda makosa mengine kuuawa, hivyo kusukuma watu kujichukulia sheria mkononi.

Akihojiwa na moja ya vituo vya redio jana, Polepole alisema: "Tunachukizwa na wezi, majambazi, wabadhirifu wa mali ya umma, wala rushwa, majangili wanaoharibu urithi ambao Mungu wa mbinguni ametupatia Watanzania kwa kuchoma moto au kuua wanyama, tunachukizwa mno."

Alisema wakati kiongozi anachukizwa na mambo hayo ndiyo wakati ambao anapaswa kuzui hisia ili kuepuka lugha ambazo zitasababisha matatizo.

"Wakati unapochukizwa ndipo kiongozi unatakiwa uzuie hisia, kuchukizwa na watu wabaya kunakuja hisia, niwaombee msamaha wale viongozi ambao wana haki ya kuchukizwa, lakini chuki yao ya kutusaidia Watanzania dhidi ya watu wabaya ilipitiliza wakawa na hisia," alisema na kuongeza:

"Kama viongozi, hawa hawakupaswa kusema vile, lakini ilikuwa kwa sababu ya chuki dhidi ya watu wabaya wanaotuhujumu, Tanzania ni namba tatu kwa utalii duniani halafu unasikia mtu anakuja kuua twiga, unapata hasira.

"Niwaombe samahani kwa niaba yao, dhamira yao ilikuwa njema, lakini mtu akikufanyia kitu kibaya, unaweza kufanya kitu kikubwa na baadaye ukajutia," alisema.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Musa Taibu, ni miongoni mwa waliolengwa na ombi hilo la msamaha. Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi aliwataka wananchi wanaomiliki silaha wanapokutana na majambazi, wawaue.

"Ndugu zangu wananchi, pale inapotokea kwamba kuna jambazi na wewe una bunduki, tumia akili za kuona ni namna gani unaweza kukabiliana na jambazi huyo, mtandike risasi, hakuna atakayekulaumu," alisema.

"Na bunduki yake ichukue tuikute, tukikuta na mwili, hakuna tatizo lolote, huyo ni jambazi na alichokitaka kufanyiwa ndiyo hicho alichostahili kupewa."

Hivi Karibuni, Waziri Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, alisema angekutana na mmoja wa majangili waliokamatwa Septemba 3, angempiga risasi na kumuua.

Dk. Kigwangalla alitoa kauli hiyo baada ya vipande 339 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.4 kukamatwa maeneo ya Chamazi. Idadi hiyo ya vipande vya meno sawa na tembo 117.

Kauli nyingine zenye viashiria vya uvunjifu wa sheria zilizomwibua Polepole kuomba radhi ni pamoja na iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipoagiza anayeingia nyumbani kwa mtu kwa nguvu, auawe kwa sababu "amechagua kifo".

Pia, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, alisema anajua kuna watu wanaishi kwa kutegemea wizi huku wakiamini kuwa wakipelekwa mahakamani wanapewa dhamana.

"Sasa nawaambia siku zao zinahesabika, watapigwa na kupewa ulemavu kwa kuvunjwa miguu," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Fatma Karume amshtaki Musiba Korti Kuu Zenji

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, amemshtaki Cyprian Musiba katika Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa madai ya kukashifiwa na mwanaharakati huyo.

Baada ya kuona nakala ya wito wa mahakama ikisambazwa kwenye mitandao ya kijamii, Nipashe jana ilimtafuta Fatma kuuzungumzia, na alidai kuwa wanatakiwa kufika katika mahakama hiyo iliyoko Vuga mjini Zanzibar Oktoba 3, mwaka kwa ajili ya kutajwa kwa kesi hiyo Na. 39 ya mwaka 2019.

"Ninamshtaki kwa kunikashfu kwa kusema kwamba eti nimetiwa mimba na muuza unga, na kwamba sina staha, mimi nina mume na watoto, sasa siwezi kukubali ujinga huu," Fatma alidai.

Fatma ambaye pia ni wakili wa kujitegemea, anaungana na Waziri wa zamani Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, kufungua mashtaka kwa madai ya kushushwa hadhi na Musiba.

Mwanaharakati huyo ambaye amekuwa akijipambanua kuitetea serikali, amekuwa akiingia katika migogoro na watu mbalimbali ikiwamo hivi karibuni kuingia katika vita ya maneno na Waziri wa Mambo ya Ndani na Nchi, Kangi Lugola, baada ya waziri huyo kumtaka kutofautisha harakati zake na serikali.

Mwanaharakati huyo pia aliingia katika mgogoro na viongozi wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakiwamo makatibu wakuu wastaafu, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, aliodai ni wasaliti ndani ya chama hicho na kushauri wafukuzwe uanachama.

Membe amefungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam akitaka kulipwa fidia ya Sh. bilioni moja na mwanaharakati huyo kwa kuzushiwa uongo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa na Daktari Mkuu wa Kituo cha Afya Kibaoni, Happiness Ndosi (kushoto), akikagua kituo hicho, kilichopo katika Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro, jana. **PICHA: OWM**

# Kina Mbowe kujitetea kwa siku saba mfululizo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kusikiliza ushahidi wa upande wa utetezi wa kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, baada ya mawakili wa utetezi kuwa na udhuru wa kikazi.

Mahakama hiyo imesema itaanza kusikiliza ushahidi huo mfululizo Septemba 24, 25, 26, 27 na Oktoba Mosi, 2 na 3, mwaka huu.

Hata hivyo, Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba anayesikiliza kesi hiyo, kabla ya kupiga kalenda alisema haridhishwi na kuahirishwa mara kwa mara na kwamba ni lazima isikilizwe na imalizike.

Alisema kesi hiyo tangu ianze ina migogoro japo imepitia kwa mahakimu tofauti kwamba inatakiwa kumalizika.

Awali, upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Gaston Shundogalumbindi kwa niaba ya jopo la mawakili wote, alidai kuwa wanaudhuru wa kikazi katika Mahakama Kuu tofauti ikiwamo Kanda ya Shinyanga.

Pia, mshtakiwa Peter Msigwa na John Heche, wamefiwa na kuomba ruhusa ya kusafiri kwenda kuwazika wapendwa wao.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Dk. Zainabu Mango, Faraja Nchimbi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Mawakili wa Serikali Jaqline Nyantori na Salim Msemo.

Nchimbi alidai kuwa sababu za mawakili wa utetezi hazina mashiko na kwamba wapo mawakili wengine walitakiwa kufika kuendelea na kesi hiyo.

Alisema kesi hiyo lazima imalizike na kwamba itaanza kusikilizwa utetezi Septemba 24, mwaka huu.

Alisema kwa kuwa washtakiwa wamefiwa mahakama yake imeridhia kwenda kuwazika wapendwa wao.

Mbali ya Mbowe washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vincent Mashinji , Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Wengine ni, Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama na wote wanadaiwa kuwa, Februari Mosi na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko la kutawanyika.

# NACTE wafungua udahili wa mwisho

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi (Nacte) limesema linaendelea na udahili kwenye taasisi na vyuo vyote vilivyosajiliwa au kuwa na programu zinazotambuliwa na baraza kutoa mafunzo ngazi ya astashahada na stashahada.

Mkuu wa Kitengo cha Udahili wa baraza hilo, Twaha Twaha, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema pia wanaendelea kufanya uhakiki wa majina 58,193 ya waliochaguliwa na taasisi na vyuo mbalimbali vinavyotoa elimu ya ufundi na mafunzo.

Alisema majibu ya uhakiki yatatolewa Oktoba 4, mwaka huu, kama ilivyo kwenye kalenda ya baraza inayoongoza shughuli za kitaaluma. "Kwa kuzingatia kuwa bado kuna vyuo vyenye nafasi wazi na kwamba wapo wanafunzi ambao hawajadahiliwa kwenye chuo na taasisi yoyote lakini wanayo nia ya kufanya hivyo, Nacte ilifungua dirisha la udahili kwa awamu ya pili na ya mwisho kwenye vyuo na taasisi zinazotoa programu za astashahada na stashahada nchini kuanzia Septemba 7, mwaka huu na litafungwa Septemba 25," Twaha alisema.

Aliongeza kuwa nafasi za kujiunga na vyuo vya ualimu na uuguzi vya serikali zimejaa na hivyo wanaendelea kudahiliwa kwa vyuo vingine.

Twaha pia aliwataka wahitimu wa kidato cha nne na sita na walio na sifa za kujiunga na programu mbalimbali, kutumia fursa hiyo kutuma maombi ya udahili kwenye taasisi na vyuo vyenye nafasi na ambavyo bado vinapokea maombi au udahili katika ngazi ya astashahada na stashahada. Alisema majina ya watakaochaguliwa na taasisi na vyuo mbalimbali yatawasilishwa Nacte kuanzia Septemba 25 hadi Septemba 27, mwaka huu kwa ajili ya uhakiki.

Mbali na hilo, Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu (Tahliso), ilifanya ziara ya mafunzo Nacte kwa lengo la kupata elimu na uelewa wa kutosha kuhusu taasisi hiyo na namna inavyofanya kazi.

Mwenyekiti Tahliso, Peter Niboye, akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, aliwataka wanafunzi kutimiza wajibu wao ikiwamo kutembelea tovuti ya Nacte yenye mifumbo mbalimbali itakayowawezesha kutatua changamoto zao kwa wakati bila kufika ofisini.

"Pia kama Tahliso tunavitaka vyuo kudahili kwa kufuata kanuni na vigezo walivyoelekezwa na Nacte na hii ikiwa ni pamoja na kufuata mitaala kama inavyoelekezwa ili kuzalisha wataalamu walio bora," Niboye alisema. Kiongozi huyo wa Tahliso pia aliitaka serikali na vyuo kuimarishe ulinzi na usalama katika vyuo ili wanafunzi waishi kwenye mazingira salama.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




TAIFA STARS VS SUDAN
SEPTEMBA 22, 2019 - UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Viongozi, wanahabari wamlilia Dilunga



**Na Mwandishi wetu**

VIONGOZI mbalimbali na wanataaluma ya habari wamemlilia aliyekuwa Mhariri wa Gazeti la Jamhuri, Godfrey Dilunga (43) (pichani), aliyefariki dunia jana alfajiri.

Katika ukurasa wake wa Twiter, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema "Godfrey Dilunga, Mhariri wa Gazeti la Jamhuri na kwa muda mrefu sana Mhariri Mkuu wa Gazeti la Raia Mwema ametangulia mbele ya haki.

"Salaam zangu za pole kwa familia yake, Jukwaa la Wahariri na waandishi wote nchini. Mmoja wa wahariri mahiri kabisa wa magazeti katika nchi yetu."

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliandika "Nimepokea kwa masikitiko na mtetemo mkubwa msiba wa rafiki yangu Godfrey Dilunga aliyekuwa akifanya kazi za kupasha habari umma. Mwenyezi Mungu muweza akuhifadhi unapostahili

INAENDELEA UK.8



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (wa pili kushoto), akizungumza na wanafunzi wa shule mbalimbali katika hafla ya kukabidhi msaada wa kimasomo kwa wanafunzi wa kike 100 waliofaulu masomo ya sayansi na kuchanguliwa kujiunga kidato cha tano kwa mwaka 2019, iliyofanyika jijini humo jana. Kushoto ni Balozi wa Umoja Falme za Kiarabu hapa nchini, Khalifa Abdulrahman Mohammed Al Marzooqi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wasichana 100 wasio na uwezo wapata ufadhili kidato cha tano

**Na Mariam Magili,** TUDARCO

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda kwa kushirikiana na Balozi wa Falme za Kiarabu, Khalifa Abdul-Ragman Al-Marzoo, wametoa ufadhili wa masomo kwa wasichana 100 wasio na uwezo waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano.

Kati ya wanafunzi hao 75 ni waliofaulu masomo ya Sayansi na 25 ya Sanaa kutoka katika manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam. Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makonda aliomba msaada kwa balozi huyo ambaye alikubaliana na wazo lake la kuwasomesha wanafunzi hao 100 wa mkoa huo. "Rais Magufuli amejitahidi kutoa elimu bure kwa wanafunzi hawa wa shule za msingi hadi sekondari kwa kutambua mchango wanafunzi wa kike ambao wanafaulu vizuri, lakini wazazi au ndugu zao hawana uwezo wa kuwasomesha, nimejitolea kuwatafutia ufadhili wa masomo," Makonda alisema.

Aliahidi kuwa wanafunzi hao atawasomesha hadi kidato cha sita na kila mwaka ataendelea kujitolea kuwatafutia ufadhili wanafunzi wengine.

Kwa upande wake, Balozi Al-Marzoo, alimpongeza Makonda kwa juhudi zake za kusaidia watoto wa kike wa masomo ya Sayansi ili kupata elimu. Alisema Falme za Kiarabu zinashirikiana na Tanzania katika masuala mbalimbali ya kusaidia jamii ikiwamo ufadhili wa masomo. Alisema amependa kusaidia wasichana hao 100 ambao wamefaulu kidato cha nne na hawana uwezo wa kuendelea na masomo kwa sababu anaamini wakipata elimu watakuja kusaidia jamii. Alisema pia ameandaa ripoti kwa ajili ya kuomba miradi ikabidhiwe ofisini kwake badala ya kuwa chini ya madiwani kama ilivyo sasa. Alisema madiwani wamekuwa wakikwamisha miradi ya maendeleo bila sababu.

"Wapo watendaji ambao wamekaa muda mrefu na kuchelewesha miradi mbalimbali kwa makusudi tu hayo majina yao tunayo na tunawafahamu na wengine wapo humu ndani," Makonda alisema. Makonda pia alisema kabla ya kukubaliwa kwa ombi lake la miradi kupitishwa katika ofisi yake, hataacha kuwachukulia hatua watendaji watakaokuwa vikwazo katika kukwamisha miradi ya serikali. "Tunaiandaa kamati ambayo itafuatilia mienendo ya miradi kila hatua ili tupate kujua nani anayekwamisha maendeleo na miradi ya serikali kwa sababu zake binafsi," alisema.




## 6 mbaroni tuhuma kutakatisha bil. 4/-

**Na Hellen Mwango**

WATU sita wakazi wa jijini Dar es Salaam wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuratibu genge la ujangili, kukutwa na nyara za serikali na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni nne.

Washtakiwa hao ni Hassan Likwena (39) maarufu Nyoni, Bushiri Likwena, Oliver Mchuwa (35), Salama Mshamu (21), Haidary Sharifu (44), maarufu White na Joyce Thomas (33).

Washtakiwa hao wote walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali Salim Msemo, Tully Helela na Elizabeth Mkunde. Wankyo alidai shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanatuhumiwa kwa kushiriki genge la uhalifu kati ya Januari Mosi, 2017 na Septemba 3, mwaka huu katika mikoa ya Mtwara, Pwani na Dar es Salaam, kupanga uhalifu wa kupokea vipande vya meno ya tembo na kiboko.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Septemba 3, mwaka huu eneo la Saku, Chamazi, walikutwa na meno ya tembo 413 yenye thamani ya Dola za Marekani 1,755,000 bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku na eneo la tukio la pili, washtakiwa walikutwa na vipande viwili vya meno ya kiboko vikiwa na thamani ya Dola za Marekani, 1,500 bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Shtaka la nne, ilidaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2017 na Septemba 3,mwaka huu, washtakiwa walitakatisha Sh. 4,043,463,000 na kukutwa na nyara hizo za serikali wakati wakijua ni zao la kosa tangulizi la ujangili.

Hata hivyo, kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote mpaka upelelezi utakapokamilika na kuhamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba Mosi, mwaka huu na washtakiwa watarudishwa mahabusu.

policy forum

# TAMKO LA POLICY FORUM NA TACCEO KUHUSU KANUNI ZA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA, 2019

**A. UTANGULIZI**

Mtandao wa Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TACCEO) na Jukwaa la Sera (Policy Forum) tumeendelea kufuatilia mchakato wa utayarishaji wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa,2019 nchini Tanzania kwa kutoa maoni kwenye rasimu ya kanuni husika ambapo maoni na mapendekezo yetu yaliwasilishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI mnamo mwezi Aprili, 2019. Baada ya kuchapishwa na kutangazwa kwa kanuni husika na waziri mwenye dhamana, tumefanya uchambuzi wa kina wa kanuni hizo ili kubaini kuzingatiwa kwa maoni na mapendekezo tuliyowasilisha.

Imekua desturi kwa mashirika na mitandao ya AZAKI kufanya uchambuzi kuhusu masuala ya Sera, Kanuni, Sheria na Miongozo mbalimbali inayohusu michakato ya maendeleo nchini. Uchambuzi huu wa kanuni umelenga kubaini mambo mazuri, mapungufu na changamoto zake kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tukiamini kuwa uchaguzi huo ni sehemu muhimu na msingi wa demokrasia shirikishi na mfumo wa uwakilishi hapa nchini.

Tukiwa Asasi za Kiraia ambazo haziungi mkono mgombea yeyote wala chama chochote cha kisiasa, tunatimiza wajibu wetu kama raia wazalendo kwa mujibu wa ibara ya 8 ya Katiba ya Tanzania.

Kutokana na uchambuzi wetu, Policy Forum na TACCEO tumebaini mambo kadhaa katika maeneo makuu mawili ya kimchakato na kimaudhui. Kwanza, Mchakato umekua wa uwazi na shirikishi kwa kiasi kikubwa, jambo ambalo ni zuri na la kuipongeza serikali ya awamu ya tano.

Pili, masuala mengi katika kanuni yamezingatiwa na kufanyiwa maboresho kama tulivyopendekeza. Policy Forum, TACCEO na wadau wengine tunaipongeza serikali kwa kuzingatia takribani asilimia 70 ya maoni na mapendekezo yetu kama tulivyowasilisha. Hata hivyo, pamoja na maboresho makubwa yaliyofanyika katika kanuni hizo, bado tumeona kuna masuala ya msingi ambayo hayakuzingatiwa katika utungaji wa kanuni hizo. Hivyo basi, tumeona ni muhimu umma na mamlaka husika kujua na kuangalia namna ya kuyazingatia wakati wa uchaguzi.

1. Masuala Ambayo Hayakuzingatiwa
1.1 Masuala ya Jumla
1.1.1 Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu na Mwenye Mahitaji maalum

Kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka za Miji na mamlaka ya wilaya (vijiji) kifungu cha 32(1) na mamlaka za wilaya (vitongoji) Kifungu cha 31(1) kinasema kutakuwa na sanduku maalumu la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakavyomwezesha mpiga kura kutumbukiza karatasi ya kura kwa urahisi, pia kifungu cha 36(1) (Mamlaka za miji na Wilaya-vijiji) na kifungu cha 35 (1) cha Mamlaka za wilaya-vitongoji) kinaelezea juu ya usaidizi kwa wenye mahitaji maalumu kusaidiwa kupiga kura. Maoni yamezingatiwa ingawa kanuni hizo hazibainishi namna ambavyo watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum watafikia sanduku la kupigia kura kwa urahisi.

### 1.1.2 Sababu za Kuahirisha Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019, kifungu cha 37 (Mtaa na Kijiji) na 36 (Kitongoji) vinasema kwamba endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika,msimamizi msaidizi wa uchaguzi baada ya kuwasiliana na msimamizi wa uchaguzi atahairisha uchaguzi. Hivyo basi, ni vyema kanuni hizo ziwe bayana juu ya sababu za msingi ambazo zitapelekea kuhairisha zoezi la uchaguzi. Kwa mfano, kufariki kwa mgombea, kutokea kwa janga la asilia na kutokea kwa magonjwa ya mlipuko.

### 1.1.3 Sifa za Msimamizi wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019, tafsiri ya msimamizi wa uchaguzi ni mtumishi wa umma tu, jambo ambalo linamnyima nafasi raia mwingine asie mtumishi wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.

### 1.1.4 Mkanganyiko wa Majina ya Kanuni

Katika Kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa (mamlaka za Miji) Sura 288, inaonesha jina ni Kanuni za Uchaguzi kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji. Ambapo kwenye Mamlaka za Miji hakuna Kitongoji, badala yake ingesomeka Kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka Ya Miji Midogo Za Mwaka 2019(sura ya 288).

### 1.1.5. Kinga kwa Msimamizi wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019, kifungu cha 49(Mtaa na Vijiji) na 46 (kitongoji) vimempa kinga msimamizi wa uchanguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au Mtumishi yeyote wa Umma aliyehusika na Usimamizi wa Uchaguzi hatowajibika kwa jinai au madai au kuchukuliwa hatua za kinadhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni hizi.

Changamoto ya kifungu hiki ni uwezekano wa mhusika kutumia vibaya madaraka yake kwa kisingizio cha "nia njema". Kwa kuwawekea kinga wasimamizi wa uchaguzi, kunazuia vyombo vya kutoa haki kutimiza wajibu wake na raia yoyote kukosa haki ya kudai katika vyombo hivyo.

### 1.1.6 Kibali cha Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 (1) (2) cha mamlaka za wilaya -vijiji na mamlaka za miji, na kifungu cha 47(1) cha mamlaka za wilaya – vitongoji, waangalizi wa ndani wa uchaguzi wataweza kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa tu. Kifungu hiki kinaleta urasimu usiowalazima wa kupata vibali hasa kwa vikundi amabavo viko mbali na Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara.

### 1.1.7 Tafsiri ya Mkazi

Kwa mujibu wa kanuni hizi tafsiri ya mkazi ni raia wa Tanzania anayeishi kwenye eneo la mtaa, Kijiji au kitongoji ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la kijiji,mtaa au kitongoji. Kifungu hiki hakikutamka bayana muda wa mtu kutambuliwa kuwa mkazi wa kijiji, mtaa ama kitongoji. Hivyo kinaweza kutoa mwanya kwa raia yeyote mwenye nia ovu au wahamiaji haramu kujiandikisha na kupiga kura.

### 1.1.8 Mapungufu ya kiuchapaji kwenye Majedwali na Fomu

Tumebaini mapungufu ya kiuchapaji kwenye majina ya kanuni ambayo pia yameathiri fomu zilizoambatanishwa, tunatambua kwamba baadhi ya fomu zitarekebishwa katika Halmashauri husika;

- Fomu za matokeo hazina nafasi ya kutaja jina la kituo cha kupigia kura.
- Fomu za uteuzi hazibainishi /kutambua watu wenye ulemavu walioonesha nia ya kugombea nafasi za uongozi.
- Fomu za Mpiga kura hazina picha ya Mgombea, hali hii inaweza kuleta ugumu wa utambuzi wa mpiga kura kuchagua mgombea anaemtaka hasa kwa mpiga kura asiejua kusoma na kuandika.

**Mapendekezo**

1. Tunapendekeza Waziri mwenye dhamana kuzielekeza mamlaka husika kufanya maboresho katika fomu za uteuzi, upigaji kura, na matokeo ya uchaguzi. Hususan Fomu ya matokeo ya uchaguzi kutaja jina la kituo la kupiga kura.
2. Wadau wa uchaguzi wa serikali za mitaa watoe msaada na ushirikiano ili kuhahikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi.
3. Mamlaka ya uchaguzi, Msimamizi wa uchaguzi, Msimamizi msaidizi wa uchaguzi na Msimamizi wa kituo watoe msaada na ushirikiano ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi.
4. Katibu Mkuu ofisi ya Rais TAMISEMI akasimu mamlaka ya kutoa vibali ya kuangalia uchaguzi na kuendesha elimu ya mpiga kura kwa Msimamizi wa uchaguzi ngazi ya Halmashauri.
5. Baada ya uchaguzi, Waziri mwenye dhamana azielekeze Halmashauri zote nchini kuandaa na kutoa taarifa ya uchaguzi ya serikali za mitaa kwa umma ikiainisha pamoja na masuala mengine upigaji kura, matokeo, ushiriki wa makundi maalum (vijana, wanawake na walemavu).
6. Sanduku la kupigia kura liwekwe mahali ambapo watu wenye mahitaji maalum wanaweza kulifikia kwa urahisi.

215422802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukaguzi huu wa asubuhi unakera

**UKAGUZI** wa mabasi ya daladala asubuhi na mapema unaofanywa na trafiki kwenye barabara zote jijini Dar es Salaam, wakati mwingine unawakera abiria.

Wakati trafiki ni haki na wajibu wao kufanya ukaguzi huo, tunaona kama kufanyakazi hizo asubuhi pamoja na foleni zilizoko barabarani kunawatatiza abiria.

Wanatatizika kwa sababu wanawahi kazini, shuleni, safarini na hata hospitalini na wakati mwingine inatokea kusimamisha magari kwa utaratibu wa kuyapiga mkono kukasababisha foleni zaidi.

Usumbufu huu unaozuia magari pande zote mbili za barabara kwa mfano yanayokwenda na yanayorudi, hukwamisha vyombo vingine vya usafiri kama pikipiki, bajaji na mabasi ya mikoani.

Ndiyo sababu tunaona pengine ni vizuri kuwa na programu maalumu ya kufanya kazi hiyo ambayo haiukwazi muda wa asubuhi wakati watu wengi wakikimbilia kazini na watoto wakiwahi shuleni.

Tunasema hivi kwa sababu ukaguzi huo mara nyingi unafanywa mapema asubuhi kuanzia saa 1:00 na kusababisha malalamiko miongoni mwa abiria na hata mabishano na trafiki.

Abiria, hawakatai ukaguzi huo lakini, muda unaofanyika unawachelewesha na pia unazidi kuwapotezea wakati kwa kuwa barabara nyingi kuu zinakuwa na foleni.

Licha ya kwamba ukaguzi wa magari ni muhimu kwa ajili ya usalama wa wasafiri na vyombo vya moto, lakini suala la muda mwingi kupotea wakati dereva, kondakta wanapojadiliana na polisi unawafanya watu kuona kuwa hatua hiyo inawakwaza.

Tunashauri polisi kuwa na programu ya ukaguzi inayowezesha kufanya ukaguzi hiyo, wakati ambao magari hayo hayana abiria wengi na bila msongamano barabarani, pengine kuanzia saa 4:00 asubuhi.

Lakini, pia ukaguzi ufanyike kwa uwazi na kosa la wahusika mathalani dereva na kondakta lifahamike. Ukaguzi unapochukua dakika nyingi aidha, ukifanyika mbali kama mita 20 kutoka lilipoSimama basi unawafanya wasafiri kuwa na hasira na malalamiko zaidi.

Wakati wa ukaguzi huo, polisi analisimamisha basi na mara linapoegeshwa kondakta hushuka kuzungumza na wakaguzi.

Jambo jingine ambalo ni vizuri likafahamika ni utaratibu wa kukaguliwa. Hivi iwapo trafiki amelikamata gari Mbezi na kulikagua kuna haja tena ya kuendelea kulipiga mkono na kulikagua likifika Mwenge au eneo jingine njiani?

Iwapo kila kituo au sehemu daladala inasimamishwa na kukaguliwa, abiria wanaweza kuwaza kuwa huenda hakuna ukaguzi bali jambo jingine.

Hii ni kwasababu kama kuna tatizo kwanini, trafiki waliofanya ukaguzi mwanzo wasiligundue? Kama hitilafu zimeendelea kuwapo walikagua nini basi? Hivi sheria nazo zinasemaje?

Aidha, tunashauri ukaguzi barabarani uende mbali si kukamata daladala pekee bali pia kuyaondoa magari mabovu yanayofuka moshi na kuleta kero njiani nzima.

Ukumbukwe ni zama za sayansi na teknolojia polisi hawana sababu ya kuendelea na ukaguzi wa kizamani wa kusimamisha magari njiani na kupoteza muda wanaweza kutafuta njia bora zenye ufanisi zaidi.


Tunaamini kuwa zama hizi kazi hufanyika kwa utaratibu wa kiteknolojia na popote gari linaweza kupata maelekezo ya ukaguzi bila kujali kama lipo barabarani au lina abiria.

Tunasema hayo kwa sababu ni ukweli kuwa baadhi ya madereva wenye magari mabovu wakishapata habari kuwa polisi wako barabarani hawatafanya kazi siku hiyo.

Ndiyo maana tunasema ni vyema kubuni mbinu nyingine za kisasa ili kufanya ukakuzi wa kweli badala ya kuwindana barabarani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Demokrasia ianzie ndani ya vyama vya siasa

Na Sabato Kasika

**MWAKA** 1992 ni wa kukumbukwa na wadau wa vyama vya siasa, kwa vile ndio ambao mfumo wa vyama vingi vya siasa uliruhusiwa rasmi nchini na kuwafanya baadhi ya Watanzania kuanzisha vyama hivyo.

Baadaye mwaka 1995, ulifanyika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo na kulifanya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na wabunge mchanganyiko wakiwamo kutoka chama tawala na upinzani.

Hatua hiyo ya kuruhusiwa kwa mfumo wa vyama vingi ilikuja baada ya kukusanywa kwa maoni kutoka kwa wananchi waliotakiwa kuchagua aidha vyama vya siasa viruhusiwe au visiruhusiwe.

Baada ya hoja hiyo kufikishwa kwa wananchi, matokeo yake ni kwamba asilimia 80 walitaka mfumo wa chama kimoja uendelee na asilimia 20 walitaka mfumo wa vyama vingi.

Pamoja na matokeo hayo, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alishawishi kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini.

Sasa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofuata mfumo wa vyama vingi, lakini moja ya changamoto ambayo imekuwa ikitajwa kuvikabili baadhi ya vyama vya siasa ni ukosefu wa demokrasia.

Hali hiyo imesababisha migogoro kwenye vyama hivyo, baadhi ya wanachama wakivihama, sababu inayopelekea wananchi kutokuwa na imani navyo.

Migogoro hii inaacha makovu, pia inaibua makundi yanayohasimiana na hatimaye kuchangia vyama vyenyewe viporomoke.

Mfano ni kile kilichotokea ndani ya Chama cha Wananchi (CUF) chanzo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad kujiondoa na kuhamia ACT-Wazalendo.

Watanzania wameshuhudia hamahama ya baadhi ya wanachama wa vyama vya upinzani wakiwamo wabunge, madiwani na wenyeviti wa halmashauri, wengi wakikimbilia CCM.

Ukosefu wa demokrasia ndani ya vyama hivyo ni miongoni mwa sababu zinazotajwa kuhamisha wanaohama, ishara ya ombwe la demokrasia.

Umefika wakati sasa kwa vyama vya siasa kuzingatia ujumbe ambao umekuwa ikitolewa kwenye Siku ya Kimataifa ya Demokrasia, inayoadhimishwa Septemba 15 ya kila mwaka.

Viongozi wa vyama vya siasa wazingatie kuwa demokrasia inajengwa na ni jumuishi, kutenda usawa na ushiriki ni msingi muhimu kwa ujenzi wa amani ndani ya vyama vyao.

Kwa maana hiyo ni vyema wanasiasa wakatumia siku hii kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vyao badala ya kulalamika kuonewa wakati wana changamoto ya demokrasia kwenye nyumba zao.

Moja ya viashiria vya demokrasia ni maridhiano au kukaa pamoja kwa kutumia vikao halali kumaliza tofauti zinazojitokeza, kwa kutambua kwamba kutofautiana kwa hoja ni jambo la kawaida.

Lakini bahati mbaya baadhi ya wanasiasa wanaohama vyama huwa wanadai wanapotofautiana na wakubwa wao au kuhoji jambo fulani ambalo wanadhani haliko sawa wanatishiwa kutimuliwa.

Katika mfumo wa vyama vingi, hasa vikubwa vyenye ushawishi kwa jamii, migongano na malumbano ya ndani kwa ndani ni jambo la kawaida, lakini ukweli hukwamisha ukuaji wa demokrasia.

Vinapoibuka vikundi vya wanachama wachache wenye mawazo mbadala na kupaza sauti zao kwamba baadhi ya mambo hayaendi sawa, ni muhimu viongozi kukaa navyo ili kupata muafaka.

Lakini viongozi wanapoziba masikio, matokeo yake ni kuviathiri vyama vyao na kuvifanya vipoteze ushawishi mbele ya jamii kwa kukimbiwa na baadhi ya wanachama na kuwafukuza.

Kwa ujumla suala la demokrasia lina umuhimu ndani ya vyama, kwani lisipozingatiwa, baadhi ya vyama vinaathirika kwa kukimbiwa na wanachama na kuwa aupande mwingine vingine vikifaidika kwa kupata wanachama wapya.

Lakini pia migogoro ndani ya vyama ina faida katika ustawi wa demokrasia kwani kundi la wanachama linapoondoka katika chama na kuanzisha chama kingine ,hutoa ushindani wa kisiasa.

Vyama hivyo vinaweza kuwa na mawazo mbadala katika maendeleo ya demokrasia na taifa kwa ujumla, lakini jambo la msingi ni kwamba demokrasia ni muhimu ndani ya vyama vya siasa.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Godfrey Mngereza, akizungumza kwenye Maonyesho ya Utamaduni, Sanaa na Urithi wa China, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Baba aua mtoto kikatili kwa kupoteza ng'ombe

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

MTOTO Lusambaja Bundala (7), mkazi wa Kitongoji cha Luhafwe, Kata ya Ntongwe Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, ameuawa kikatili kwa kukatwa kichwani na kitu chenye ncha kali na baba yake mdogo, baada ya mtoto huyo kupoteza ng'ombe aliokuwa akiwachunga.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema mauaji hayo yaligunduliwa jana asubuhi katika kitongoji hicho.

Alisema mtoto huyo alikuwa akiishi nyumbani kwa baba yake mdogo, Juma Lusambaje (28), ambaye ndio mtuhumiwa wa mauaji hayo.

Kabla ya kuuawa kwa Bundala, Septemba 12, alikuwa na mtoto mwenzake, Ibrahimu Lusambaja (13), walipotumwa na mtuhumiwa kwenda kuchunga ng'ombe.

Kwa mujibu wa Kamanda Kuzaga, tangu siku hiyo alipokwenda kuchunga mtoto huyo hakuonekana tena hadi jana saa nne asubuhi mwili alipokutwa amekufa kwa kuuawa kikatili kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na kuchomwa na kisu chini ya kidevu.

Kamanda Kuzaga alisema upelezi ulibaini chanzo cha mauaji ya mtoto huyo ni hasira za baba yake mdogo kuchukia baada ya Bundala kupoteza ng'ombe alizokuwa akizichunga.

"Baada ya marehemu kupoteza ng'ombe ndipo mtuhumiwa alipoamua kuchukua sheria mikononi na kuamua kumpiga mtoto hiyo kwa kutumia chuma chenye ncha kali na kumchoma na kisu hadi kumuua, na kuwa hakutoa taarifa kwa mtu yeyote," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema mtuhumiwa anaendelea kushikiliwa na Polisi kwa mahojiano, na anatarajiwa kufikishwa mahakamani.

Mwili wa Bundala ulikabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu.

# Wabunge waunganisha nguvu kudhibiti malaria

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa wabunge wanaopambana na malaria na magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Tapama), ukanda wa joto umeanza juhudi ya utekelezaji wa mpango wa kusaidia na kuwezesha ongezeko la utashi wa kisiasa katika mapambano hayo.

Mwenyekiti wa Tapama, Riziki Lulida, alisema Lengo ni kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini Tanzania ifikapo mwaka 2030, ikiwa ni utekelezaji wa Malengo ya Milenia.

Mradi huo utasaidia kuendeleza programu ya kadi ya ALMA ya tathmini ya uwajibikaji na utendaji wa malaria kwa kuiweka katika mfumo mtandao kuwezesha taarifa za takwimu kupatikana katika simujanja.

Mradi huo unadhamiria kujenga uwezo na kuimarisha zaidi ushiriki wa kisiasa na uwajibikaji unaotokana na kuhamasisha upatikanaji wa takwimu sahihi za malaria kuanzia ngazi ya majimbo hadi taifa.

Lulida alisema mradi huo pia utaongeza na kujenga uwezo wa wabunge wanachama wa Tapama na wabunge wengine wa Bunge la Tanzania kushiriki katika wajibu wao wa kusaidia kupambana na kutokomeza malaria katika majimbo yao.

Alisema lengo ni kusaidia taasisi zinazotekeleza harakati mbalimbali na uwajibikaji katika utekelezaji kwa kupitia mfumo huo.

"Takwimu zinavyoonyesha kupungua kwa kiwango cha maambukizi kimepungua kwa zaidi ya nusu kutoka asilimia 14.4 mnamo mwaka 2016 hadi asilimia 7.3 mwaka 2018," alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Tapama, Dk. Raphael Chegeni, alisema zinahitajika jitihada za kuongeza rasilimali, ushiriki wa wadau mbalimbali na sekta mbalimbali kwa kuona suala hilo ni mtambuka na kuongeza uwajibikaji.

"Kama wabunge tuna jukumu kubwa katika kuunga mkono maono na malengo ya serikali kuelekea kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa wa malaria kufika sifuri ifikapo 2030," alisema.

Katika mradi huo wabunge watapatiwa mafunzo jinsi ya kutumia Kadi ya ALMA ya tathmini ya uwajibikaji na utendaji wa malaria, kuendesha mikutano ya mara kwa mara ya kukagua na kutathimini taarifa ya kadi hizo.

Mpango huo utalenga zaidi kusaidia utendaji wa haraka wa kupunguza maambukizi kwenye mikoa ya Kigoma, Geita, Kagera, Lindi na Mtwara yenye mzigo mkubwa wa ugonjwa wa malaria.

# Kesi kupinga ukomo wa urais, Sept. 24

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imepanga kuanza kuisikiliza kesi ya kupinga ukomo wa urais iliyofunguliwa na mkulima Dezydelius Mgoya dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Septemba 24, mwaka huu.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Mwenyekiti wake, Jaji Kiongozi, Eliezer Feleshi, Benhajj Masoud na Seif Kulita.

Mgoya alijitambulisha mbele ya jopo hilo kwamba yeye ni mkulima wa mihogo, matikiti na mboga mboga na kwamba katika kesi hiyo hana wakili.

Wakili wa Serikali, Daniel Nyakiha, alidai mahakamani kuwa walipeleka majibu yao na mapingamizi nane na kwamba kutokana na kukosa anauani ya mlalamikaji Mgoya, walimpatia nyaraka hizo jana asubuhi.

Mgoya kwa upande wake aliiomba mahakama, kwa sababu alipewa nyaraka hizo muda mchache kabla ya kuingia mahakamani hapo, apewe nafasi ndani ya siku saba ili aweze kuzipitia na kuzijibu.

Hata hivyo, kutokana na kutokuwapo kwa pingamizi kutoka upande wa walalamikiwa, jopo hilo lilikubali hoja za mlalamikaji.

Jaji Feleshi alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa Septemba 24, mwaka huu na kumtaka Mgoya iwapo atakuwa na majibu ya nyongeza juu ya hati ya kiapo kinzani, ayawasilishe kabla ya siku hiyo kwa walalamikiwa.

Jaji Feleshi alimuhoji Mgoya sababu za kutotoa anauani yake, lakini Mgoya alidai kuwa alitoa anauani yake na namba ya simu zaidi ya wiki mbili zilizopita.

Kwa mujibu wa hati ya pingamizi la walalamikiwa ni pamoja na kwamba mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo, mlalamikaji hana mamlaka ya kupinga kifungu cha 3,4,5,6 na 8(3) vya Sheria ya haki za binadamu.

Awali, Mgoya alifungua kesi hiyo chini ya kifungu cha nne cha sheria ya utekelezaji haki na wajibu, sura ya 3 ya 1994 chini ya Ibara ya 30(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.

Kwa mujibu wa hati ya madai ya kesi hiyo, Mgoya anahoji Ibara ya 40(20) ya Katiba ambayo imeweka ukomo wa mihula miwili peke ya miaka mitano mitano (10) ya uongozi katika nafasi hiyo ya urais.

Anaiomba mahakama hiyo itoe tamko na tafsiri ya maana sahihi na athari za masharti ya ibara hiyo.

Pia anaiomba mahakama itoe tafsiri ya maana dhahiri ya masharti ya Ibara ya 42(2) ya Katiba kwa kuhusianisha na masharti ya Ibara za 13, 21 na 22 za Katiba hiyo. Vilevile anaiomba mahakama itoe tafsiri ya maana ya Ibara hiyo ya 40(2) kwa kuhusianisha na Ibara ya 39 ya Katiba.

# Afya ya Askofu Ruwa'ichi yaendelea kuimarika

**Na Mary Geofrey**

HALI ya Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, aliyefanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo, imeendelea kuimarika. Juzi Askofu Ruwa'ichi alitolewa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) baada ya afya yake kuimarika na kuhamishiwa katika wodi ya kawaida.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa Tasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Prof. Joseph Kahamba, alisema jana hali ya kiongozi huyo inazidi kuimarika. "Afya ya Askofu Ruwa'ichi inaendelea kuimarika kila siku, alianza kutembelea tangu wiki iliyopita akiwa ICU kwa hatua chache lakini sasa aneweza kutembea kwa hatua nyingi zaidi," Prof. Kahamba alisema.

Aidha, alisema Askofu Ruwa'ichi anaendelea kufanya mazoezi kwa muongozo wa madaktari bingwa wanaomuangalia kwa karibu.

"Hali yake inaendelea vizuri sana, anazidi kufanya mazoezi kwa kusaidiwa na watalaam kwa sababu hawezi kufanya mwenywe bila kupewa maelekezo," Prof. Kahamba alisema.

Jopo la wataalam hao saba wanaomfanyia uchunguzi na mazoezi kiongozi huyo wa kanisa nchini ni pamoja na madaktari bingwa watatu wa magonjwa Ubongo, Dawa za Usingizi na Magonjwa ya ndani, wataalam wa lishe, wauguzi wabobezi na wataalam wa mazoezi tiba.

Septemba 9, mwaka huu, Askofu Ruwa'ichi alifanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo, ugonjwa unaotambulika kwa jina la 'Chronic Subdural Haematoma'.



Watuhumiwa wanaokabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo, kuratibu genge la ujangili, kukutwa na nyara za serikali na kutakatisha zaidi ya Sh. Bilioni 4 wakiwa chini ya ulinzi wa Askari Polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka yao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wazawa wapigiwa debe zabuni kampuni madini

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SERIKALI imeziagiza kampuni za uchimbaji madini nchini kuwapa kipaumbele wafanyabiashara wazawa, badala ya kutoa zabuni ya kutoa huduma migodini kwa kampuni za kigeni.

Imesema kuwa wapo wafanyabiashara wazawa wenye uwezo wa kutoa huduma hizo.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alitoa agizo hilo juzi mkoani hapa wakati akifungua warsha ya siku mbili kwa wafanyabiashara wa mkoani Geita iliyoandaliwa na Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM) .

Pia aliipa angalizo GGM kuyapa zabuni ya kutoa huduma mgodini humo kampuni ya kigeni badala ya kuwapa kipaumbele wazawa, hivyo kuwataka kufuata mabadiliko ya sheria ya madini namba 8 ya mwaka 2017 inayowataka kuwapa kipaumbe wafanyabiashara wazawa.

Waziri huyo alisema kuwa mgodi wa GGM unaongoza kwa kulipa kodi kubwa serikali kuliko kampuni zote za uchimbaji wa madini nchini, lakini upande wa kitengo cha biashara ndani ya Mgodi huo bado kuna changamoto kubwa Wafanyabiashara wazawa hawapewi fursa hiyo.

Kwamujibu wa Waziri huyo, upo udanganyifu mkubwa kwa baadhi ya kampuni za uchimbaji madini kwenye ukaguzi waliofanya hivi karibuni baada ya kukuta kampuni moja ina kampuni ndogo 54, hivyo kuutaka mgodi wa GGM kuwapa kipaumbele wafanyabiashara wa Geita na ajira.

Mkurugenzi wa Mgodi wa GGM, Richard Jordinson, akitoa taarifa ya mafunzo ya warsha hiyo mbele ya Waziri huyo, alisema kuwa lengo ni kuongeza ufanisi kwa na kuboresha mawasiliano kwa watoa huduma waliopo na watarajiwa sambamba na kuwaelimisha mnyororo wa thamani na mchakato kufanya kazi na GGML zikiwa ni jitihada za kuiunga mkono serikali kuhimiza manunuzi ya bidhaa za ndani.

Makamu wa Rais wa Migodi ya Ashanti Gold Mine (GGML), Simon Shayo, alisema lengo ni kuhakikisha jamii inayozunguka Mji wa Geita inanufaika na kutokana na ushirikiano wa pamoja kati yake na Anglo Gold Ashant.

Aliongeza kuwa mwaka 2018 mtandao wa utoaji huduma ndani ya Mgodi wa GGML uliongezeka na kufikia Watanzania 305 wanaomiliki biashara ambao ni asilimia 76 ya manunuzi yanafanyika wapa nchini .

Awali Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambae pia ni Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, alisema hali ya sasa ya Mji wa Geita ni tofauti na mwaka 2015 wageni waliokuwa wakifika ilikuwa ni vigumu kutambua kuwa kuna utajiri wa dhahabu na kuongeza kuwa anaipongeza serikali kwa kubadlilisha Sheria ya Madini .

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA ) Mkoa wa Geita, Chacha Mwita Wambura, alisema warsha hiyo ikitumika vizuri itafungua milango ya fursa kwa wafanyabiashara .

# Viongozi, wanahabari wamlilia Dilunga

INATOKA UK. 4

rafiki yangu."

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliandika "Innalilah Wainnailayhii Rajiuun, RIP brother (kaka) Dilunga, Allah akujaalie makazi mema peponi."

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kampuni ya Jamhuri, na Mkurugenzi Mtendaji, Deodatus Balile, Dilunga alilazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Septemba 9, mwaka huu, akitokea Hospitali ya Mwananyamala iliyompa rufani, akikabiliwa na maumivu ya tumbo.

"Madaktari na wauguzi wa Muhimbili wamejitahidi kwa kila hali, ila Mungu amempenda zaidi," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa Balile, kampuni kwa kushirikiana na familia ya Dilunga wanaandaa taratibu za kuaga mwili jijini Dar es Salaam na maziko yanatarajiwa kufanyika mkoani Morogoro alikozaliwa katika siku itakayotangazwa na familia.

Alisema mwili utasafirishwa kesho kwenda Morogoro na kwa sasa msiba uko Kimara Stop Over kwa dada yake.

Mkurugenzi huyo ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alisema Dilunga aliajiriwa kwa nafasi ya mhariri na kampuni hiyo Februari Mosi, mwaka huu, na kabla ya hapo aliwahi kufanya katika magazeti la Raia Mwema na Mtanzania.

"Kwa muda mfupi aliofanya kazi Gazeti la Jamhuri, Dilunga amekuwa mtu wa msaada na ametoa mchango mkubwa katika kuboresha maudhui ya gazeti la uchunguzi. Hakika pengo lake ni vigumu kuzibika," alisema.

Alisema kampuni hiyo iliwashukuru wauguzi wa Hospitali ya Mwananyamala na Muhimbili, wahariri, waandishi wa habari, maofisa uhusiano, wanasiasa na watu mbalimbali ambao walifika kumjulia hali na kuomba mshikamano katika kipindi hiki cha kuhifadhi mwili wake.

Dilunga alizaliwa Oktoba 26, mwaka 1976, ameacha mjane na watoto watatu.

Msemaji wa serikali kupitia ukurasa wa Tweeter ya Msemaji Mkuu wa Serikali, alisema "Kwa niaba ya serikali nimepokea kwa masikitiko kifo cha mwanahabari Godfrey Dilunga. Nilimfahamu Dilunga kuwa mmoja wa wanahabari vijana, lakini aliyeipenda sana kazi yake na alijituma kuifanya kwa ukamilifu."

# Diwani amvimbia RC Mwanri

INATOKA UK. 2

"Hivi mkuu wa mkoa nimekaakaaje hasa? Yaani huu mkoa umenipwayapwaya, unanishindashinda, kama siuweziwezi hivi, wee! Hapa nitakuja na fukuafukua.

"Leo tutapiga kura hapa mtu akitajwa na watu 40, swali letu, ooh! Nimeonewa swali letu litakuwa ilikaakaaje ukatajwa na watu 40 wanaotoka maeneo tofauti? Tunataka mtutajie watu wote, siyo mliowaona, mnaowahisi tu."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa, akizungumza kwenye mkutano huo, alisema waliotajwa ni lazima wachukulie hatua za kisheria kwa kuwa kuna watu wananufaika na uhalifu.

"Kuna kina mama wanakula chakula cha uhalifu, anaweza kunenepa na akipata matatizo, anaacha kukumbuka mwanaye na kukumbuka vyakula alivyokuwa anakula," alisema.

Akiwa katika eneo la Bukene, Mwanri alisema atatembea nyumba kwa nyumba kukagua wageni wanaolala kwenye nyumba mbalimbali kwa kuwa uhalifu huanza kwa wenyeji kushirikiana na wageni.

"Katika maana ya amani na utulivu, kama hujitambulishi na kuorodhesha mgeni aliyekuja kwako, utaingia matatizoni,"alisema.

Mwanri alisema watatembelea nyumba za wageni na kuangalia majina yaliyoandikwa kwenye madaftari ya wageni kama yanaoana na majina ya vitambulisho vyao na maeneo wanayotoka.

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (kushoto), akifanya usajili upya wa laini ya simu kwa mfumo wa alama za vidole wakati alipotembelea banda la Tigo, wakati wa mkutano wa mawaziri (Tehama) wa nchi wanachama wa SADC, unaoendelea jijini Dar es Salaam juzi. Kampuni ya simu ya Tigo ni mtoa huduma ya WI-FI ya Bure katika wa mkutano huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kimbunga cha Majaliwa chakumba watumishi wanane

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewasimamisha kazi watumishi nane wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro na kuagiza wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni tatu za mapato ya ndani.

Amesema watumishi wa umma wanawajibu wa kufanya kazi kwa bidii, maarifa na ubunifu. "Nawasihi nyote muache kufanya kazi kwa mazoea, mbadilike na kuenenda sawa na matakwa na maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano na anayejiona hatoshi ajiondoe." Waziri Mkuu amewasimamisha kazi watumishi hao juzi wakati akizungumza na watumishi na madiwani wa Halmashauri ya wilaya ya Ulanga kwenye mkutano uliofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo uliopo mjini Mahenge.

Watumishi hao ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Yusuph Semguruka ambaye kwa sasa amehamishiwa TAMISEMI, Rajabu Siriwa (mwekahazina), Stanley Nyange, Jonson Mwenyembole, Isack Mwansokope, Said Majaliwa, Charles Steven na Hezron Lopa.

Pia, Waziri Mkuu alitumia kikao hicho kumrejesha kazini na kumpandisha kuwa mkuu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani, Agustine Mwaria, ambaye awali alikuwa akikaimu nafasi na kuibua ubadhirifu huo. Baada ya kuibua ubadhirifu huyo mtumishi huyo alisimamishwa kazi.

Majaliwa aliwataka watumishi hao wazingatie sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi pamoja na kujiepusha na vitendo vya wizi kwa sababu wanaoathirika baada ya wao kuchukuliwa hatua za kisheria ni wenza wao na watoto. Awali, Mkuu wa wilaya ya Ulanga, Ngollo Malenya, alisema wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya ubadhilifu wa fedha za umma hali inayosababisha kuwapo kwa mpasuko kati ya watumishi na Baraza na Madiwani. Alisema watumishi wanaotekeleza majukumu yao ipasavyo wanaandamwa.

# Kesi uhujumu uchumi dhidi ya hakimu yapigwa kalenda

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KESI ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi inayowakabili washtakiwa watano akiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Bernad Nganga, Mwanasheria wa hifadhi za Taifa (TANAPA), Maneno Mbunda na Mwanasheria wa Serikali, Fortunatus Mhalila, imepigwa kalenda kwa sababu ya kusubiri jalada kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP).

Akiomba kuahirishwa kesi hiyo mbele ya Hakimu Rose Ngoka wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Wakili wa Serikali Eliainenyi Njiro, alisema kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kutajwa japo upelelezi umekamilika.

"Mheshimiwa kesi hizi tunaomba tarehe nyingine sababu jalada bado lipo kwa DPP na upelelezi umekamilika," alisema.

Hakimu Ngoka alisema kesi hiyo anaiahirisha hadi Oktoba mosi, mwaka huu itakapotajwa tena.

Washitakiwa hao na wenzao Nelson Kangero na Tumaini Mdee mbali na mashtaka hayo, pia wanakabiliwa na mashtaka mengine tisa.

Awali, washitakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo Mei 6, mwaka huu na kusomewa mashtaka yao 11 na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Javelin Rugahuruza, yalikiwamo ya kujihusisha na rushwa,kughushi na kujipatia mali kwa njia ya rushwa kati ya Juni mosi, 2018 na Aprili 15, mwaka huu katika maeneo mbalimbali.

Mashtaka mengine walisomewa waliyotenda katika kipindi hicho ni kuchukua rushwa ya Sh. milioni 31.5 toka kwa Kangero, utakatishaji fedha ya Sh. milioni 31.5, kughushi nyaraka za uwongo za nyara ya Serikali za kilo 15 za meno ya tembo ya Sh. milioni 9.8.

Huku mshtakiwa Kangero akikabiliwa na shtaka la uhujumu uchumi kwa kukutwa na meno ya tembo vipande 15 vya thamani ya dola za Marekani milioni 15,000 (sawa na zaidi ya Sh. milioni 108) bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

# Agizo kutembelea wanufaika Tasaf

**Na Elizabeth Zaya,** KIBAHA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka viongozi wa halmashauri zote nchini kuanza kutembelea wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Alisema TASAF ni mpango wa serikali wa kunyanyua hali ya maisha ya wananchi wa hali ya chini kama lilivyo lengo la serikali ya awamu ya tano la kuwakomboa wanyonge, hivyo kunahitajika nguvu ya pamoja ya viongozi wote wa Halmashauri zote kuanzia Wakurugenzi na wataalam mbalimbali kuwatembelea wanufaika hao kuangalia miradi yao na kuwawezesha kielimu Dk. Gwajima alisema kumekuwa na kasumba ya viongozi wengi kuwaachia kazi peke yao TASAF makao makuu wakati lengo mahsusi la mfuko ni kuisaidia nchi na jitihada yake ya kupambana na umasikini

"TASAF ni kitu kimoja kikubwa na muhimu ambacho ni shirikishi, tumeshuhudia imefanya kazi kubwa ya kuwatoa Watanzania wengi katika hali ya chini kabisa ya umasikini na kuwafikisha katika hatua nzuri, kwa hiyo tunatakiwa kufanya kazi kama timu, bila hivyo tutakuwa tunakwamisha juhudi za Rais za kuwakomboa wanyonge," alisema Dk. Dorothy na kuongeza:

"Tunataka kila kiongozi katika kila eneo panapotekelezwa mradi, hususani wataalam katika nyanja mbalimbali za kilimo, ufugaji, afya na nyinginezo, kuhakikisha wanaenda vijijini kuwatembelea walengwa na kuwapatia elimu inayoendana na shughuli mbalimbali wanazozifanya katika maeneo yao."

"Tumeshuhudia wapo wanaolima, wanaofuga na wanafanya miradi mbalimbali kupitia kwenye vikundi vyao, na kwa kuwa lengo letu ni kutaka watoke katika hali ya umasikini, kwa nini tusishirikiane na kuwashika mkono, twende tukawape elimu ya mifugo yao isife, tuwape elimu ya kilimo, tusiwaachie TASAF makao makuu peke yao, kila mtu ajipangie ratiba ya kuwasaidia," Dk. Gwajima alimuagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Teresia Mbando, kumpatia ratiba ya viongozi katika eneo lake ambayo itaonyesha namna watakavyoanza kujipanga kuwatembelea walengwa wa TASAF kuwapatia elimu kuhusiana na shughuli mbalimbali wanazozifanya Mbando alisema mpaka sasa TASAF, imesaidia kwa kiwango kikubwa kunusuru kaya maskini, na kwamba ni vema kutanua mpango huo kwa kaya maskini ambazo zina hali mbaya kimaisha na ambazo hazijapata fursa ya kuingizwa katika mpango.

## Wajenga vyumba vya madarasa 450

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa** MUSOMA

WAKAZI wa jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, kwa kushirikiana na serikali na wadau wa maendeleo jimboni humo, wamefanikiwa kujenga vyumba vipya 450 vya madarasa ya shule za msingi na sekondari.

Wakati vyumba hivyo vimekamilika, ujenzi wa vingine 70 unaendelea, lengo likiwa ni kuhakikisha hakuna wanafunzi kusomea chini ya miti.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma, vyumba 350 ni vya shule za msingi na 100 vya sekondari.

"Shule za msingi hapa Musoma Vijijini zipo 111 za serikali na tatu za binafsi na pia zipo shule shikizi mpya 10 zinajengwa ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu," alisema Magoma.

Alifafanua kuwa kuna sekondari 18 za kata na mbili za binafsi, huku sekondari mpya nane zikiendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi na wadau wengine wa maendeleo ya elimu.

"Kwa ujumla ni kwamba kampeni ya kuondoa madarasa ya chini ya miti imekuwa na mafanikio makubwa, kwani tumedhamiria wanafunzi wote wanasomea katika madarasa, siyo chini ya miti, " alisema.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na juhudi za Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anney kwa kushirikiana na mkurugenzi wa halmashauri, John Kayombo.

Wanavijiji, mbunge, Profesa Sospeter Muhongo na wadau wengine wa maendeleo, wanashirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya elimu katika kata 21, vijiji 68 na vitongoji 374 vya jimbo letu," alisema.

# Mhudumu afya apekekwa jela mwaka mmoja kwa rushwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MHUDUMU wa afya wa Hospitali ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Lucia Thomas Mihayo, amehukumiwa kufungwa jela mwaka mmoja au kulipa faini ya Sh. 500,000, baada ya kukutwa na hatia ya kupokea rushwa ya Sh. 50,000, ili ampatie matibabu mgonjwa.

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Shinyanga, Husseni Mussa, alisema hukumu hiyo ilitolewa Septemba 12, mwaka huu na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Ushindi Swallo, baada ya kumkuta mhudumu huyo ana kosa la kuomba na kupokea rushwa. Alisema hukumu hiyo ilisomwa mbele ya Mwendesha Mashtaka wa Takukuru wilayani Kahama, Winfed Komba, ambapo mshtakiwa huyo alihukumiwa kwenda mwaka mmoja jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 pamoja na kurudisha fedha za rushwa Sh. 50,000 ambazo alizipokea. "Mshtakiwa huyu tulimfikisha mahakamani Mei 16, mwaka huu kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa Silas John Simon, ambaye alikuwa anamuuguza baba yake mzazi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kahama, ili kumpatia matibabu ndipo ukawekwa mtego na kufanikiwa kumkamata," alisema Mussa. "Baada ya kesi kuendelea kusikilizwa ndipo Mahakama ikamkuta ana hatia ya kosa la kuomba na kupokea Rushwa Sh. 50,000 kinyume na kifungu cha 15 (1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 katika kesi ya jinai namba 186 ya mwaka 2019, na kuhumkumu kufungwa jela mwaka mmoja au kutoa faini ya Sh.500,000," aliongeza.



Mafundi wakijiandaa kwaajili ya kukarabati taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua, katika Barabara ya Cameroon, eneo la Makumbusho, Kata ya Kijitonyama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Taboa yaipa jukumu Latra kutatua kero za wasafirishaji

**Na Yuster Prudence,** TUDArCO

CHAMA cha wamiliki wa Magari (Taboa), kimesema ni vyema Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), kujikita kutatua kero za wasafirishaji na usafirishaji kwa ujumla kabla ya kuongeza jukumu la kukusanya mapato.

Katibu Mkuu wa Taboa, Enea Mrutu, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa mkutano kati ya wadau hao kujadili kanuni za sheria ya usafirishaji.

Alisema kuna kero nyingi katika sekta ya usafirishaji ikiwemo tozo mbalimbali ambazo siyo rafiki kwao hivyo aliwaomba Latra wafute tozo hizo ili kodi ibaki kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Tunawaomba Latra wabaki kwenye jukumu lao la kutoa leseni na siyo kukusanya mapato ya faini mbalimbali kama wanavyotaka kufanya. Hatuna mgogoro na ukataji tiketi kwa mtandao wanachohitaji ni utaratibu kufuatwa," alisema.

Naye, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Johansen Kahatano, aliwatoa wasiwasi wamiliki wa mabasi kwa kuahidi kutatua kero mbalimbali zinazowakabili katika shughuli zao za usafirishaji.

Aidha, wamiliki wa mabasi kupokea sheria mpya zilizowekwa wakati jitihada za kupata utaratibu mpya ukiendelea.

Kwa mujibu wa Kahatano, Bunge ndio chombo chenye mamlaka ya kufanya kazi maoni waliyotoa pamoja na wizara husika ambayo ndiyo yenye maamuzi ya mwisho, hivyo kero zao zitafika moja kwa moja kwa wahusika na baada ya mapendekezo hayo kutolewa maamuzi watajulishwa.

"Kero zote zitawafikia wahusika hasa Bunge ambacho ndicho chombo chenye mamlaka ya kufanyia kazi maoni yenu, lakini pia katika wizara husika ambayo ndiyo yenye maamuzi ya mwisho na baada ya mapendekezo yenu kutolewa maamuzi mtajulishwa," alisema Kahatano.

Aidha, alithibitisha kuwapo na malalamiko ya wadau wa sekta ya usafirishaji juu ya kutumika kwa mfumo wa ufatiliaji wa magari (VTS) unaosemekana kuwa siyo rafiki kwa wamiliki hao na kudai kuwa mfumo huo ni sehemu ya gari kama sehemu nyingine na kazi ya kifaa hicho ni kudhibiti mwendokasi.

"Mfumo wa VTS ni sehemu ya gari kama sehemu nyingine kazi yake ni kudhibiti mwendo wa gari na ndio maana madereva wengi hawakubaliani nao kwasababu wanavunja baadhi ya kanuni za usalama barabarani, ifike wakati tukubaliane kuwa sote tuna lengo moja hivyo tushirikiane katika kutoa huduma bora na salama kwa wananchi," alisema Kahatano.

Aidha alieleza kwa kile kilichosemekana kuwa wadau wanashirikiana na kituo cha Taifa cha Utunzaji wa kumbukumbu (NIDC) ili kutoa tozo kwa wamiliki wa mabasi na kusema kuwa wadau waliotafutwa na LATRA ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na siyo NIDC wao wamepewa maagizo na Waziri wa Uchukuzi.

Naye, Mtaalam wa mifumo ya kutunza kumbukumbu, Cathbeth Simalengo, alieleza baadhi ya faida za mfumo wa kielektroniki ambao utakua unatumika kukata tiketi kwa njia ya mtandao kuwa ni pamoja na kuongeza kipato kwa wamiliki, kuweza kukata tiketi kokote utakapokuwa.

Alisema pia itasaidia mmiliki kujua wakina nani wamepanda gari lake na pia mfumo huo utarahisisha ukusanyaji wa mapato.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mpaka sasa mfumo uko tayari kiufundi na mfumo wao utakua ni wa gharama nafuu kuliko mifumo mingine yote ambapo hela za watu watakao kata tiketi zitaingia moja kwa moja katika akaunti za wamiliki wa magari hayo na hivyo usajili wa wamiliki utaanza hivi karibuni.

Naye Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Mkada Mkada, aliishukuru Taboa kwa mkutano huo na kuwataka watekeleze yale yote yaliyojadiliwa kwa ushirikiano.

# H/shauri yafagiliwa utekelezaji miradi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga, ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Jiji la Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kutembelea miradi ya vituo vya afya na hospitali ya wilaya, Nyamhanga alisema ameridhishwa na ujenzi wa miradi hiyo iliyokidhi ubora na viwango vinavyotakiwa.

Alisema halmashauri hiyo, imesimamia na kutekeleza miradi hiyo kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani, jambo ambalo linapaswa kuigwa na kuwa mfano kwa halmashauri nyingine hapa nchini.

Aliongeza kuwa Jiji la Arusha limekuwa la kwanza nchini kutekeleza miradi mikubwa kwa kutumia fedha za ndani, pia limepiga hatua kubwa ya kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kujenga vituo vya afya na zahanati kwenye kila kata na wilaya. Alimpongeza Mkurugenzi wa Jiji, Dk. Maulid Madeni, na Meya Kalisti Lazaro, kwa usimamizi wao makini na kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi za Serikali za huhakikisha wananchi wanapata huduma

"Kwa hatua hii naagiza majiji na halmashauri zote nchini kuiga Jiji la Arusha katika ujenzi wa miradi ya afya na ununuzi wa vifaa tiba kwa kutumia fedha za ndani," alisema Nyamhanga.

Katika ziara hiyo Mkurugenzi wa Jiji hilo, alisema kupitia mapato ya ndani wamefanikiwa kujenga hospitali ya wilaya eneo la kata ya Engutoto, Njiro na imeanza kutoa huduma ya chanjo na wanatarajia kufunga mashine za kisasa hivi karibuni kwa ajili ya kutoa huduma za matabibu.

Alisema wataendelea kusimamia na ukukusanya mapato ya ndani na kukamilisha ujenzi wa vituo katika kata mbalimbali za Jiji la Arusha kikiwapo Kituo cha Afya Moshoni kilichokuwa hatua ya mwisho kukamilika.

Meya wa Jiji la Arusha, Calist Lazaro, alisema halmashauri hiyo inaunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha kila kata inapata kituo cha afya kwa lengo la kupunguza na kuondoa changamoto kwa wananchi kufuata huduma hizo kwa kutembea umbali mrefu.

Hata hivyo, alisema hospital mpya za Kata ya Engutoto, Muriet na Moshono zinakabiliwa na uhaba wa watumishi hivyo ameiomba wizara ya afya kufanya utaratibu wa kuwapatia watumishi wapya kwani wastani wa kila hospital ya wilaya na vituo vya afya ni watumishi 50, na vituo hivyo hadi sasa vina watumishi 25, tu wanaotoka kwenye vituo mbalimbali jijini Arusha kwenda kutoka huduma ya matibabu.

Bado mahitaji ni makubwa kwani vituo hivyo vina watumishi wapatao 25 tu wanaotoka vituo mbalimbali vya Jiji la Arusha.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Daniel Ole Materi, akizungumza kwenye kikao cha viongozi wa tarafa ya Terrat, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mbunge ashauri kumtolea Mungu

**Na Zanura,** ARUMERU

WANANCHI Mkoani Arusha, wametakiwa kujitolea kwa mali na vitu walivyonavyo kwa ajili ya kumtumikia Mungu ili waendelee kubarikiwa.

Rai hiyo, ilitolewa na Mbunge viti Maalum wa Jimbo la Arumeru Magharibi, Amina Mollel, wakati wa harambee ya umaliziaji wa jengo la Ibada katika Kanisa Katoliki Kigango cha Lengijave wilayani Arumeru, mkoani hapa.

Katika harambee hiyo jumla ya Sh. milioni 100, zilikuwa zinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa nyumba hiyo ya ibada.

Viongozi wengine walioshiriki katika harambee hiyo ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha na baadhi ya viongozi wa dini kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha.

Katika harambe hiyo, Jumla ya Sh. milioni 14 zilipatikana ahadi ikiwa ni Sh. millioni 7 .

Kundi la mtandao wa kijamii la "Watsap" la Masai Famili Tanzania na duniani kote, pia walijitokeza katika harambee hiyo na kutoa michango yao.

Alimuomba Nasha mchango wake kwa ajili ya kutatua changamoto katika shule mbili ya Lengijave na Olback zilizopo wilayani humo.

Alizitaja changamoto hizo ni uhaba wa vyumba vya madarasa, mabati kuchakaa, uchakavu wa sakafu pamoja na uhaba wa matundu ya vyoo vya wasichana na wavulana.

Nasha aliahidi Sh. milioni 42 kwa ajili ya kujenga darasa moja kwa kila shule na choo kimoja kwa kila shule.

# Watumishi Umma watakiwa kuzingatia sheria na kanuni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Arusha DC, Wilayani Arumeru mkoani hapa, Dk. Wilson Mahera, amewataka watumishi wa halmashauri hiyo, kufanya kazi kwa bidii, ushirikiano na kuzingatia sheria kanuni na taratibu ili kufikia malengo yaliyooanishwa kwenye mpango mkakati wa halmashauri hiyo.

Rai hiyo, aliitoa jana alipokutana na watumishi wa sekta zote za halmashauri hiyo, katika kikao kazi cha kawaida, kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuwakumbusha watumishi wajibu na majukumu yao ya kila siku pamoja na kuwajengea uwezo na uwajibikaji na kutatua changamoto zinazowakabili ili kufikia malengo ya serikali ya kuwahudumia wananchi.

Alisema watunishi hao wanapaswa kutambua kuwa utumishi wa umma ni dhamana waliyopewa na serikali, hivyo aliwataka kufanya kazi, kwa kuzingatia kanuni, sheria, taratibu za utumishi wa umma pamoja na miongozo ya serikali, kwa taaluma zao katika kutekeleza majukumu yao. "Serikali imewaamini na kuwapa dhamana ya kuwatumikia wananchi, tumieni taaluma zenu kutekeleza majukumu yenu, tushirikiane kama timu ili kuijenga Arusha DC na Serikali yetu kwa ujumla," alisema Mahera.

Aliwaagiza maofisa watendaji wa kata kusimamia suala la usafi wa mazingira na kuhakikisha wananchi wanatozwa tozo stahiki za taka na kupewa risiti za fedha walizolipia, sambamba na kuwachukulia hatua za kisheria, wananchi ambao wanakaidi maagizo na miongozo ya serikali.

Mkuu wa Idara ya Utumishi, Halmashauri ya Arusha DC, Hamis Mpume, aliwaahidi watumishi hao kuendelea kusimamia haki zao, wajibu na usawa, lakini aliwakumbusha watumishi hao kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja na kutekeleza wajibu wao.

"Nina imani kila mtumishi anafahamu vizuri majukumu yake, natoa wito kila mtumishi atekeleze kazi zake kwa ufanisi, naahidi kutenda haki kwa kila mtumishi, sitamuonea mtu yeyote lakini sitasita kumchukulia hatua stahiki mtumishi asiyetekeleza majukumu yake," alisema Mpume. Ofisa Mtendaji Kata ya Mateves, Muyai Kivuyo, alimshukuru Mkurugenzi wa halmashauri hiyo kwa kukaa pamoja na watumishi kujadili changamoto zinazowakabili.

Hata hivyo, walimuomba mkurugenzi huyo kuwapa taarifa za shughuli za miradi ambayo inaendelea katika kata zao ili wafahamu na waweze kushirikiana kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo.

# Aficha sare kuzuia mwanawe asisome

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWANAFUNZI wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Sumaye iliyoko Mabogini mkoani Kilimanjaro, anadaiwa kukatishwa masomo kwa miezi nane baada ya mzazi wake kuficha sare zake.

Mwanafunzi huyo wa miaka saba (jina tunalo) ambaye shule yake iko katika kata ya Mabogini, anadaiwa kukatisha masomo yake kwa miezi zaidi ya nane, baada ya baba yake mzazi kuficha sare zake.

Inaelezwa kuwa baba wa mtoto huyo (jina tunalo), alificha nguo za shule za mwanae akitaka asiendelee na masomo ili amsafirishe kwenda kijijini kwao, Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga kumsaidia bibi yake kazi za nyumbani.

Kufuatia kisa hicho, wawezeshaji ndani ya jamii wanaofanya kazi chini ya shirika la kirai la Tusonge, wamemuokoa mtoto huyo na kumrejesha shuleni.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya kumbana baba mzazi na kukubali kuzitoa sare za shule alizozificha tangu mwezi Januari mwaka huu.

Akizungumzia mkasa huo jana, mwezeshaji wa ndani ya jamii wa Tusonge, Anna Karonge, alisema mtoto huyo aliandikishwa darasa la kwanza mwezi Januari mwaka huu, lakini hakuwahi kwenda shule hata siku moja.

"Tulimuuliza mtoto kwa nini haendi shuleni, akajibu baba yake alificha nguo zake za shule na kumueleza kuwa anataka kumpeleka Tanga akamsadie bibi yake kazi za nyumbani na kuchunga mifugo,"alisema Karonge

Zaidi aliongeza: "Huyo baba alificha nguo za shule kuanzia Januari hadi juzi, tulipokwenda kufuatilia kesi na kupata sare za mtoto huyo na akarejea shuleni kuendelea na masomo. Ingawa atakuwa ameachwa nyuma na wenzake."

Aidha, Mratibu wa Mradi wa Paza Sauti, Tokomeza Ukatili unaotekelezwa na Shirika la Tusonge, kwa kushirikiana na Foundation For Civil Society, Joyce Kessy, alisema jitihada zote hizo zilifanywa na Tusonge.

Alisema walifanya kwa kuwa ndiyo waliotoa elimu kuhusu kuacha ukatili ndani ya jamii na ikaunda kundi la watu ambalo lina jukumu la kufuatilia kesi za aina hiyo. Mradi huo wa Paza Sauti, Tokomeza Ukatili unatekelezwa kwa kipindi cha miezi nane, kuanzia Julai 2019 na Machi 2020.

"Mtoto huyo sasa anapata haki yake ya elimu na anafurahi na wenzake, hata hivyo bado ufuatiliaji wa karibu unaendelea, kwa sababu tunaamini baba anaweza kuzua jambo jingine ili kumzuia mtoto asiende shule.

Kwa vile anaweza akamsafirisha kimya kimya kwenda Tanga, ingawa tunawasiliana na Mtendaji wa Kata pamoja na kijiji hicho ili wampe onyo kali na atakaporudia tena, basi sheria ichukue mkondo wake,"alisisitiza Joyce



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo (katikati), akisaini mkataba wa utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe ngazi ya jamii, wilayani humo, mkoani Kilimanjaro jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Masama Mashariki, Eliwario Munuo na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Upendo Wella. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Milioni 30 kutumiwa kukabili udumavu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KATIKA jitihada za kupambana na udumavu miongoni mwa watoto wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, halmashauri, imetenga Sh. milioni 30 kukabili tatizo hilo.

Hatua hiyo inachukuliwa wakati takwimu za afya zikionyesha udumavu wa watoto Hai unafikia asilimia 29.

Katika kupambana na tatizo hilo, zaidi ya Sh. milioni 30 zitatumiwa kuboresha utendaji kazi na usimamizi wa lishe katika ngazi ya jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alisema wataanza kwa kutoa elimu kwa jamii, kupitia viongozi wa ngazi za vijiji na mitaa yote.

Alikuwa akizungumza jana na watendaji wa kata 17, watendaji wa vijiji, timu ya uendeshaji huduma za afya ya wilaya na wakuu wa idara, wakati wa kusaini mkataba wa utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe ngazi ya jamii.

"Naomba tusifanye mchezo na jambo hili , tupambane kwa nguvu zetu zote, kwa sababu hili ni agizo la Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo.

"Hizo fedha zimetengwa katika bajeti ya 2019/2020 kwa ajili ya kusaidia ufuatiliaji na utoaji wa elimu ya lishe. Tunataka jamii nzima ya wilaya yetu iwe na afya njema na iondokane na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora." Alisema Sintoo.

Aliwaambia watendaji wa kata wasikae na nyaraka za kazi ofisini, wazisome na kutekeleza mkataba huo.

Awali, mwenyekiti wa kamati ya uendeshaji wa huduma za afya ya wilaya ambaye pia ni Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Irene Haule, akitoa taarifa kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai (DAS), Upendo Wella, kuhusu kutia saini mkataba huo alisema vipo vigezo vya upimaji.

Alisema vimewekwa vigezo vya upimaji kati ya Mkurugenzi Mtendaji (DED) na maofisa watendaji wa kata (WEO's).

Wakati Ofisa Lishe wa Wilaya hiyo, Silvania Kullaya, akiwasilisha mada kuhusu mkataba wa utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe ngazi ya jamii alisema pia ukondefu wa watoto chini ya miaka mitano katika wilaya hiyo ni asilimia 3.1 na kitaifa ni asilimia tano.

Kwa mujibu wa Kullaya, uzito pungufu kwa watoto wachanga wilayani humo kwa sasa ni asilimia 10 na upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa (15-49) ni asilimia 29.1 na uzito uliozidi ni asilimia 22.

Hata hivyo, kabla ya kutia saini mkataba huo, Katibu Tawala wa Wilaya , Upendo Wella, aliwasihi watendaji hao kuzingatia maelekezo yaliyomo katika mkataba pamoja na maelekezo ya Makamu wa Rais aliyoyatoa Agosti 2017 katika mkutano wa kimataifa wa urutubishaji vyakula.

"Kutokana na hali ya lishe kuwa mbaya na udumavu kufikia asilimia 34 kitaifa kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano, Makamu wa Rais aliagiza kuwapo na mkataba wa usimamiaji wa shughuli za lishe kati yake na wakuu wa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, hivyo mpambane kwa sababu mkuu wetu wa mkoa naye atapimwa kwa maelekezo haya,"alisisitiza Wella.

## Wazururaji 100 wajipatia ajira

**Na Mary Mosha,** SAME

ZAIDI ya vijana 100 wa kata ya Saweni wilayani Same mkoani Kilimanjaro waliokuwa wazururaji , wameachana na 'shida' hiyo baada ya kuajiriwa na kiwanda kipya kilichoanzishwa wilayani humo.

Walinufaika na neema ya ajira baada ya mfanyabiashara mmoja kujenga kiwanda cha kutengeneza bidhaa za nyumbani.

Kiwanda hicho kinachotengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni na mishumaa, kimeajiri idadi kubwa ya vijana.

Taarifa ya menejimenti iliyowasilishwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia uwekezaji, Angellah Kairuki, inaeleza kuwa kuanzishwa kwa kiwanda hicho ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya serikali ya kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alithibitisha kuwa vijana hao walikuwa wakitumia vibaya muda kwa kucheza kamari, kuzurura na kukaa vijiweni, kwa sasa wamepata ajira na wanaweza kukabiliana na gharama za maisha.


Katika taarifa hiyo, ilielezwa kuwa vijana hao wamemweleza Waziri Kairuki kwamba kutokana na mazoea ya familia za Kiafrika, walikuwa wakisubiri ajira serikalini na walijua ajira za sekta binafsi haziwafai, kwa sababu kuna urasimu katika kupata kazi.

"Pamoja na fursa ya ajira tuliyoipata katika kiwanda hiki bado tunakabiliwa na changamoto ya ukosefu ya umeme katika kiwanda hicho, tunaomba serikali kututazama kwa jicho la pekee ili tuweze kuzalisha bidhaa zinazohitaji umeme," alisema Eva Mbwambo

Akiwa Wilaya ya Same, Waziri Kairuki aliahidi kuwasiliana na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani ili Wakala wa Umeme Vijijini (REA) aweze kuharakisha upelekaji wa nishati hiyo katika kata ya Saweni.

Alisema kukosekana kwa umeme katika eneo hilo la mradi, ni sawa na kufifisha juhudi za serikali katika sekta ya viwanda.

Aidha, Waziri Kairuki aliitaka menejimenti ya kiwanda hicho kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinakuwa na ubora unaozingatia viwango vya Shirika la Viwango nchini (TBS) ili ziweze kumudu ushindani wa soko huru.



Ukurasa 14

**JPM ameshinda mtihani kivitendo na kuliishi 'neno'**

Mawakili walalamika kutoruhusiwa kumuona Waziri



Ukurasa 17

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 18, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 19

**Mzee Mugabe; Mpigania uhuru aliyekumbukwa kabla hajafa**



Ukurasa 20

**Mahakama Uingereza zasutana majaji kuzuia Brexit Oktoba 31**

# Chadema: Upinzani kurejesha wabunge wengi uchaguzi ujao

- Ubabe unaoendelea ni sehemu ya siasa
- Sifa mgombea Chadema serikali za mitaa ni uadilifu
- Kesi ya Lissu imeonyesha Mahakama haziko huru

**Na Enock Charles**

TANZANIA inatarajiwa kufanya uchaguzi wake wa Serikali za Mitaa, Novemba mwaka huu na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwaka ujao.

Kwa hivi sasa vyama vya siasa viko katika maandalizi kwa ajili ya kuibuka na ushindi kwenye ngazi mbalimbali za chaguzi hizo.

Nipashe kupitia kwa Mwandishi wake ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji kuhusiana na mambo mbalimbali lakini zaidi chaguzi zijazo nchini. Fuatilia sehemu ya kwanza ya mahojiano hayo:

**SWALI: Mmejipanga vipi kuhusiana na uchaguzi wa Serikali za Mitaa?**

**JIBU:** Uchaguzi wa Serikali za Mitaa huwa ni local election na unahusika sana na wenyeji wa eneo husika mahalia. Sisi kama chama cha siasa kwa ngazi ya

INAENDELEA UK.16



Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vicent Mashinji. **PICHA: MTANDAO**

**Rais Magufuli na mapambano ya ukombozi wa pili kiuchumi** Ukurasa 18

# JPM ameshinda mtihani kivitendo na kuliishi 'neno'

## • Nape na wenzake ni darasa



Rais John Magufuli (kushoto), January Makamba (katikati na William Ngeleja. **PICHA: MTANDAO**

**Joseph Muhozi**

BINADAMU ameumbiwa mitihani mingi, lakini moja kati ya mitihani hiyo ni kupewa uwezo wa kuhisi maumivu na hasira huku akiagizwa na Muumba wake kumsamehe anayemkosea na kumuombea mema adui anayepanga kumdhuru.

Huenda mtihani huu ndio uliosababisha mpigania uhuru wa India aliyefanikiwa, mmoja kati ya wanafalsafa ambao fikra zao zinaishi ingawa miili yao imelala, Mahatma Gandhi kusema, "watu dhaifu hawawezi kusamehe, kusamehe ni kielelezo cha tabia ya watu imara".

Lakini falsafa hiyo ya Gandhi itaongezwa nguvu kwa mtu ambaye anasamehe si kwa sababu hana namna ya kumuadhibu aliyemkosea, bali ana mamlaka yote na nguvu za kumuadhibu lakini ameyavumilia maumivu na kumsamehe aliyemuumiza.

Hivi karibuni, Rais John Magufuli ameonyesha uimara wa hali ya juu, akiwasamehe watu ambao wameonekana au kusikika hadharani, wakimkashfu au kumtukana.

Licha ya kuwa na nguvu kubwa anayopewa na Katiba ya Nchi kama Rais na Amiri Jeshi Mkuu, amejishusha akawakumbatia waliomtukana na kuwasamehe, ingawa amekiri kweli 'inauma'.

Septemba 4, 2019, Rais Magufuli alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa pamoja wa wahandisi na wasanifu majenzi jijini Dar es Salaam, aliweka wazi kuwa amewasamehe Januari Makamba na William Ngeleja ambao walimtukana na akajiridhisha kwa asilimia zaidi ya 100 kuwa walitenda kosa hilo.

> Katika Quran Takatifu pia, inaeleza jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu anampenda mtu anayeweza kudhibiti hasira zake na kuwasamehe wenzake (Quran: Surah Al-e-Imran, Ayat 133-134).

Kumbuka mmoja alikuwa Waziri katika awamu yake na mwingine amewahi kuwa waziri katika serikali zilizopita.

Kama hiyo haitoshi, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye naye alipokea msamaha wa Rais Magufuli kwa kosa hilo hilo, kumtukana.

Alimualika Ikulu, akamsikiliza, akamsamehe hadharani na zaidi akampa ushauri wa namna ya kupiga hatua kwenye maisha yake ya kisiasa.

Akamtia moyo na kumuondoa wasiwasi! Hii ni ishara kuwa Rais Magufuli amefanikiwa kuushinda mtihani ule wa binadamu, ameonyesha uimara na kuishi maandiko ya Mungu anayoyasoma, ingawa anakiri inauma.

"Inauma, kusamehe kunaumiza lakini ninasema kwa dhati kabisa kwamba nimemsamehe," alisema Rais Magufuli alipokuwa akitangaza msamaha wake.

Katika Biblia Takatifu, neno 'msamaha' kwa lugha ya Kigiriki limeandikwa zaidi ya mara 146, na kwenye Quran Takatifu msamaha umetajwa zaidi ya mara 100 na rehema takriban mara 200.

Hii inaonyesha jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu anasisitiza kusameheana. Ni maneno matatu makuu yanaweza kuiokoa dunia nzima, 'msamaha, upendo na rehema'.

"Unisamehe makosa yangu, kama ninavyowasamehe walionikosea." Huu ndio mstari wa Biblia Takatifu, unaopatikana kwenye sala maarufu ya 'Baba Yetu' aliyoifundisha Yesu Kristo kwa wanafunzi wake, mstari ambao Rais Magufuli alieleza kuwa aliutafakari alipokuwa anausema anaposali na akaamua kuwasamehe Makamba na Ngeleja.

Je, kukasirika ni dhambi? La hasha, kukasirika si dhambi kwani hata Mwenyezi Mungu hukasirika.

Watu humuudhi Mungu, na watu huudhi watu, lakini Mungu aliyesema hata kama dhambi zako ni nyekundu kama bendera zitakuwa nyeupe kama theruji atakapokusamehe, anatutaka tuishi hivyo katikati ya maudhi na hasira.

Lakini matunda ya hasira yanaweza kuwa dhambi. Biblia inasema, "kuweni na hasira lakini msitende dhambi, jua silichwe na uchungu wenu bado haujatoka (Waefeso 4:26)."

Katika Quran Takatifu pia, inaeleza jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu anampenda mtu anayeweza kudhibiti hasira zake na kuwasamehe wenzake (Quran: Surah Al-e-Imran, Ayat 133-134).

Ni dhahiri Rais Magufuli alikasirika sana kusikia sauti za walivyokuwa wakimsema kwa lugha za ukakasi, lakini ameamua 'jua lisichwe akiwa hajatoa uchungu wa maumivu'.

Ukiacha mbali kusamehe saba mara sabini kama alivyoeleza Bwana Yesu Kristo, Mwenyezi Mungu anatuagiza kusamehe na kusahau.

Rais Magufuli ameonyesha hilo, amewasamehe Nape, Makamba na Ngeleja, amesahau na amemueleza aliyekuwa amemkosea njia bora zaidi ya kufanikiwa.

Ameonyesha kuwa hajabaki na chembe ya kinyongo, tena amemualika Ikulu kwa heshima kama mgeni wake wa heshima na sio mtu anayetaka kumpigia goti.

Mwanafalsafa mmoja alisema, "dunia ingekuwa sehemu salama zaidi ya kuishi kama watu wangekuwa wanasameheana."

Hata hivyo, Nape, Makamba na Ngeleja ambao walikosea wametufundisha somo kubwa la wazi.

Kwanza, kukosea tumeumbiwa binadamu. Hata Petro ambaye alipewa hadhi na Yesu kuwa ndiye 'Jiwe' ambalo juu yake atajenga kanisa lake, alimkosea Yesu lakini alipojuta na kutubu alisamehewa.

Marehemu Bluce Lee, Mfalme wa Karate, aliwahi kusema, "Makosa husamehewa daima, kama mkosaji atakuwa na ujasiri wa kuyakiri."

Makamba, Ngeleja na Nape walikuwa na ujasiri wa kuyakiri makosa yao na kuomba msamaha kwa dhati.

Nape amekuwa funzo zuri, ni kama Mungu amemtumia pia kutukumbusha binadamu sio tu kuomba msamaha, kuitafuta kwa dhati nafasi adhimu ya kuomba msamaha kwa tuliowakosea.

"Nape amekuwa akiomba msamaha, akiandika messages (jumbe) hata usiku wa manane, alikuwa anaomba anione... anione. Hata wasaidizi wangu wamekuwa wakiliona hili," amesema Rais Magufuli.

"Amehangaika sana, ameenda hadi kwa Mzee Mangula [Philip Mangula], amefika mpaka kwa Mama Nyerere, amehangaika kweli lakini baadaye... ni katika hiyohiyo kwamba sisi tumeumbwa katika kusamehe. Na leo umemuona asubuhi amekuja hapa, nikaona siwezi kumzuia kuniona, kikubwa anachozungumza ni 'naomba Baba unisamehe'," ameongeza Rais Magufuli.

Wengine wasio na busara wameeleza utetezi wa kufunika makosa kuwa eti makosa yale yalifanywa kwenye faragha hivyo aliyeyafichua ndiye mkosaji!!

Wanasahau kuwa hata Mungu wetu anajua kuna faragha, na Mungu pia yuko sirini. Lakini kuwa sirini hakumpi mtu yeyote ruhusa ya kufanya makosa.

Kosa ni kosa haijalishi umelifanya kwa mazingira yapi, muhimu ni kukiri, kujuta na kuomba msamaha kama walivyofanya.

Kufanya kosa hakukuondolei hadhi yako endapo utakiri, kujuta na kuomba msamaha bali litabaki kuwa fundisho kwa wengine.

Mfano, katika Biblia, Mungu alimfanya Mfalme Daudi kuandika makosa yake mwenyewe na hadi leo tunayasoma. Aliyafanya, alikiri, akajuta, akatubu na akasamehewa na akabaki kuwa ni mteule wa Mungu.

Kwa haya yaliyotokea ni dhahiri Rais Magufuli ameyaishi maandiko matakatifu na ameongoza kwa mfano. Tuendelee kumuombea.

Tupo wengine huku mtaani, mbavu mbili tu na hata uongozi wa darasa hatujawahi kupata lakini tunavyopania kulipa visasi ni kama tuna mkataba na shetani.

Tujifunze kwa rais wetu, vitabu vyote vitakatifu vinaelekeza kusamehe na kuepuka visasi.

***Mwandishi anapatikana kwa namba 0754-999541***

# Waingereza wachekelea uwanja mtupu ibada mazishi ya Mugabe

Na Michael Eneza

VYOMBO vya habari nchini Uingereza na kwenye mitandao kwa jumla vilikenua kwa uwazi na raha zao kutokana na uhaba wa waombolezaji Uwanja wa Taifa jijini Harare ambako ibada ya kuuaga mwili wa kiongozi mkuu wa Zimbabwe, Robert Mugabe ilifanyika Jumamosi.

Gazeti la Daily Telegraph ambalo kimsingi linaendana na hisia za chama tawala cha kihafidhina, Conservative liliandika "viti vitupu vyampa Robert Mugabe heshima za mwisho alizostahili" ibada ya mazishi kitaifa.

Likasema walikuja kwa maelfu, lakini siyo kama ilivyotazamiwa kwa makumi ya maelfu, na kuongeza kuwa ndege za kijeshi zilipita juu kwa heshima yake, ila zilikuwa sita tu. Yote ni kuainisha umaskini na kutopendwa Mugabe.

Waandishi wa gazeti hilo London na Harare walisema kuwa ibada hiyo ilikosa hamasa, ya msukumo hafifu ukionyesha hisia kinzani zinazomzunguka mgombanishaji huyo mkuu miongoni mwa viongozi wa Afrika.

Ilikuwa ni 'nenda salama' stahili kwa mtu ambaye mafanikio yake kama shujaa wa ukombozi wa Afrika na baba wa taifa la Zimbabwe milele yatakuwa na doa kwa urithi wa kukwama kwa uchumi, kutengwa kimataifa na utumiaji mabavu kisiasa.

Ni kielelezo cha upande wa pili wa utawala wa Mugabe hadi kuelekea mwisho wa 2017, ila kukosekana watu ilikuwa vile vile kumpuuza mrithi wake, Emmerson Mnangagwa ambaye alishirikiana na jeshi kumpindua Mugabe, mkewe Grace akiwa anajiandaa kumrithi.

Waandishi walisema kuwa uwanja huo wenye uwezo wa kuketi watu 60,000 ulifikia takriban theluthi moja ya uwezo wake, ikiwa zaidi ni viongozi wa kisiasa na makamanda wa jeshi la nchi hiyo, kundi dogo kiasi la wageni kutoka nje na wanafamilia wa marehemu ambao walitoa heshima za mwisho kwa Mugabe.

Ilikuwa ni hafla iliyochukua saa tano, huku Rais Mnangagwa akionekana kupata tabu kidogo akimsifia mtu ambaye alimsaliti na kumpindua kama "tunu ya mapinduzi, kiongozi, kamanda wa vita vya ukombozi na rais aliyepita," kwa mujibu wa gazeti hilo.

Alijitahidi pia kuonyesha hisia ya shukrani na heshima kwa Grace Mugabe, mjane wa kiongozi huyo ambaye ni adui yake wa kwanza kisiasa, na ambaye alikaa kimya katika hadhara hiyo, asiseme neno lolote mwanzo hadi mwisho, ana shela nyeusi usoni.

Waliofika kumuaga Mugabe kutoka nchi kadhaa za Afrika pia walionyesha mchanganyiko huo wa hisia kama si mkanganyiko, iwe ni kwa watu waliokuwapo hapo au waliokuwa wakifuatilia hadhara hiyo nchini humo, kwingineko Afrika na maeneo mengine duniani.

Mmoja ni Teodoro Obiang Nguema Mbasago, dikteta wa Equatorial Guinea anayeendesha utawala wa mafisadi tangu 1979, alikuwa wa kwanza kutoa heshima kwa Mugabe kama 'tunu halisi ya Afrika katika ukombozi wa bara hili kutoka ukoloni.'



Mzee Robert Mugabe akiwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, Margaret Thatcher. **PICHA: MTANDAO**

> Yuko mwanamke mmoja aliyetajwa kwa jina la Fadzai Mutasa, mkazi wa Harare mwenye umri wa miaka 42 aliyesema kuwa wakati Mugabe anaondolewa, mikate ilikuwa inauzwa dola mbili (za Marekani) na chakula, usafiri watu walikuwa wanamudu.

Jerry Rawlings, mtawala wa kijeshi wa zamani nchini Ghana aliyeikubali demokrasia, alisema Mugabe 'alionyesha dhamira isiyotetereka kutetea taswira ya Afrika tunayoitaka.'

Serikali za China na Russia ziliwapa mabalozi wao jukumu la kutoa wasifu wa kiongozi hiyo, siyo kupeleka viongozi wa juu.

Kundi la watazamaji, licha ya kutokujaza uwanja lilipaza sauti zao kwa nguvu zaidi dhidi ya Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini ambaye alizomewa muda wote wa hotuba yake hadi alipoomba radhi kwa mashambulizi na mauaji ya wafanyakazi kutoka nje ya Afrika Kusini.

Maelfu ya raia wa Zimbabwe walihamia huko miaka iliyopita kutafuta kazi, na wamekuwa wakishambuliwa kwa nguvu pamoja na wahamiaji kutoka Malawi, Somalia na Nigeria, na wengine kadhaa. Alipoomba radhi, watazamaji wakabadilika wakaanza kushangilia, hatua iliyoonekana kuridhisha umati huo, kuondokana na mabaya.

Kulikuwa na kupigwa mizinga 21 ya heshima na askari wa mizinga wa jeshi hilo. Na ndege sita za kijeshi zilisisimua kwa kupita kwa kasi angani, kabla ya hafla hiyo kumalizika.

Hapakuwa na maelezo kuhusu kupigwa kwa wapinzani katika maandamano, au maelfu ya waliokufa katika Operesheni Gukurahundi.

Waandishi wa Telegraph pia waligusia kuwa hakuna kilichozungumzwa kuhusu operesheni hiyo ya miaka ya 1980 au jinsi ilivyoanza, kugunduliwa kwa silaha katika shamba la kiongozi wa upinzani, mkongwe Joshua Nkomo aliyekuwa na muungano dhaifu wa vyama vya ZANU na Patriotic Front, na Mugabe.

Pia walikumbusha kuwa miaka iliyofuatia kunyang'anywa mashamba Wazungu na kuharibika uchumi wa Zimbabwe, familia ya Mugabe ilijikusanyia utajiri mkubwa huku wananchi wanahangaika.

Wakizungumzia hisia za wananchi wakati wa kuagwa rasmi mwili wa kiongozi huyo, walisema kuwa kusema kweli, wananchi wa Zimbabwe wanapata shida na kuishi siku hadi siku 'kutoa nafasi kubwa kwa mtu ambaye alikuwa anapenda kujifikiria kuwa yeye ndiye mkombozi wao,' kuwa alishapoteza hadhi hiyo.

Wachunguzi hao wa habari walieleza kuwa hali ya kuzorota kwa uchumi bado inaendelea nchini humo, maji yakiwa hayatoki ila kwa nadra, umeme unapatikana kwa saa chache kila siku, bei za bidhaa muhimu kuanzia mikate hadi petroli ikiwa imevuka uwezo wa watu wa kawaida kumudu.

Walimhoji kinyozi mwenye umri wa miaka 45 anayeishi mtaa wa kawaida wa Harare na ambaye hakuhudhuria sherehe hiyo ya kuagwa, aliyesema kuwa hakuwa anampenda Mugabe 'lakini hataki kusema mabaya juu ya wafu.'

Alisisitiza wananchi wa Zimbabwe hawakupata chochote ila walifukarika zaidi.'Hakuwa kiongozi mzuri.'

Wakichambua hisia zilizokuwepo katika kuagwa mwili wa marehemu na maeneo mengine, walisema kuwa hata waliohudhuria sherehe ya kuagwa Mugabe walikuwa wana mawazo kibao kuhusu mahitaji yao ya kila siku, 'licha ya kuwa walikuwa wanailaumu serikali ya Mnangagwa na siyo mtangulizi wake.'

Yuko mwanamke mmoja aliyetajwa kwa jina la Fadzai Mutasa, mkazi wa Harare mwenye umri wa miaka 42 aliyesema kuwa wakati Mugabe anaondolewa, mikate ilikuwa inauzwa dola mbili (za Marekani) na chakula, usafiri watu walikuwa wanamudu.

Alipinga wazo (walilompa waandishi hao) kuwa alihudhuria kuagwa Mugabe kama kuelezea upinzani wake kwa Mnangagwa, akisema 'amekuja tu kutoa ushuhuda wa kazi nzuri za Mugabe.'

Wengi tayari wanamtofautisha Mugabe na waliochukua serikali mwaka 2017.

Alitaja alichosema ni tofauti kati ya Mugabe na utawala wa sasa, kuwa watu wakipata tabu Mugabe alikuwa anaelewa, 'lakini watawala wa sasa haielekei kuwa wanasikiliza kilio cha watu kama alivyokuwa akifanya.'

Yuko mwanamke mwingine aliyehojiwa, akamsifu Mugabe kwa kuinua haki za wanawake, akataja kuwa mkate sasa unanunuliwa dola 10 (za Marekani) na kuwa angekuwa Mugabe angekomesha hali hiyo, atoe amri ya kupunguzwa bei za bidhaa muhimu au vyakula.

Ni hisia zinazoonyesha mvutano kati ya wananchi kuhudhuria au kutohudhuria sherehe ya kuagwa Mugabe, kwani kilichowatatiza siyo tu yale Mugabe aliyotenda katika utawala wake, ila endapo pia wanataka kujiunga na utawala wa sasa katika adhimisho hilo, kuonyesha mshikamano na serikali ya Mnangagwa kuhusu Mugabe na serikali hiyo pia.

# Chadema: Upinzani kurejesha wabunge wengi

INATOKA UK.13

kitaifa, tutaendelea kutoa miongozo mbalimbali na kutafsiri kanuni pia za uchaguzi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na kanuni mbalimbali na miongozo. Ila kwa ngazi za chini, zitaendelea kutafsiri kuhakikisha kwamba tuna wagombea wa kupiga kampeni na kuhakikisha ushindi kwa wagombea. Kwahiyo tumegawa kazi katika makundi makuu mawili.

**SWALI: Sifa za wagombea wenu katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni zipi?**

**JIBU:** Sifa ni nyingi, zipo zimeainishwa kisheria na kikatiba lakini sifa moja kubwa kabisa ni kwamba awe mtu mwadilifu na anayekubalika katika jamii inayohusika, kwenye kijiji ama kitongoji alichopo. Na sifa za ndani ya chama ni kuwa awe mtu ambaye amekuwa active (hai) na ameshiriki katika shughuli za ujenzi wa chama, either (ama) kwa kuonekana au kwa kutokuonekana, ambaye yupo tayari kutetea wananchi, kupigania haki na kuhakikisha kwamba haruhusu udhalilishaji au ukandamizaji wa binadamu mahali popote.

**SWALI: Upinzani umesikika ukilalamikia kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa. Je mkakati wenu ni upi katika kukabiliana na kanuni hizo mnazozilalamikia?**



Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vicent Mashinji (wa pili kulia) akiwa na Mwenyekiti wa chama hicho Freeman Mbowe.

**JIBU:** Kimsingi ni kweli kuwa kanuni zilizopo si rafiki tu kwa vyama vya upinzani, hata kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). Na tukiweka kwenye mizania sawa ya sheria, maana yake tutakwenda wote sawa, kwamba hizi kanuni si rafiki katika kuhakikisha tunakuwa na uchaguzi huru na wa haki.

Na kimsingi, kwa chaguzi hizi za serikali za mitaa inakuwa ni ngumu zaidi kwa wananchi mahalia, kwa sababu saa nyingine zinaweza zikatumika hizi kanuni vibaya kuwazuia kupata viongozi wanaowafaa kwa kipindi hicho, kwa sababu ni uchaguzi ambao watu wanachaguana kwa kufahamiana na kujuana. Lakini inapokuwa imeingiliana sana inakuwa ni ngumu kufanya. Kanuni zinapokuwa zinawabana sana ni rahisi watu kuenguliwa na michezo ya rushwa na rafu zingine ni rahisi kufanyika kwa kanuni hizi zilizopo.

Kwa hiyo kimsingi tuta-base (tutajikita) sana kwenye moral support (uungwaji mkono kimaadili) na wananchi kuliko kanuni, kwa sababu si rafiki tu kwa vyama vya upinzani, hata kwa chama tawala, hata kwa wasimamizi wenyewe wa uchaguzi kanuni si rafiki sana.

**SWALI: Ni vipengele gani ambavyo vinabana sana katika kanuni hizo?**

**JIBU:** Aah kwa mfano unaposema kwamba mgombea lazima awe amedhaminiwa na ngazi ya chini kabisa ya chama, sasa vyama vina tafsiri mbalimbali ngazi ya chini kabisa ya Chadema, si ya CCM, si ya ACT, si ya NLD unaona. Sasa katika hizi tafsiri zinapoleta mkanganyiko inawezekana msimamizi msaidizi wa uchaguzi, akatumia tafsiri hii mbovu kuengua wagombea, unaona mpaka tukija kurecover (kubaini) kwamba huyu wamemuonea, inawezekana ikawa muda umepita na tumeshachelewa uchaguzi.

**SWALI: Tukiacha uchaguzi wa Serikali za mitaa, ni ipi mipango ya Chadema kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwakani?**

> Kwa hiyo, polisi na wenzao wa usalama wana jukumu la kuhakiksha kila raia yupo salama including (akiwemo) Tundu Lissu.

**JIBU:** Ni jana tu tumemaliza kuweka taratibu za namna gani tutafanya hizo document (nyaraka). Kwa hiyo si kitu cha ajabu sana, ilani tulishaanza kukusanya data na government plan (mpango wa serikali), sera tayari tunazo ambazo nadhani zimeshafika hata ofisini kwenu... lakini this time (wakati huu) ilani ambayo tutakuja nayo kwa Watanzania, lazima waelewe ni ilani ambayo inayokuja kujibu masuala ya muhimu ya kimaendeleo ya Taifa letu na ni ilani inayolenga kukuza uchumi na kuiwezesha sekta binafsi kukua.

**SWALI: Kwa sasa Chadema inajiamini kiasi gani kuingia kwenye uchaguzi, ikizingatiwa kwamba kuna idadi kubwa ya Wabunge na Madiwani wamehamia chama tawala?**

**JIBU:** Aah kila uchaguzi una matukio yake na chaguzi hazifanani. Uchaguzi wa mwaka 2010, lilikuwa ni tukio la aina yake na uchaguzi wa mwaka 2015, ni tukio la aina yake. Uchaguzi wa 2020, nalo litakuwa ni tukio la aina yake na huwezi ukategemea kuwa uchaguzi mmoja ufanane na mwingine, kwa sababu uchaguzi huwa ni kutatua tatizo lililopo mbele. Sasa, tatizo lililopo mbele ndio linalo define (tafsiri), mfumo wa uchaguzi uweje.

Kwa mfano kama sasa hivi tumekuwa na kiongozi ambaye ni populist (maarufu), anayejinasibu kwamba yeye anakubalika na anaweza kushinda, na ni kind of messiah (aina fulani ya masiya), Kwa hiyo nature ya approach (asili ya kushughulikia) yake ya uchaguzi ni tofauti na ambayo tulikuwa nayo na Jakaya Kikwete ambaye alikuwa anatoa demokrasia na uhuru wa watu kushindana. Kwa hiyo approach ya uchaguzi ujao, ni tofauti, si sawa na za nyuma.



Wanachama na wafuasi wa Chadema, wakiwa kwenye mkutano wa hadhara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**SWALI: Uchaguzi uliopita kulikuwa na changamoto mbalimbali katika ushirikiano wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (ukawa), ikiwemo baadhi ya majimbo na kata kusimama wagombea wawili kutoka vyama vya ukawa badala ya mmoja. Je safari hii, Chadema imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hii?**

**JIBU:** Sehemu yoyote panapokuwa na makubaliano, changamoto huwa hazikosekani na tunaamini kabisa katika sehemu ambapo kuna watu wengi, asilimia 25 ya watu wanaweza wasikubaliane na kila kitu wakati wote. Kwa hiyo, kimsingi ukiangalia ni kwamba nchi ni kubwa sana, watu ni wengi na wagombea wa nafasi mbalimbali ni wengi sana. Kwa hiyo kupata sehemu chache ambazo panakuwa na mtanziko huo, inakuwa si shida sana. Sehemu ambazo zilikuwa na conflict (mgongano), zilikuwa ni chini ya asilimia moja ya maeneo yote. Kwa hiyo, halikuwa tatizo kubwa, kitu ambacho ni cha kawaida.

Na yalitegemewa hasa kwa sehemu yenye watu wengi, palikuwa na maandalizi ya ghafla... kwa hiyo, hatutakiwi kuliona kama ni tatizo kubwa sana la kufanya kutuondoa kwenye mstari.

**SWALI: Kwa aina ya siasa za sasa hivi, Je unafikiri kuna mbunge yeyote wa upinzani atakayerejea bungeni?**

**JIBU:** Ni wabunge wengi tu watakaorejea bungeni kwa sababu ubabe unaoendelea na hizi hali za kutumia nguvu ni sehemu tu ya siasa. Kwa hiyo kwa wanasiasa wanajua kwamba siasa ina hizo element tatu za ushawishi, propaganda na ubabe. Kwa hiyo ni sehemu ya siasa na katika utaratibu wa kawaida wa siasa, ni rahisi kukabiliana na hali kama hiyo. Kikubwa tu ni kwamba mtu ajulikane kwa wananchi, na wananchi baada ya kuwa wamemjua na ajenda zake na nini anasimamia, watamchagua na watamsimamia.

Kwa hiyo wanaoweza kuwa wababe wazuri zaidi wanategemewa kuwa ni wananchi na si vyombo vya dola.

**SWALI: Tundu Lissu amekuwa akijinasibu kuwa akipewa nafasi na Chama ya kugombea ataweza kuipeperusha vyema bendera ya chama. Je hiyo ni dalili pia kuwa chama kimeanza kumfikiria Lissu katika suala la urais?**

**JIBU:** Kwa mfumo wetu wa kugombea, wanapewa nafasi watu walioomba. Kama tutakosa mtu aliyeomba, basi tutatafuta mtu ambaye hajaomba. Tuna mfumo wa kuomba kugombea nafasi katika serikali. Kuna mwongozo ambao upo ndani ya Katiba yetu, upo wazi kabisa... mtu anayetaka nafasi ya kugombea cheo cha kiserikali, anatakiwa aandike barua kwa katibu wa ngazi yake. Kwa hiyo, kwa urais anatakiwa aandike barua kwa Katibu Mkuu, akiambatanisha na vyeti vyake pamoja na wasifu wake. Baada ya hapo, Katibu Mkuu atachukua hayo majina na kuangalia kama huyo mtu anakidhi vigezo vya kikatiba na sheria za nchi.

Na kwa kupitia Sekretarieti ya chama, baada ya hapo atawasilisha hayo majina yote kwenye Kamati Kuu na kuelezea kwamba, ni wapi wamekidhi vigezo na wapi hawajakidhi vigezo. Baada ya hapo, Kamati Kuu itatoa idhini sasa hayo majina yatangazwe na kuanza kuyatafiti kwamba, ni jina lipi ambalo linastahili na linafaa kupewa hiyo fursa ya kugombea.

**SWALI: Ukweli ni upi kuhusu kurejea kwa Tundu Lissu, kwa kuwa alipanga kurejea na sasa ameahirisha na vipi kuhusu usalama wake?**

**JIBU:** Atarudi, na chombo pekee kinachoweza kuhakikisha usalama wake ni vyombo vya dola na sisi wengine tuna supplement (ongezea). Kwa hiyo, polisi na wenzao wa usalama wana jukumu la kuhakiksha kila raia yupo salama including (akiwemo) Tundu Lissu. Kwa hiyo sisi hatuna hofu ya usalama wa mtu yoyote kwa sababu ni wajibu wa mamlaka za serikali kuwalinda watu wake. Sisi tutakachokifanya ni ku- compliment (ongezea).

**SWALI: Uamuzi wa Jaji katika kesi ya ubunge ya Tundu Lissu, umeleta mjadala. Je wewe kama Katibu Mkuu wa chama, una lipi la kusema?**

**JIBU:** Aah kwa kesi ya Lissu, Jaji mwenyewe alieleza pale... sisi wengine hatuwezi kuwa na comment (maoni) nyingi. Jaji ameeleza kabisa kwamba hawezi kumpa Lissu haki yake kwa sababu anaogopa mihimili kugongana, Mahakama ooh na Bunge. Ukitafsiri maana yake na yeye mwenyewe alikiri kabisa kwamba Lissu atashinda hii kesi. Sasa kama ameshakiri Lissu atashinda hii kesi, amemnyima haki. Kwa hiyo kwa lugha rahisi tu, ni kwamba Mahakama hazipo huru.

**SWALI: Ni kwanini chama hakikuwasiliana na Spika wa Bunge kuhusiana na hali ya afya yake, kitu kilichopelekea Lissu kupoteza ubunge?**

**JIBU:** Sasa inategemea hiyo ni matter ya local stand (msimamo wa ndani) kwamba kwa nafasi yako unawasiliana naye kwa capacity (nafasi) ipi kwa sababu suala la Tundu Lissu kutokuwa bungeni linajulikana, wala si suala la kuanza kufanyia mikutano kwamba alikuwepo au hakuwepo. Yaani halibishaniwi, inajulikana kwamba yupo matibabuni na dhana tu ambazo zimefanywa ni hila, chuki ndio zinapelekea kufanya kitu kama hicho. Kuna watu wengi tu ambao hawapo bungeni, mfano mara ya mwisho umemsikia Nimrod Mkono lini? Yuko bungeni? Lakini hamna aliyemuongelea.

Kwa hiyo inaonyesha kabisa hizi ni siasa za chuki na figisufigisu zinazoendelea na hakuna chochote cha maana ambacho mtu anaweza akasimamia kwamba alikuwa hajui eti Lissu yupo wapi.

**SWALI: Pamekuwa na maazimio mbalimbali ya kupinga zuio la mikutano ya hadhara, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Je kama chama mnakwama wapi?**

**JIBU:** Haujawa wa kusuasua na sielewi tafsiri ya wengine ya kupinga ni nini. Lakini kwa upande wetu, tumeshapeleka kesi mahakamani, tukaondolewa mahakamani kwa technicalities(ufundi), na ambacho tulikuja kuamua ni kuwaandaa wananchi sasa kuja kufanya mikutano kwa nguvu. Kwa hiyo, lazima kuwe na maandalizi...hivyo bado tupo kwenye process (michakato) ya maandalizi.

> Kwa hiyo inaonyesha kabisa hizi ni siasa za chuki na figisufigisu zinazoendelea na hakuna chochote cha maana ambacho mtu anaweza akasimamia kwamba alikuwa hajui eti Lissu yupo wapi.

**SWALI: Mahakama ilishatoa uamuzi kuhusu suala la umbali wa mita 100 kutoka kwenye vituo vya kupigia kura, huoni kuwa hiyo pia itaathiri ushindi wenu?**

**JIBU:** Unajua ni concept (maoni) tu ya watu ambao wanataka kuwa frustrate (changanya) wenzao na kuwafanya wauogope uchaguzi. Lakini kimsingi katika uchaguzi ambao unaendeshwa vizuri, hakuna hata sababu ya watu kukaa pale na kulinda, kwa sababu ndani tayari kuna mawakala. Pia katika kuhakikisha kuwa kuna mifumo ambayo ni sahihi ya upigaji kura, hamna sababu ya watu kulinda kura. Kinachotakiwa kulindwa ni ushindi, ushindi ndio huwa unalindwa na si kura.

Na ushindi unaanzia toka umekiandaa chama kwenda kwenye uchaguzi, sasa kama watu umeshawaandaa kwenda kwenye uchaguzi, huhitaji kuwa na mita 100. Nitakupa mfano, unaweza ukaamua kuandaa timu yako ya ulinzi, kila baada ya watu tisa, wa kumi ni wa kwako, si tayari unalinda. So you don't need a hundred metres (huhitaji mita 100), unaweza ukawa upo palepale kwenye mstari kujipanga na lisiwape watu confusion (kuchanganyikiwa).

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**

## Mawakili walalamika kutoruhusiwa kumuona Waziri Ilunga huko DRC

MAWAKILI wa aliyekuwa waziri wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Oly Ilunga, wamelalamikia hatua ya kutoruhusiwa kukutana na mteja wao

Ilunga alikamatwa Jumamosi iliyopita na kuwekwa rumande akituhumiwa kujaribu kutoroka kwenda nje ya nchi wakati uchunguzi ukiendelea dhidi yake, kuhusiana na matumizi mabaya ya dola milioni 4.4 za kupambana na ugonjwa wa Ebola Mashariki mwa DRC.

Polisi walizuia mawakili hao kukutana na mteja wao, kwa kile walichoeleza kuwa ni amri ya viongozi wa Mahakama. Hatua hiyo ililalamikiwa na Guy Kabeya, kiongozi wa jopo la mawakili wa Ilunga akisema waliambiwa na polisi kwamba hawana haki ya kukutana na mteja wao.

Kibeya amesema alipotaka maelezo zaidi, Ofisa mwingine wa polisi alimwambia kwamba mawakili wamepigwa marufuku kukutana na Ilunga.

Hata hivyo, taarifa ya polisi imeeleza kwamba baada ya kuhojiwa na mwendesha mashtaka, Ilunga alipigwa marufuku kutosafiri kwenda nje ya nchi.

Lakini Polisi wamesema kwa wiki kadhaa sasa, hawakufahamu mahali alipokuwa akiishi, na walimkamata akijaribu kwenda jimbo la Kongo-Central ili kuvuka mpaka wa Congo-Brazzaville.

Taarifa hiyo imetupiliwa mbali na mawakili wa Ilunga ambao wamesema kwamba mteja wao alikamatwa akiwa nyumbani kwake.

Ilunga ambaye alikuwa waziri wa afya, amehojiwa na mwendesha mashtaka kuhusu matumizi ya dola milioni 4.4 za serikali zilizotolewa kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa Ebola.



Aliyekuwa Waziri wa Afya DRC, Oly Ilunga. **PICHA: MTANDAO**

Waziri huyo wa zamani anatuhumiwa kutumia vibaya fedha hizo, huku msaidizi wake na dereva wake pia wakiwa bado wanashikiliwa na polisi kutoka mwishoni mwa mwezi wa Agosti kwa sababu za uchunguzi.

Toka kujiuzulu kwake mwezi Julai, Ilunga alieleza kwamba amepata vitisho na shinikizo kutoka kwa watu ambao hakuwataja.

Familia yake inaeleza kwamba ameandamwa kutokana na hatua yake ya kujiunga na rais mstaafu Joseph Kabila mwishoni mwa mwaka 2016.

Ilunga ambaye alikuwa Daktari binafsi wa Etienne Tshisekedi, baba wa Rais wa sasa Felix Tshisekedi, alikihama chama chake cha UDPS na kujiunga na serikali ya rais wa wakati huo Kabila.

Alipochaguliwa kuwa Rais, Felix Tshisekedi hakuwa na uhusiano mzuri na Waziri wake wa afya wakati ambapo ugonjwa wa Ebola umeenea katika majimbo ya Kivu ya Kasazini na Ituri, hali ambayo iliathiri juhudi za kupambana na ugonjwa huo.

Polisi inasema Ilunga atafikishwa mbele ya Mahakama Kuu ya Taifa, ambako kesi yake itafunguliwa. **DW**

# Rais Magufuli na mapambano ya ukombozi wa pili kiuchumi



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akizindua mradi mkubwa wa maji vijijini uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 28 katika wilaya saba za Mkoa wa Tabora. **PICHA: MTANDAO**

**Na Reubeni Lumbagala**

DESEMBA 9, 1961, Tanzania ilipata uhuru wake kutoka katika mikono ya wakoloni.

Huu ulikuwa ni ukombozi wa kwanza wa kisiasa ambao ulileta furaha na matumaini mapya kwa Watanganyika walioishi kwa miaka mingi katika utumwa na manyanyaso ya wakoloni.

Baada ya Tanzania kujitoa katika minyororo ya ukoloni na kupata ukombozi wa kwanza, jitihada za kuleta ukombozi wa kiuchumi (ukombozi wa pili) zilichukua nafasi yake.

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemedari wa vita vya uchumi Rais John Magufuli imepania kwa vitendo kuhakikisha mapambano ya ukombozi wa pili wa kiuchumi yanafanikiwa, kwani ndiyo malengo na dira ya nchi katika kuleta ustawi na ukuaji wa maendeleo ya kweli.

**DIRA YA MAENDELEO YA UCHUMI WA VIWANDA**

Rais Magufuli amesimama imara katika kuhakikisha dira ya maendeleo ya nchi yetu ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 inafanikiwa.

> Mwelekeo wa kuifikisha Tanzania katika nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati unaenda vizuri, na hakika tutafika kama nchi.

Ndiyo maana serikali ikaweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi kuwekeza nchini kwa kujenga na kuendeleza viwanda vikubwa, vya kati na vidogo ili kufikia dira hii.

Ujenzi wa viwanda zaidi ya 3000 kote nchini umefanyika ambapo vijana wengi wamepata ajira za kudumu na za muda, hali iliyoboresha maisha yao.

Wakulima na wafugaji wadogo na wakubwa wameweza kupata masoko kwa ajili ya kuuza mazao yao ambayo hutumika kama malighafi za kulisha viwanda hivyo. Hii imesaidia kukuza sekta ya kilimo na mifugo kwa kiwango kikubwa.

Pia, serikali imeweza kukusanya kodi kupitia viwanda hivi, hali inayochagiza ongezeko la mapato ya nchi na hivyo mapato hayo kutumika katika ukuzaji wa sekta zingine kama elimu, nishati, afya, maji, miundombinu, mawasiliano, kilimo nk.

Mwelekeo wa kuifikisha Tanzania katika nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati unaenda vizuri, na hakika tutafika kama nchi.

**UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI**

Ukombozi wa pili wa kiuchumi unakwenda sambamba na ujenzi na uboreshaji wa miundo mbinu ya barabara, reli, madaraja na vivuko.

Kumekuwa na kasi kubwa ya ujenzi wa miundombinu hii kote nchini ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Wakulima, wafanyabiashara na wajasiriamali wamewekewa mazingira rafiki kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na bidhaa zao ili kupunguza gharama kubwa za usafirishaji.

Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) na Wakala wa Barabara za vijijini (Tarura) wanafanya kazi kubwa katika usimamizi wa ujenzi na uboreshaji wa barabara.

Aidha, ujenzi wa reli ya mwendokasi (SGR) unaendelea ambapo wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro wataweza kusafiri kwa urahisi na kuokoa muda wa safari muda si mrefu ujao.

Pia, reli katika mikoa ya Tanga hadi Kilimanjaro imekamilika ambapo wafanyabiashara wanaweza kusafirisha bidhaa zao kwa bei nafuu.

Ujenzi wa meli katika mikoa ya kanda ya ziwa na maeneo mengine ya nchi yetu unaendelea ili kuwarahisishia wananchi usafiri huo.

Usafiri wa anga nao umeboreshwa kwa kiwango kikubwa, ambapo serikali imeboresha na kujenga viwanja vingi vya ndege katika mikoa mbalimbali.

Aidha, serikali imenunua ndege kwa ajili ya kuwahudumia abiria wa ndani na wa nje ya nchi katika safari zao za kikazi, kibiashara, kiutalii na za kimapumziko.

Mapato yanayopatikana katika usafiri wa anga yanachangia ukuaji wa uchumi na hatimaye kuchagiza ukombozi wa pili.

**MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE**

Kutokana na ongezeko la mahitaji ya nishati ya umeme katika kuendesha shughuli mbalimbali za kijamii na za kiuchumi, Rais Magufuli aliamua kutimiza ndoto za Mwalimu Nyerere za kujenga Bwawa kubwa kwa ajili ya kufua umeme wa maji katika Mto Rufiji.

Mradi huu utagharimu dola za Marekani bilioni 2.9 sawa na Sh. trilioni 6.5 za Kitanzania na kufanikisha uzalishaji wa Megawati 2115.

Megawati 2115 ni kiasi kikubwa kuliko kinachotumika sasa kwa nchi nzima.

Umeme huu utamaliza kabisa mahitaji ya nishati ya umeme. Kama hiyo haitoshi, kukamilika kwa mradi huu kutaiwezesha Tanzania kuuza umeme kwa Watanzania kwa bei nafuu na kuziuzia nchi nyingine.

Hivyo basi, mradi huu ni utekelezaji wa dira ya maendeleo ya kuhakikisha shughuli za kiuchumi hasa za viwandani na huduma nyingine za kijamii kama afya na elimu zinapata nishati ya umeme ili kuongeza uzalishaji.

**KUONGEZA MAKUSANYO NA MATUMIZI BORA YA MAPATO**

Ili kufikia maendeleo na ukombozi wa kiuchumi, ni lazima kodi ikusanywe kutoka kwa wananchi.

Tangu serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya kodi kutoka Sh. bilioni 800 hadi trilioni 1.43.

Mafanikio haya yametokana na nia njema ya Rais Magufuli katika kuhakikisha kodi inakusanywa na kutumika katika uwekezaji wa miradi mikubwa na midogo ya maendeleo kwa ajili ya ustawi wa wananchi na nchi kwa ujumla wake.

Kutokana na mafanikio ya makusanyo ya kodi, serikali imeongeza uwezo wake wa utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo.

Ukombozi wa pili wa kiuchumi ndiyo agenda ambayo wananchi wanaitaka kuisikia na kuona serikali yao ikiisimamia kwa vitendo kwani ni katika ukombozi huu ndipo yalipo maendeleo ya kweli ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja. Tafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764 666349***

# Mzee Mugabe; Mpigania uhuru aliyekumbukwa kabla hajafa

**Na Mashaka Mgeta**

HABARI zake bado zinaendelea kuandikwa, historia yake inaelezewa kabla ya mwili wake kuzikwa katika siku ambayo haijatangazwa rasmi.

Mpigania uhuru wa Afrika aliyeiongoza Zimbabwe tangu mwaka 1987 hadi 2017, Robert Gabriel Mugabe, alifariki dunia Septemba 6, mwaka huu kwenye Hospitali ya Gleneagles nchini Singapore, alikokuwa akitibiwa.

Mugabe amefariki akiwa na miaka 95 huku akikumbukwa kwa ujasiri wake dhidi ya ukoloni kutokana na misimamo yake nchini Zimbabwe.

Wanaofuatilia na 'kuziishi' fikra za ki-Magharibi, wanamuona Mugabe kama kiongozi mwenye hulka ya udikteta, kwa namna alivyoitawala nchi hiyo kwa takribani miaka 37.

Lakini barani Afrika na hasa wanaojua na kuifuatilia historia ya ukombozi uliojikita katika kudai uhuru, haki, usawa na hadhi ya 'mtu, Mugabe anaangaziwa kama jemedari wa vita aliyevishinda vikosi vyenye silaha kubwa na nguvu za kijeshi, akabaki kuwa mshindi.

Kwa sababu ya wigo mpana wa mawasiliano, mikakati ya kueneza propaganda, japo kutaja kwa uchache, sifa hasi dhidi ya Mugabe zilienea kwa kasi na hivyo kuyafanya mambo mema aliyolitendea taifa lake na raia wa Zimbabwe kutojulikana.

### KUTETEA UHURU WA ZIMBABWE

Mugabe aliuamini na kuutetea uhuru wa Zimbabwe uliopatikana 18 Aprili 1980, na mara kadhaa alipenda kuweka bayana kwamba uhuru huo na ule wa raia wake ni mambo yanayopaswa kuheshimiwa daima.

Aliyasema hayo wakati akijibu mashambulizi ya propaganda zilizoenezwa na mahasimu wake wa kisiasa na utawala, hasa nchi za Magharibi.

Mugabe alisimamia msingi wa kuzirejesha rasilimali za raia wa Zimbabwe na hasa ardhi kuwa milki ya Wazimbabwe, akisisitiza kwamba si raia wa nchi hiyo tu, bali hakuna mwafrika aliyewahi kwenda kudai na kumiliki ardhi kwa nguvu kwenye mataifa hayo (Magharibi) kama wanavyofanya baadhi ya raia wao kwa Afrika.

Moja ya kauli yake iliyowahi kuzua mjadala mkubwa ni pale alipowahi kutamka, "Sisi sio watu wa Ulaya, hatujawahi kuomba hata sehemu ndogo ya Ulaya, Blair, kaa na Uingereza yako na mimi niache nibaki na Zimbabwe yangu."

Tony Blair alikuwa Waziri Mkuu wa Uingereza kuanzia mwaka 1997 to 2007. Pia Blair alikuwa kiongozi wa chama cha Labour kuanzia 1994 hadi 2007. Aliwahi kuwa kiongozi wa upinzani kuanzia 1994 mpaka 1997 na kati ya 1983 na 2007, Blair alikuwa mbunge wa jimbo la Sedgefield.

Historia inamuangazia Mugabe hasa yanapotajwa masuala ya ardhi yaliyosababisha kuporomoka kwa uhusiano kati yake na wakulima wakubwa wa kizungu.



Waombolezaji wakiwa na bango lenye picha ya Robert Mugabe siku ya kuaga mwili wake jijini Harare nchini Zimbabwe. **PICHA: MTANDAO**

> "Kwa upande mwingine, yapo mafanikio kadhaa aliyoyafikia Mugabe katika kipindi cha utawala wake.

Wakati wa mzozo wa ardhi uliosababisha ghasia nchini humo, Mugabe aliwahi kutamka, "Hii ni ardhi ya mtu mweusi, hivyo ni mtu mweusi ndio ana haki ya kuamua nani akae na nani asikae. Tuna ardhi yetu na katika ardhi yetu ndio tutapata fedha."

Kwa upande mwingine, yapo mafanikio kadhaa aliyoyafikia Mugabe katika kipindi cha utawala wake.

Miongoni mwa sekta zilizoboreka, kukua na kuwa mfano bora kwa kiongozi huyo alipokuwapo madarakani ni afya na elimu kwa weusi walio wengi dhidi ya wazungu wachache waliokuwa wanufaika wakubwa baada ya uhuru.

### KUMINYA UPINZANI

Licha ya mafanikio yake katika maendeleo ya nchi na ustawi wa raia wa Zimbabwe, Mugabe alikosolewa kwa namna alivyowadhibiti wapinzani na shughuli zao za kisiasa, akitumia zaidi majeshi ya taifa hilo lililopo Kusini mwa Afrika.

Majeshi hayo yalionekana tena katika utekelezaji wa kunyakuwa ardhi kutoka kwa wakulima wachache wa kizungu, hatua iliyomfanya kuzidi kuungwa mkono na wapigakura wa nchi hiyo huku akichukiwa na washirika wa maendeleo kimataifa.

### SAFARI YA KUONDOKA MADARAKANI

Dalili za Mugabe kuelewa na 'mzigo' wa urais zilianza kuonekana baada ya kuibuka kwa mzozo kati yake na aliyekuwa Makamu wa Rais, Emmerson Mnangagwa ambaye kwa sasa ndiye Rais wa nchi hiyo.

Ingawa mzozo huo ulikua kiasi cha kusababisha Mugabe 'kuwekwa kizuizini' na baadaye kuondolewa madarakani, wahusika wa mpango huo wakitajwa kuwa washirika wa Mnangagwa, Rais huyo wa sasa wa Zimbabwe akafunguka kusifu na kupongeza utawala wa Mugabe, baada ya habari za kifo chake kuenea kuanzia nchini humo hadi pande zote za dunia.

Kwa Mnangagwa, hadi kuwa shujaa wa taifa kama alivyokabidhiwa na chama chake cha Zanu -PF, ilimstahili Mugabe.

### KUKUMBUKWA KWAKE

Ingawa Mugabe anatajwa kwa mema mengi baada ya kufariki dunia, lakini zipo taarifa kuwa raia wa Zimbabwe walianza kumtaja kwa utawala wenye mafanikio, siku kadhaa baada ya kuondolewa madarakani, yaani kabla ya kifo chake.

Raia kadhaa wa Zimbabwe walikaririwa wakisema licha ya ugumu wa maisha waliyokuwa nayo wakati wa utawala wa Mugabe, lakini uongozi wa Mnangagwa ulisababisha hali kuwa ngumu zaidi.

Miongoni mwa wananchi waliokaririwa wakilalamikia ugumu wa maisha baada ya Mugabe kuondolewa madarakani ni pamoja na Fadzayi Mahere wa chama kikuu cha upinzani cha Movement for Democratic Change (MDC).

Chama cha MDC kikiongozwa na Morgan Tsvangirai aliyefariki Februari 14, mwaka jana huko Johannesburg, Afrika Kusini kiligawana mamlaka ya utawala na Mugabe baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2008, ulioghubikwa na vurugu na madai ya wizi wa kura uliofanywa na watawala.

Ili kurejesha hali ya utulivu na amani nchini humo, iliundwa serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyosababisha kuwapo mgawanyo wa madaraka, Tsvangerai wa MDC akawa Waziri Mkuu.

Ni kutokana na hali ngumu ya maisha, upinzani nchini humo ukikihusisha chama cha MDC, kikatoa rai kwa Wazimbabwe kuandamana, ikiwa ni ishara ya kupinga hali ngumu ya maisha kiuchumi.

Hali hiyo ilijitokeza baada ya Mugabe kundolewa madarakani 2017 na taifa hilo kuwa chini ya uongozi wa Mnangagwa.

Kigezo kikubwa kilichotumiwa kutathmini hali ya maisha ya watu ni viashiria vya uchumi vilivyoyagusa maisha ya raia wa Zimbabwe, miongoni mwao vikiwa ni ufinyu wa ajira, kushuka kwa kipato ikiwamo mishahara na kudorora kwa biashara.

### HISTORIA FUPI

Mwaka 1980, Mugabe alishinda uchaguzi na kuwa Waziri Mkuu.

Mwaka 1982 aliushutumu upinzani kwa kupanga njama za kutaka kuipindua serikali yake.

Mwaka 1987, utawala wa Mugabe ulibadilisha Katiba ili imruhusu kuwa Rais na kuongeza mamlaka yake.

# Mahakama Uingereza zasutana majaji kuzuia Brexit Oktoba 31




Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

SIASA nchini Uingereza inaanza kuwa kichekesho kutokana na Bunge na washikadau tofauti kupania kuzuia Uingereza kuondoka katika uanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) mwishoni mwa mwezi ujao bila mkataba.

Wanamlaumu Waziri Mkuu Boris Johnson kwa hali hiyo kuwa bayana kutokana na utayari wake kusimamia Uingereza kuondoka umoja huo siku hiyo ikifika, kama ambavyo EU pia umeeleza bayana kuwa hakuna majadiliano ya kina kuhusu vipengele vya kujitoa, nje ya kile kilichoafikiwa na aliyekuwa waziri mkuu, Theresa May.

Bunge la Uingereza linaamini linaweza kuendelea kuchelewesha kujitoa hadi mkataba ufikiwe.

Ili kufanikisha mkakati wa kujitoa bila mkataba na kupunguza usumbufu bungeni wakati serikali inajipanga kwa hatma hiyo kibajeti na mahusiano mengine ya kiuchumi kimataifa, Johnson alifikia uamuzi wa kuahirisha shughuli za Bunge kwa wiki tano, hadi katikati ya mwezi Oktoba.

Ni hatua ambayo iliwagawa wabunge wa chama tawala cha Conservative na mawaziri wawili wakajiuzulu akiwamo mdogo wa kuzaliwa wa Johnson, akisema mvutano wa utii kifamilia na kuzozana kisiasa umemzidi nguvu, abwage manyanga.

Johnson aliomba na kupata idhini ya Malkia Elisabeth II kuhusu hatua hiyo, halafu wapinzani wakacharuka kuwa 'alimdanganya.' Upinzani huo kuhusu kuahirishwa shughuli za Bunge wakati kujitoa bila mkataba kunaiva punde, ukaleta sura nyingine, ambako ubishi katika siasa ukahamia mahakamani.

> Alifikia uamuzi huo kwani kanuni hazimruhusu kumkoromea Waziri Mkuu Johnson kuhusu sera ya kusimamia kujitoa bila mkataba na anajua suala hilo linamgusa mno hisia zake hawezi kubaki kitini huku linapita tu.

Kwanza wabunge (Commons) wakapitisha sheria (muswada) kuzuia kuondoka kwa Uingereza bila mkataba EU, kana kwamba ni uamuzi wa waziri mkuu peke yake.

Wanachotaka ni yeye aombe muda zaidi wa kujiandaa kujitoa kwa kupata mkataba, licha ya mikataba takriban mitatu na mifumo mingine ya kujitoa iliyowahi kufikishwa mbele ya Bunge kupigiwa kura kukwama.

Ndiyo hapo 'hesabu' za upinzani zinachanganya; Johnson hataomba muda wa nyongeza na huu uliopo unaisha Oktoba 31.

Siyo rahisi kuona jinsi Bunge linavyoweza kutimiza azma hiyo ya kuzuia kujitoa bila mkataba, kwani kinachotakiwa ni kupitisha sheria (yaani azimio la Bunge) kuwa Uingereza sasa inasitisha mchakato wa kujitoa, ipuuze matokeo ya kura ya maoni kitaifa mwaka 2016.

Hali hiyo haijawahi kufikiwa hata wakati wa kujadili mikataba aliyofikia May awali, na iliposhindikana kukubaliana akapewa na EU muda wa nyongeza, halafu ikabidi aombe tena mwezi mmoja, ila akapewa sita.

Ndiyo hiyo inakatika Oktoba 31 na Bunge liko katika azma ya kujitoa, ila linalazimisha iwe ni kwa mkataba, wakati imeshindwa kuafiki kila mkataba ulioletwa mbele yake tangu Machi 2019.

Cha kushangaza ni jinsi mvutano huo ndani ya Bunge ulivyosambaa na kuanza kuathiri hisia za vyombo muhimu vya dola nchini humo, kuanzia Baraza Shauri la Bunge (House of Lords) ambalo lilipiga kura kukazia 'sheria' ya kutokujitoa bila mkataba.

Ni sheria ya upande wa Uingereza ambayo haiungwi mkono na serikali ya nchi hiyo na pia haitambuliwi na EU.

Hivyo haiibani Tume ya Ulaya kuendelea kuitambua Uingereza kuwa ni mwanachama ifikapo saa sita usiku Oktoba 31.

Ikiishia kuwa sheria, hiyo haitazuia Uingereza kuondoka EU licha ya kuwa Bunge lilikataa pia pendekezo la Johnson la kufanya uchaguzi mkuu wa haraka Oktoba 15 ili kuamua 'ni nani atahudhuria kikao muhimu EU Oktoba 17 kama waziri mkuu wa Uingereza.

Kukataa pendekezo la kufanyika uchaguzi mkuu kunatokana na uhalisia kuwa upinzani unajua kujitoa EU hata bila mkataba ni 'dili' katika hisia za makundi ya sera za kizalendo, au tuseme za ki-Trump.

Ni makundi tofauti yanayopinga, ikiwa ni pamoja na wenye viwanda na hata bidhaa nyingi za kilimo ambao soko lao kuu ni barani Ulaya, wanahofia ongezeko kubwa la ushuru wa forodha.

Pia kuna aina tofauti za vyakula vinaagizwa kutoka barani humo, na aliyekuwa waziri mkuu wa mwisho kutoka upinzani, yaani Labor, Gordon Brown, 'akatishia nyau,' akadai kujitoa bila mkataba kutaleta uhaba mkubwa wa chakula, kana kwamba Uingereza inawekewa vikwazo.

Cha kushangaza ni jinsi vyombo kadhaa vya juu vya sheria vilivyojitosa katika sakata hilo, kuanzia na House of Lords ilipopiga kura kukazia uamuzi wa House of Commons wa kutojitoa bila mkataba, huku wanajua kuwa uamuzi huo hauko mikononi mwa waziri mkuu.

Wanasisitiza alete mapendekezo ya mkataba wakati eneo moja tu ambalo Johnson angalau anajitahidi kupata muafaka ni suala la kuendelea kuwapo 'mpaka laini' kati ya Ireland ya Kaskazini (jimbo tengefu la Uingereza) na Jamhuri ya Ireland.

Ni ndugu zao wa dhehebu tofauti na hao wa Kaskazini, ila mpaka huo ukiwa mgumu kuvuka itarudisha chokochoko za kujitenga kikamilifu, ugaidi urudi.

Baada ya Lords kupitisha 'sheria mkazo' kutojitoa EU bila mkataba, wapinzani wakapeleka kesi Mahakama Kuu ya Scotland, jimbo lingine tengefu la Uingereza, ambako chama chake cha siasa kiko karibu na Labor kupinga mkakati wa Brexit kwa jumla, na siyo tu kujitoa bila mkataba.

Kama ilivyotazamiwa kesi hiyo ilishinda na ikatolewa rai ya kisheria kuwa kuahirishwa kwa shughuli zote za Bunge kwa wiki tano ilikuwa kinyume cha sheria.

Sasa wachunguzi wa habari wakaanza kujiuliza, kama waziri mkuu Johnson anaweza kuchukua hatua ambayo anajua ana mamlaka nayo, halafu akaomba kibali kwa suala hilo kwa Malkia, wote wawili wasiijue sheria?

Ili kukoleza sukari katika mkanganyiko huo wa Mahakama, kesi tofauti ikafunguliwa Ireland ya Kaskazini, kuhusu suala hilo, wakijua kuwa hisia jimboni humo kuhusu Brexit ni tofauti na Scotland, kwani wanajali zaidi suala la mpaka, na yaliyobaki si hoja muhimu kwao.

Kesi hiyo iliundwa ili kutokutegemea tu rufani ya uamuzi wa Mahakama Kuu ya Scotland kuhusu hali ya Bunge kutokuwa na vikao, ambayo serikali ya Johnson imepeleka Mahakama ya Juu zaidi nchini humo, Supreme Court.

Mahakama Kuu ya Ireland ya Kaskazini ilikanusha maamuzi ya hiyo Mahakama Kuu ya Scotland, na 'kulainisha koo' kwa mjadala wa suala hilo 'Supreme Court.'

Kulikuwa na kimalizio cha aina yake katika mjadala huo, jinsi ulivyopita bungeni na pia jinsi unavyoonekana kukwama mbele ya safari, pale Spika wa Bunge (Commons) John Bercow akitangaza kujiuzulu (labda tuseme ni kustaafu mapema).

Alifikia uamuzi huo kwani kanuni hazimruhusu kumkoromea Waziri Mkuu Johnson kuhusu sera ya kusimamia kujitoa bila mkataba na anajua suala hilo linamgusa mno hisia zake hawezi kubaki kitini huku linapita tu.

Hatua yake inafanana na ile ya aliyekuwa waziri mkuu, Theresa May kuwa aliahidi kuifikisha Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya kwa mkataba. Hakuweza kusimamia kujitoa bila mkataba.

Kinachoonekana ni kuwa sarakasi hizo za kisheria hazitabadilisha lolote kwani uamuzi wa kuahirisha kwa muda unaostahili au unaofaa shughuli za Bunge si jambo la ajabu Uingereza licha ya kuwa wengi walishtuka.

Halafu ni wazi kujitoa bila mkataba kunahitaji Bunge la Uingereza (Commons) liridhie mkataba wa May na siyo litafute mwingine ndani ya wiki sita au pungufu, jambo ambalo limeshindikana.

Suala la kuendelea kuomba muda halipo mezani EU na Johnson hana mpango huo, sasa sheria gani itazuia Uingereza isitoke bila mkataba Oktoba 31?





# Familia kadhaa zanusurika kifo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

FAMILIA tisa zimenusurika kifo jijini Mbeya baada ya moto ambao chanzo chake hakikujulikana kuteketeza makazi yao.

Nyumba pamoja na mali ziliungua kabla ya zimamoto na wananchi kushirikiana kuudhibiti moto huo.

Tukio hilo lilitokea juzi jioni katika Mtaa wa Isanga jijini Mbeya ambako baadhi ya familia zilikuwa zimezingirwa na moto huo na kuanza kukimbia hovyo.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa wapangaji wa nyumba hiyo, Firimina Ibrahim, alisema kuwa akiwa ndani na wenzake walianza kuona moshi mzito ukiingia ndani ya chumba chao lakini hawakujua unatokea wapi.

Alisema kuwa baadaye walisikia kelele za moto ndipo walipotoka nje na kushuhudia nyumba hiyo ikiteketea kwa kasi.

"Tulipotoka nje tukaona moto mkubwa ukiwaka juu ya nyumba yetu ulituogopesha hata kurudi ndani kuokoa baadhi ya vitu, hivyo tukaanza kukimbia kunusuru maisha yetu," alisema Firimina. Mmiliki wa nyumba hiyo, Joseph Mpanji, alisema kuwa moto huo umesababisha hasara kubwa kwake yeye mwenyewe na wapangaji wake kwa vile mali nyingi ziliteketea.

"Katika nyumba hiyo upande wa uwani ninao wapangaji saba na huku nyumba kubwa nina mpangaji mmoja, mali zote za wapangaji wa uwani zimeteketea. Tumeokoa gari lililokuwa limeegeshwa jirani na nyumba," alisema Mpanji

Alisema chanzo cha moto hakijafahika kwa vile mita ya umeme inayotumika katika nyumba nzima ni moja na ipo mahali anapoishi yeye na imebaki salama.

Ofisa Habari Msaidizi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Ester Kinyaga, alisema kuwa walipata taarifa za moto kupitia simu ya dharura ya 114 baada ya kupigiwa na wananchi.

Alisema walifanikiwa kuudhibiti moto na hakuna madhara yoyote kwa binadamu isipokuwa mali nyingi ndani ya nyumba zimeteketea.

Kinyaga alitoa wito kwa wananchi wanapoona matukio ya moto, ajali au hata janga lolote kwenye jamii kutoa taarifa mara moja kwenye Jeshi hilo ili wapate msaada badala ya kuanza kujiokoa wenyewe kwa vile wakati mwingine hawana mbinu wala ujuzi huo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila akizungumza na wananchi wa Kata ya Maendeleo, jijini Mbeya jana, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kutembelea kata za Jiji hilo na kusikiliza kero za wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# HESLB lawamani kuangamiza vipaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imelaumiwa kuua vipaji vya vijana nchini kutokana na utaratibu wa kuweka vipaumbele kwa baadhi ya kozi zinazopewa mikopo huku nyingine zikiachwa.

Hali hiyo inawalazimisha wanafunzi kusoma kozi hizo na kuachana na ndoto zao ili wapate mikopo.

Hayo yaliibuliwa juzi jijini Mbeya na Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vikuu yanayotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuwasaidia kujiajiri.

Chalamila alisema kitendo cha bodi kuweka utaratibu wa vipaumbele hivyo unasababisha wanafunzi kuacha kusoma kozi ambazo zinaendana na ndoto zao na kujilazimisha kusoma zile zenye mikopo hivyo vipaji vyao kufa.

Alisema ni vyema bodi hiyo ingetoa mikopo kulingana na ufaulu wa mwanafunzi bila kujali kozi anayosomea badala ya utaratibu huo mpya wa kutoa kuweka vipaumbele kwa kozi.

"Wanachokifanya sasa ni kuwahamisha kutoka kwenye kile wanachokipenda kwenda kwenye wasichokipenda kwa sababu kipo kwenye kipaumbele cha mikopo.

"Hapo tunaua kipaji ambavyo vijana walikuwa wanavitaka tangu walipokuwa wadogo," alisema Chalamila.

Hata hivyo, alikipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuanzisha mafunzo hayo ambayo alidai yatawasaidia vijana hao kuanzisha miradi yao badala ya kusubiri kuajiriwa serikalini au kwenye sekta binafsi.

Mwakilishi wa wakufunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Issack Allan, alisema vijana wengi ambao wamehitimu elimu ya juu wapo mitaani wakiwa hawajui cha kufanya huku wakiilaumu serikali kwa kutotoa fursa za ajira.

Alisema hali hiyo inaichelewesha Tanzania kuingia katika nchi zenye uchumi wa kati na kwamba baadhi yao wamejaribu kuanzisha biashara lakini zinashindwa kuendelea kutokana na vijana hao kukosa maarifa.

Alisema baada ya chuo hicho kubaini hali hiyo ndiyo maana kinatoa mafunzo hayo ambayo yameanzishwa kupitia kitengo chake cha ubunifu na ujasiriamali ili kuwasaidia vijana hao kujiajiri badala ya kuendelea kulalamika.

"Vijana wengi wanashindwa kubadili changamoto zao kwenye jamii kuwa fursa ndiyo maana tunatoa mafunzo haya. Tunawapa mambo ya ujasiriamali na uanzishaji wa biashara," alisema Dk. Allan.

Aliwaeleza kuwa chuo hicho kinatoa mafunzo hayo kwa kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya ndani na kwamba mafunzo hayo yatafanyika kwa muda wa siku tisa.

Alisema mafunzo hayo kwa mwaka huu yanafanyika katika mikoa 10 ambayo nane ni ya Tanzania Bara na miwili ni ya Zanzibar.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Iringa, Lindi na Katavi, Unguja Kusini na Pemba Kasikazini kwa Zanzibar.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vincent Msolla, alisema serikali imeandaa mazingira bora kwa vijana wenye ujuzi na nia ya kuwa wajasiriamali ikiwamo kuwapatia mikopo kupitia asilimia 10 ya mapato ya halmashauri inayotolewa kwa vikundi vya wajasiriamali vya vijana, kinamama na wenye ulemavu.

# Vijana wafundwa mbinu za utafutaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA 36 kutoka kata za Mabatini na Sinde jijini Mbeya wamefunzwa mbinu za ujasiriamali na mafunzo ya fani nyingine mbalimbali ikiwamo teknolojia.

Walionufaika ni wale wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 25 ambao pamoja na ujasiriamali wamefundishwa uongozi, Tehama, huduma za hotelini ili kuwasaidia kupata ajira na kujiajiri.

Mafunzo hayo yanaratibiwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Catholic Relief Service (CRS) chini ya Mradi wa Youthbuild ambao ulianzishwa April 16 mwaka 2018.

Akizungumza juzi wakati wa mahafali ya kuhitimu mafunzo ya fani mbalimbali kwa vijana 36 kutoka kata za Mabatini na Sinde jijini Mbeya Meneja Mradi wa Youthbuild Marilyn Chottah, alisema umelenga kuwajengea uwezo.

Uwezo huo unawasaidia kuzitambua fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo zitawasaidia kujikimu na kujimudu kimaisha.

Chottah alisema wakati mradi unaanzishwa ulisajili vijana 158 wenye umri kati ya miaka 18 hadi 25 kutoka kata ya Mabatini na kuchagua vijana 60 kwa ajili ya hatua za awali za mpango huo.

Alisema katika mchakato huo waliendelea kuwachuja kwa kupitia mashindano na mafunzo kadhaa ili kuwapata wenye sifa stahiki.


Alisema miongoni mwa vigezo walivyovitumia kupima uwezo wa vijana kujitoa kushiriki katika program ya Youthbuild ni kuanzisha biashara yenye mtaji usiozidi Sh. 2,000 kwa siku.

"Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, anayeshughulikia mipango Conrad Millinga, aliwasisitiza vijana kutumia vyema ujuzi walioupata kwa kuanzisha shughuli za miradi ya maendeleo katika jamii.

Alisema ujuzi walioupata uwe dira kwao kwa kufungua na kuanzisha shughuli za ujasiriamali kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuingia kwenye soko la ushindani.

Aliwashauri vijana hao kujiunga kwenye vikundi ili wanufaike na fursa mbalimbali za mikopo ikiwamo ile inayotolewa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani.

Katika risala yao vijana waliohitimu mafunzo ya fani mbalimbali ileleza umuhimu wa mradi wa Youthbuild kuwa daraja la kuwatoa sehemu moja kwenda nyingine kwani imewaongezea ujuzi na maarifa ambayo yanawasaidia kupambana na umaskini.





# Askofu akemea kugeuza watoto kitega uchumi

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

ASKOFU wa Kanda ya Kati Kanisa la PHAM (T), Julius Bundala, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawaendeleza kielimu watoto waliohitimu elimu ya msingi mwaka huu badala ya kuwafanya vitega uchumi vya familia.

Askofu Bundala alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini kwenye Kongamano la Wanawake Kanda ya Kati wa kanisa hilo lililofanyika Mlali wilayani Kongwa.

Alisema kwa sasa watoto hao wamehitimu elimu ya msingi na wanasubiri matokeo, lakini imekuwa ni tabia kwa baadhi ya wazazi kuwafanya kitega uchumi badala ya kuwaendeleza kielimu.

"Unakuta mzazi au mlezi yeye anawaza tu mtoto wake wa kike aolewe au kuwatafutia kazi za ndani huku anawaza mtoto wakiume achunge mifugo, hili jambo halikubaliki, huku ni kuwafanya watoto vitega uchumi vya familia," alisema.

Askofu huyo alisema wazazi wana wajibu wa kuhakikisha watoto hao wanapata haki za msingi za kuwaendeleza kielimu pamoja na elimu ya kiroho ili watimize ndoto zao.

Alisema badala ya wazazi kuwaza kupata fedha kupitia watoto hao na kuwapa majukumu ya kutunza familia, ni wajibu wao kuwapa haki zote za msingi zitakazowasaidia kutimiza ndoto zao.

Alisema kutoendeleza watoto kielimu kumekuwa kukisababisha umaskini miongoni mwa familia nyingi. "Ninawaomba wazazi wenzangu, tusiwakatili watoto wetu hawa kwa kutowaendeleza kimasomo, wapeni haki zao kwa kuwa hao ndiyo viongozi wetu tunaowategemea kushika nafasi mbalimbali zikiwamo za kiserikali, kidini na hata za kisiasa," alisema.

Askofu huyo alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imeondoa mzigo mkubwa kwa upande wa wazazi kwenye ada na michango ambayo ilikuwa ikilalamikiwa.

Mwenyekiti wa kina mama wa kanisa hilon (WIHA) Kanda ya Kati, Matilda Mwakibete, aliwataka wanawake kuachana na mfumo wa utegemezi, badala yake watumie fursa zilizopo kufanya kazi za mikono ili wajikomboe kiuchumi.

Pia, aliwataka wanawake wa kanisa hilo kuliombea taifa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ili lipate viongozi bora.



Diwani wa Kata ya Buigiri, katika Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Chinangali jana, wakati wa tamasha la utamaduni wa ngoma za asili wakati alipokuwa akihamasisha umuhimu wa kujiunga na bima ya afya iliyoboreshwa (CHF). **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Klabu zaundwa kudhibiti mimba utotoni Dodoma

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KUTOKANA na Mkoa wa Dodoma kukabiliwa na changamoto ya mimba za utotoni kwa asilimia 39, Taasisi ya Maendeleo ya Vijana mkoani humo (Doyodo) imeanzisha klabu 118 kupambana na changamoto hiyo.

Mkurungenzi Mtendaji wa Doyodo, Rajabu N'hunga, alieleza mkakati huo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mapambano dhidi ya mimba za utotoni.

N'hunga alisema klabu hizo zinalenga kuhakikisha elimu kuhusu madhara ya mimba za utoto inatolewa kwenye shule na jamii. Alisema klabu za wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zilizoundwa ni 78 na klabu za makundi mbalimbali ya kijamii 40.

Alizitaja shule ambazo zitakuwa na klabu hizo kuwa ni Shule za Sekondari ya Chinangali, Lukundo, Miyuji, Nzuguni, Kiwanja cha Ndege na Shule ya Msingi Mlimwa C.

N'hunga alisema wameunda klabu katika maeneo ya Kata za Chang'ombe, Miyuji, Nzuguni na Mnadani kwa kushirikisha makundi rika mbalimbali.

Alisema wanafunzi 3,025 wamefikiwa kwa kupewa elimu ya kujikinga na mimba.

Meneja Mradi wa Doyodo, Charles Ruben, aliitaja mipango mikakati ya taasisi hiyo kuwa ni pamoja na kuboresha huduma za afya kwa vijana katika maeneo ya mradi na kuwaunganisha wadau mbalimbali wanaohusika na huduma za afya ili kutokomeza mimba za utotoni.

Ruben alisema taasisi hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na waratibu elimu kata, walimu wa shule husika, Ofisi ya Jiji, wilaya na mkoa,Waratibu wa afya Kata hadi Mkoa,waratibu wa huduma rafiki kwa vijana pamoja na maofisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata hadi Mkoa.

# Wataka mgombea binafsi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya vijana wameishauri serikali kuruhusu mgombea binafsi katika uchaguzi mkuu ujao ili kuwapa fursa watu wengi kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa.

Vijana hao walitoa rai hiyo jijini hapa jana waliposhiriki majadiliano juu ya changamoto zinazowakabili vijana wakati wa uchaguzi yaliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Vijana Kibaha (YPC).

Mmoja wa vijana hao, Adolphus Mushumbusi, alisema uwapo wa nafasi ya mgombea binafsi katika uchaguzi nchini utawasaidia vijana wasio kwenye vyama vya siasa kupata fursa ya kugombea.

Alidai hivi sasa ndani ya vyama vya siasa kumekuwa na changamoto ya vijana kutopewa fursa za kugombea nafasi za udiwani na ubunge.

"Vyama vingi hivi sasa bado haviwaamini vijana, nafasi nyingi bado zinachukuliwa na wazee, hivyo vijana wengi kushindwa kupata nafasi na kutimiza ndoto zao," Mushumbusi alisema.

Aliongeza kuwa kukiwa na mgombea binafsi, kutawasaidia vijana kupata fursa ya kugombea na kupenya katika kupata nafasi mbalimbali zitakazowasaidia kutimiza ndoto zao.

Mtoa mada katika mjadala huo ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba (Jukata,) Hebron Mwakagenda, alisema kuna haja siku ya kupiga kura kusiwe na shughuli nyingine, yaani iwe kama sikukuu.

"Nchi kama Kenya na Zambia, Rais wao ndiyo huwa anatangaza siku ya kupiga kura na katika siku hiyo hakuna shughuli nyingine zaidi ya kupiga kura ili kuwapa watu wengi fursa ya kuchagua viongozi wao," Mwakagenda alisema.

Aliongeza kuwa utaratibu unaotumia nchini wa kupiga kura Jumapili umekuwa ni moja ya changamoto kwa watu wengi kushindwa kupiga kura kutokana na kuwa kanisani.

"Kama mnavyofahamu, kuna baadhi ya makanisa yanaongozwa na roho mtakatifu, mkiingia, kutoka ni majaliwa, hivyo ule muda wa kupiga kura ambao unaishia saa 10 jioni, wengi hawawezi kuwahi vituoni kupiga kura na kutimiza haki yao ya msingi," alisema.





# Wanawake Zanzibar hawafaidiki matumizi ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya kuwapo zaidi ya sheria 10 za umiliki wa ardhi na usimamizi wake, bado ni asilimia 27 pekee ya wanawake wanaomiliki ardhi Zanzibar.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar unaonyesha kwamba wanawake bado hawajafaidika na matumizi ya ardhi kwa shughuli za makazi, kiuchumi pamoja na uwekezaji.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Asha Abdi Makame, alisema Sheria za Ardhi hazimbagui mwanamke kumiliki ardhi na zimeweka bayana umuhimu wa kila mwananchi kumiliki ardhi kwa matumizi yake ikiwamo makazi.

Alisema hata sheria za dini ya Kiislamu imeweka bayana umuhimu wa mwanamke kumiliki ardhi ikiwamo kwa njia kurithi.

"Utafiti tuliofanya katika mradi wa umiliki ardhi kwa wanawake unaonyesha kwamba bado wanawake wapo nyuma katika kumiliki ardhi kwa shughuli mbalimbali ikiwamo za kiuchumi na uwekezaji," alisema.

Naye Dawa Hassan, mkazi wa Kikungwi, Wilaya ya Kati Unguja, alisema amefuatilia uhaulishaji wa ardhi kwa muda wa miaka mitatu bila ya mafanikio na sasa amekata tamaa.

"Fomu yangu tayari ipo katika uhaulishaji wa ardhi, lakini kila ukienda utaambiwa bado tunaifanyia kazi na sasa nimekata tamaa kwa sababu natumia nauli kutoka kijijini hadi mjini," alisema.

Kwa upande wake Cisilia Simon, mkazi wa Bungi, alisema mchakato wa kupata hati miliki pamoja na uhaulishaji wa ardhi haufahamiki vizuri, mtu hulazimika kutumia fedha nyingi bila risiti.

"Zipo gharama ambazo unalazimika kutoa risiti zinazokwenda moja kwa moja serikalini, lakini zipo gharama za kuchukua gari na kutoa mafuta zaidi ya Sh. 30,000 ambazo hizo hazina risiti," alisema.

# Wahimizwa utamaduni wa usafi kwenye fukwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahamoud, amewataka wamiliki wa hoteli za kitalii katika mkoa huo kujenga utamaduni wa kusafisha fukwe za bahari zilizopo karibu na hoteli zao ili kulinda na kuhifadhi mazingira ya maeneo hayo.

Alisema endapo wenye hoteli watakuwa na utaratibu huo iliyojijengea hoteli ya Protea wa kusafisha fukwe na kuondosha taka ngumu za plastiki, kutafanya fukwe hizo kuwa safi na kuwavutia wageni na kufikia malengo ya serikali ya kuimarisha sekta ya utalii.

Ayoub alitoa kauli hiyo wakati wa kufanya usafi katika hoteli hiyo iliyopo Mbweni, Wilaya ya Magharibi B Unguja na kulishirikisha Baraza la Manispaa ya Magharibi B.

Alisema usafi wa mazingira utatunza uoto wa asili kama miti ya mikoko.

Alisema utamaduni walioujiwekea katika hoteli hiyo unafaa kuigwa na hoteli nyingine za kitalii na kuondoa taka ngumu pia kupunguza athari kwa viumbe vinavyoishi baharini.

Ayoub alisema sekta ya utalii imekuwa ikiingiza fedha nyingi za kigeni na kukuza uchumi wa nchi, hivyo fukwe za bahari ndio moja ya kivutio kikubwa kwa wageni wengi wanaokwenda kutembea Zanzibar.

Aliupongeza uongozi wa hoteli hiyo kwa utaratibu mzuri wa kufanya usafi kwenye fukwe kila mwaka hatua inayohifadhi na kutunza mazingira ya bahari.

"Nimeridhishwa na utaratibu huu kwa kweli niupongeze kwa dhati uongozi wa Protea, Serikali ya Mkoa kupitia Baraza la Manispaa tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na hoteli hii ili kuona utaratibu huu wa usafi unaendelea kwa kuwa pia ni jukumu letu la msingi kupitia manispaa zetu," alisema Ayoub.

Meneja wa hoteli hiyo, Nico Balinda, alisema uongozi wa hoteli hiyo umekuwa na utaratibu wa kawaida ya kufanya usafi kila mwaka kwa kuwa wanatambua umuhimu wa fukwe na utunzaji wa mazingira kulingana na huduma wanazozitoa kwa wageni.

"Sisi kama watoa huduma hususani kwa wageni kwa maana ya watalii wanaoingia nchini suala la usafi ni kipaumbele chetu pamoja na utunzaji wa mazingira maana biashara tunayoifanya usafi ni jambo la msingi na tutaendelea na utaratibu huu," alisema Balinda.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Magharibi B, Ali Abdallah Natepe, alitoa wito kwa jamii kuendelea kushirikiana na baraza lake la manispaa katika suala la usafi wa mazingira na fukwe kwa walio karibu na maeneo ya bahari.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Waziri anayeshughulikia mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Indonesia, Rini M. Soemarno, wakati alipofika Ikulu Mjini Zanzibar jana, akiwa na ujumbe wake. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mswada Sheria ya Utawala wa Baraza kujadiliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa 15 Baraza la tisa la Wawakilishi unatarajiwa kuanza leo kwa Miswada ya kisheria mitatu kusomwa kwa mara ya pili.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanatarajia kujadili Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi na mambo mengine yatakayohusiana na hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Msellem, alisema miswaada hiyo ni miongoni mwa iliyosomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa mwezi Mei mwaka huu na utasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa.

Alisema, malengo na madhumuni ya Mswada huo ni kuwa na sheria inayohusiana na Baraza la Wawakilishi.

"Kama taasisi nyingine zilizoanzishwa na kuwekwa kwa sheria basi na sisi tunataka nguvu ya kisheria uwapo wa baraza hili, mbali ya nguvu ambayo ipo kisheria zaidi ya kikatiba tunaithamini na kuikubali, lakini pia kuna taratibu za ndani na mambo mengine ambayo yanahusu uendeshaji, uongozi wa baraza hili hivyo kuwapo kwa sheria yake ni muhimu sana.

Katibu Raya, alisema Mswada mwingine ni kufuta sheria ya viongozi wa kitaifa namba 10 ya mwaka 2002 na kutunga sheria inayoweka utaratibu wa kuwaenzi viongozi wa kitaifa na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada mwingine ni sheria ya kuanzisha Jumuiya ya Mawakili Zanzibar, kuweka malengo, utekelezaji wa shughuli za jumuiya na mambo mengine.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Mussa Kombo Bakari, alisema mambo mengine yalikuwa yakifanywa kwa mujibu wa sheria na mengine yakifanywa kwa mujibu wa kanuni.

Alisema, mswada huo umetambua uongozi wa Baraza ambao hivi sasa utawekwa kwa mujibu wa sheria.

"Uongozi wa Baraza hata kama haukutajwa katika sheria, lakini umetajwa katika maeneo mengine ikiwamo kwenye Katiba na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, lakini sasa imewekwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

"Kwa mfano atatajwa Spika, Naibu Spika Katibu wa Baraza na Wenyeviti wa Baraza basi, mswada unaeleza kuhusu viongozi hao, lakini viongozi hao wameshatajwa katika Katiba na pia katika Kanuni za Baraza kwa sababu hatukua na sheria huko nyuma, sasa tunaelekea kuwa na sheria na imewaeleza," alisema.

Hata hivyo, alisema yapo mambo ambayo hayakuwapo katika Sheria, Katiba wala Kanuni ikiwamo kutunza misingi ya historia ya Baraza la Wawakilishi jambo ambalo halikuwa likitajwa katika Katiba na maeneo mengine ya Kanuni za Baraza. "Mswada huu unajaribu kuweka na kutunza historia ya shughuli za Baraza zinazofanywa katika vipindi mbalimbali vilivyopita," alisema. Alisema eneo lingine ni kuwaenzi viongozi mbalimbali waliolitumikia Baraza la Wawakilishi jambo ambalo halikuwamo katika Katiba wala kanuni za Baraza, lakini sheria hiyo itaweka utaratibu huo na kutambua mchango wao.

Akizungumzia kuhusu nafasi na michango ya wadau katika miswada ya sheria, alisema wana mchango mkubwa pamoja na kutofikia katika kiwango cha juu.

"Wadau wanatusaidia sana kwa kuwa Baraza linaalika wadau kwa mfano sheria inahusu sekta ya mifugo basi tasisi mbalimbali zinazoshughulikia mambo hayo zinatoa michango yao na inasaidia kwa kiasi kikubwa kuiweka miswada yetu katika hali nzuri," alisema.

Katika mkutano huo pia jumla ya maswali 137 yataulizwa na kujibiwa, kuwasilishwa ripoti za wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati za kudumu za Baraza kwa mwaka 2018/2019 na mengineyo kwa ruhusa ya Spika.

# Waziri Mkuu aagiza gari la wagonjwa kupelekwa Ifakara

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupeleka gari la kubebea wagonjwa katika kituo cha Afya cha Kibaoni kilichopo Halmashauri ya Mji wa Ifakara ili kuwapunguzia wananchi gharama ya kukodi gari kwa Sh. 800,000 pale wagonjwa wao wanapopata rufaa.

Wananchi wa Mji wa Ifakara wameiomba Serikali iwasaidie kuwapatia gari la wagonjwa kwani kituo chao hakina gari na wagonjwa wao wanapopata rufaa ya kwenda hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro wanalazimika kukodi gari kutoka hospitali ya Mtakatifu Francis kwa gharama ya Sh. 80,000 ambazo baadhi yao wanashindwa kuzimudi.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Mji wa Ifakara katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa kituo cha mabasi cha mji huo. Amesema iwapo fedha za makusanyo ya mapato ya ndani katika halmashauri husika zingekuwa zinatumika vizuri kusingekuwa na changamoto kama hizo.

Alisema Serikali imedhamiria kuboresha huduma za afya kwa wananchi, hivyo amewataka wananchi hao kuendelea kuwa na imani na Serikali yao. "Nitampigia simu Waziri Ummy (Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) katika mgawo ujao alete gari la wagonjwa hapa."

Pia, Waziri Mkuu aliielekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI ihakikishe katika mgawo wa ujenzi wa hospitali za wilaya, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ipewe kipaumbele kwa sababu eneo hilo ni kubwa na lina watu wengi lakini hakuna hospitali ya wilaya hivyo kusababisha msongamano mkubwa katika kituo cha Afya cha Kibaoni.

"Nimetembelea mwenyewe kituo cha Afya cha Kibaoni na nimeshuhudia msongamano wa wagonjwa, mgawo wa pili wa ujenzi wa hospitali za wilaya Mji wa Ifakara lazima upewe kipaumbele. Suala la huduma za afya ni suala nyeti, hivyo ujenzi wa hospitali hiyo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi."

Awali, Mganga Mfawidhi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Dkt. Happyness Ndosi alisema Kituo cha Afya cha Kibaoni kinapokea na kuwahudumia wagonjwa wa nje 225 hadi 250 kwa siku na wagonjwa wanaolazwa ni kati ya 50 hadi 80 kwa siku. Wakinamama wanaojifungulia kituoni hapo ni 400 kwa mwezi.

Akizungumzia changamoto zinazikabili kituo hicho, alisema kina upungufu wa watumishi 92, kwani kina jumla ya watumishi 83 huku mahitaji yakiwa ni watumishi 175, ukosefu wa gari la wagonjwa na pia hakina gari lolote la kutolea huduma zikiwemo za chanjo, na usambazaji, uchakavu kwa baadhi ya majengo kama la wagonjwa wa nje.

Pia, kituo kinakabiliwa na ukosefu wa jengo la kutunzia watoto njiti, watoto wachanga na wale wanaohitaji uangalizi maalumu baada ya kuzaliwa (neonatal unit), ufinyu wa chumba cha kujifungulia pamoja na ukosefu wa mashine ya kutolea dawa za usingizi (anesthesia machine).

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amesema Serikali haitokuwa na msamaha na watendaji wa halmashauri watakaobainika kutafuna fedha za makusanyo ya mapato ya ndani pamoja na fedha zinazotolewa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Fedha za mapato ya ndani hazitumiki vizuri watu wanadukua mifumo, wanapaswa watambue kwamba Serikali ipo makini wakati wote. Watumishi wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo vya ubadhilifu hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao. Watumishi wa umma mnatakiwa kutekeleza majukumu yenu kwa weledi."



Mjumbe wa Baraza la Jumuiya ya Wazazi ya CCM Taifa, Mkoa wa Mara, Julius Masubo, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wazazi la Wilaya ya Musoma cha kukabidhi hati ya heshima kwa Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (hayupo pichani), kwa kutambua mchango na utendaji wake katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020 katika kijiji cha Chumwi, jimboni humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yalaumiwa malezi ya watoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI wa Shehia ya Chonga Wilaya ya Chake Chake, Pemba, wamesema jamii bado haijawa tayari kurejesha malezi ya zamani ya kushirikiana kwa lengo la kudhibiti udhalilishaji.

Wakizungumza na Nipashe, walisema bado jamii haijaona umuhimu wa malezi ya pamoja, jambo ambalo linasababisha ongezeko la vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

Walisema ipo haja kwa wazazi na walezi kurejesha malezi ya kale ya kushirikiana pamoja kuwalea watoto wao, ili wawe watoto bora na wenye maadili mema, jambo ambalo litasaidia kuondosha udhalilishaji ndani ya jamii.

"Kila siku tunasema tu mdomoni kuwa, ili tudhibiti janga la udhalilishaji tuwe na malezi ya pamoja, lakini bado hatujawa tayari katika nafsi zetu," alisema Ali Juma Nte mkaazi wa shehia hiyo.

Aidha Ali aliwashauri wazazi wa shehia hiyo kutowapa fursa vijana wa kiume kuweka magenge mtaani, kwani ndio chanzo kikubwa cha kuzalisha uhalifu na baadae kuwadhalilisha watoto wa kike.

Hidaya Yussuf Salim, alisema katika shehia yao kumekuwa na madanguro, ambapo vijana wa kiume huwachukua watoto wa kike na kuwaingiza humo na kuwadhalilisha, jambo ambalo linawatia hofu siku hadi siku.

"Kwa kweli muda wote tuna wasi wasi na watoto wetu maana kuna nyumba maalumu ambazo watoto wetu wa kike huingizwa na kubakwa, tunahitaji kusaidiwa jamani," alisema.

Rahia Mohamed Haji, alisema, kitu kingine kinachochangia udhalilishaji ni kuwapa uhuru mkubwa watoto, kwani wamekuwa na fursa kubwa ya kufanya wanalolitaka bila kuogopa wazazi wao.

Afisa Wanawake na Watoto Wilaya ya Chake Chake, Salma Khamis Haji, aliwataka wazazi kuwashughulikia watoto wao kwa kila hatua, ili kujua matatizo yanayowakabili na kuweza kupatiwa ufumbuzi kwa haraka.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Wanawake Pemba, Mwanaisha Ali Massoud, aliwataka wazazi kufuatilia mienendo za watoto wao, ili kujua na kutambua mabadiliko yao ya tabia.

Kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu, jumla ya kesi 45 za udhalilishaji zimeripotiwa katika Ofisi ya Wilaya Chake Chake, ambapo mwaka jana kuanzia julai hadi Disemba ziliripotiwa kesi 30.

## BancABC yazindua akaunti inayonufaisha mteja mwezi kwa mwezi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya BancABC Tanzania ambayo ni kampuni tanzu ya Atlas Mara, imeendelea kudhihirisha ubunifu wake katika huduma zinazowanufaisha wateja wake baada ya kutangaza kuzindua akaunti mpya ya IZZE ambayo ni rahisi kufungua na haina makato yeyote ya mwezi.

Kwa kupitia akaunti ya IZZE ya Bancabc, mteja anahitaji kuwa na kitambulisho cha taifa tu kilichotolewa na NIDA ili kufungua akaunti hiyo, na atapata riba hata akiwa na kianzio cha Sh. 10,000.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa kuzindua akaunti hiyo, Mkurugenzi wa Biashara na Wateja wadogo na wakati wa benki BancABC, Joyce Malai, alisema: 'Leo kwenye soko la biashara watu wengi wanaangalia sehemu watakayo nufaika kuwekeza fedha zao na yenye uhakika wa kupata faida/manufaa kadhaa. Uhakika wa kupata faida au manufaa ni moja ya malengo muhimu kwa kila Mtanzania.

"Vile vile, kufungua akaunti ya benki kwa siku hizi imekuwa ikichukuliwa kama hatua ngumu yenye kuhitaji muda na zaidi inaonekana kama inalenga watu wenye kipato kikubwa. Sisi BancABC tumelifanyia kazi suala hilo na ndio sababu tumekuja na akaunti ya IZZE ambayo ni rahisi kufungua kwani mteja anaweza kufungua akaunti hii hata kupitia mawakala wetu popote nchini."

Malai aliongeza kuwa akaunti ya IZZE ni rahisi kufungua kama ilivyo jina lake. Mteja anahitajika kuwa na kitambulisho cha taifa tu na haina kiasi chochote cha kuanzia, haina makato ya mwezi, na muhimu zaidi ni kwamba mteja anapata riba kila mwezi ikiwa ana salio kuanzia shilingi 10, 000 au zaidi kwenye akaunti yake.

Meneja wa huduma za uwakala wa benki hiyo, Mwita Rhobi, alisema kuwa BancABC imewawezesha mawakala ambao wanapatikana nchini kote kusaidia zoezi la ufunguaji wa akaunti ya IZZE.

HABARI KIMATAIFA

# Waisraeli waamua hatma ya Netanyahu kwa kura

**YERUSALEMU,** Israel

KATIKA kinyang'anyiro cha uchaguzi nchini Israel, Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu anawania kwa mara nyingine kiti chake, ikiwa ni muhula wake wa nne.

Wananchi nchini Israel wameanza kupiga kura katika uchaguzi utakaoamua iwapo Waziri Mkuu wa sasa, Netanyahu ataendelea kuwamo madarakani, huku akiwa katika wasiwasi wa kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kuhusika na ufisadi.

Waziri Mkuu huyo ambaye amekuwamo madarakani kwa muda mrefu zaidi kuliko mwengine yeyote anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Jenerali mstaafu, Benny Gantz.

Chama cha Jenerali huyo mstaafu cha Bluu na Nyeupe kiko sambamba na chama cha Netanyahu cha Likud.

Hata hivyo, vyama hivyo vitalazimika kuunda mseto na vyama vidogo itakapotakiwa kuunda serikali.

Jana asubuhi Rais wa Israel, Reuven Rivlin alipiga kura katika Mji wa Jerusalem na kusema kuwa: "Leo israel inasherehekea demokrasia".

**Chama cha Liebermann ndicho kinachotarajiwa kuwa muhimu kabisa katika hesabu za kuunda serikali.**

Waziri Mkuu Netanyahau amejinadi kuwa yeye ni kiongozi mwenye sifa za kipekee za kuiongoza nchi katika nyakati za changamoto.

Lakini mshindani wake Jenerali mstaafu, Gantz anamzungumzia Netanyahu kama Waziri Mkuu anayeigawanya nchi na pia mwanasiasa anayeandamwa na kashfa. Gantz anajinadi kama mtu mtulivu na mwadilifu.

Wakati anapiga kura, Gantz alisema: "Waisraeli leo hii wanapiga kura ya mabadiliko"

Kiongozi huyo wa chama cha Bluu na Nyeupe, alisema chama chake kitafanikiwa kuleta matumaini, bila rushwa na bila kuwapo misimamo mikali.

Netanyahu na Jenerali huyo mstaafu wanapambana kwa mara ya pili kwa mwaka huu baada ya kutoka sare katika uchaguzi uliofanyika Aprili.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Netanyahu alionesha matumaini ya kuendelea kuwamo madarakani kutokana na kuungwa mkono na washirika wake wa jadi wa vyama vya mrengo mkali wa kiyahudi vinavyodhibiti viti vingi bungeni.

Lakini mshirika wake wa awali ambaye kwa sasa amekuwa hasimu wake, Avigdor Lieberman alikataa kujiunga na serikali mpya ya mseto na hivyo kupunguza viti vya serikali ya Netanyahu bungeni.

Waziri mkuu huyo alilazimika kulivunja bunge na kuitisha uchaguzi mpya.

Uchunguzi wa maoni umebainisha kwamba matokeo ya uchaguzi yanatarajiwa kuwa kama ya hapo awali.

Chama cha Liebermann ndicho kinachotarajiwa kuwa muhimu kabisa katika hesabu za kuunda serikali.

Baada ya kupiga kura Lieberman alisisitiza ahadi ya kuwezeshwa kuundwa kwa serikali ya umoja baina ya chama cha Bluu na Nyeupe na chama cha Likud. Alisema haitafanyika duru ya tatu ya uchaguzi.

Katika uchaguzi huo mfungamano wa vyama vinavyowawakilisha waarabu wa Israel pia vinatarajiwa kuwa muhimu kama iliyvokuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2015 ambapo vilishika nafasi ya tatu kwa idadi ya viti bungeni. **DW**



Raia wa Israel akipiga kura huku 'aki-self' kwenye uchaguzi wa kumtafuta Waziri Mkuu na wabunge. **PICHA: REUTERS**

# Rwanda, Uganda zakubaliana usalama

**KIGALI,** Rwanda

WAJUMBE wa serikali za Rwanda na Uganda ambao wamekutana mjini Kigali, wamekubaliana mambo kadhaa ikiwamo kujiepusha na harakati za kuyumbisha usalama katika nchi mojawapo.

Katika taarifa ya pamoja iliyokamilisha kikao hicho, Rwanda imetoa orodha ya raia wake wanaozuiliwa nchini Uganda, na serikali ya Uganda imekubali kuchunguza kwa kina taarifa hiyo, na kuhakikisha wale ambao watakutwa hawana hatia kuachiliwa huru.

Pande hizo zimekubaliana pia kusahihisha mkataba wa kuwarudisha makwao watuhumiwa wa uhalifu.

Wajumbe kwenye mkutano huo wa mjini Kigali wamekubaliana pia kuachana na tabia ya kutumia vyombo vya habari au mitandao ya kijamii, kwa kufanya propaganda ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa nchi zao.

Aidha pande zote zimesema suala la uhuru wa usafiri wa watu na vitu kwenye mpaka wa nchi zao, litajadiliwa katika kikao kingine ambacho kitafanyika mjini Kampala, baada ya kipindi cha siku 30.

Ujumbe wa Uganda kwenye mkutano huo wa Kigali ulikuwa unaongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje, Sam Kutesa, nao ujumbe wa serikali ya Rwanda ulikuwa unaongozwa na Waziri wa mashauri ya kigeni, Olivier Nduhungirehe.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Manuel Domingos Augusto, na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC, Waziri wa Mambo ya Ndani na Usalama, Gilbert Kankonde Malamba, walishiriki kwenye mkutano huo kama wawakilishi wa wasuluhishi ambao ni marais wa Angola na DRC.

Walipokutana mjini Luanda, Angola, mwezi uliopita, marais Paul Kagame wa Rwanda na Yoweri Museveni wa Uganda walikubaliana kumaliza mzozo wa kisiasa kati ya nchi zao kupitia mazungumzo. **VOA**

# Mwalimu bora duniani kutoa hotuba

**WASHINGTON,** Marekani

PETER Tabichi kutoka Kenya, aliyetuzwa Mwalimu bora duniani mapema mwaka huu, amekutana na Rais wa Marekani, Donald Trump katika ikulu ya White House huku akitarajiwa kutoa hotuba katika Baraza kuu la Umoja wa Mataifa.

Tabichi, ni mtawa wa Shirika la kikatoliki la Mtakatifu Fransisco wa kapuchini na alishinda tuzo ya mwalimu bora duniani Machi, 2019.

Tabichi anafundisha masomo ya sayansi katika shule ya mseto ya upili ya Keriko katika Jimbo la Nakuru, Kaskazini Magharibi mwa Mji Mkuu, Nairobi.

Picha ya Tabichi akikutana na Rais Trump iliwekwa na ofisa wa mawasiliano kutoka ikulu kwenye mtandao wa kijamii waTwitter ambaye alisema: "Tabichi alitoa " 80% ya mshahara wake kwa mwezi kuwasaida masikini nchini mwake Kenya"

"Uwajibikaji wake na kazi yake ngumu na imani kwa talanta ya wanafunzi, imeifanya shule anayofunza kuibuka kidedea baada ya kushindana na shule zilizo bora nchini katika mashindano ya kitaifa ya sayansi".

"Peter, unatutia moyo sisi sote! Asante kwa uwajibikaji wako kwa wanafunzi wako".

Tabichi anatarajiwa kutoa maombi kabla ya kuanza kwa kikao cha Baraza kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York.

Pia anatarajiwa kuzungumzia kuhusu namna alivyofanikiwa kufika alipofika katika taaluma ya uwalimu.

Tabichi amenukuliwa kusema kwamba: "Hii ni heshima kubwa kwa watawa wa St. Franciscan. Inaonyesha kuwa Umoja wa Mataifa unatutambua kutokana na kwamba ina jukumu kuu katika kuendeleza utu."

Katika tuzo hiyo iliotolewa katika shindano lililoandaliwa na Wakfu wa Varkey, Peter aliwapiku washiriki wengine 10,000 waliochaguliwa kutoka nchi 179.

Peter anasema: "kuna changamoto ya ukosefu wa vifaa katika shule yake ukiwamo uhaba wa vitabu na walimu".

Madarasa yenye uwezo wa kuwa na wanafunzi kati ya 35 hadi 40 hulazimika kuwa na wanafunzi 70 na 80, jambo analosema linamaanisha kuwa darasa linakuwa na wanafunzi wengi kupita kiasi, na ni tatizo kwa walimu.

Ukosefu wa mtandao wa kuaminika unamlazimisha kusafiri hadi kwenye 'Cyber-café' kwa ajili ya kupakua maelezo ya masomo yake ya sayansi.

Na wanafunzi wengi hutembea zaidi ya maili nne kwenye barabara mbovu kufika shuleni. Lakini Peter anasema ameazimia kuwapatia fursa ya kusoma na kufikia ndoto zao. **BBC**

# Boti yasababisha tafrani abiria Ziwa Victoria

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

ABIRIA 56 wamenusurika kifo baada ya boti waliyokuwa wakisafiria kutoka Bandari ya Kemondo katika Ziwa Victoria wilayani Bukoba kuelekea Rushonga Bumbire wilayani Muleba mkoani Kagera kuwaka moto na kubadili uelekeo, na kusababisha tafrani kubwa kwa abiria.

Shuhuda wa tukio hilo aliyekuwa katika boti hiyo, Michael Dominick mkazi wa Isamilo Mwanza, alisema umbali mfupi baada ya kuanza gafla ulitokea mlipuko mkubwa eneo la nyuma ya boti kwenye injini .

Alisema mlipuko huo ulisababisha moto mkubwa uliogeuza mwelekeo wa boti kwa sababu ya upepo na kurudi bandarini ilikotoka, huku abiria wakipiga kelele kuomba msaada na wengine kurukia majini kuogelea ili kujiokoa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema boti hiyo iljulikana kwa jina la Lulimbe ikiwa imebeba abiria 56 pamoja na mizigo, ilianza safari saa 8:00 mchana Septemba Jumatatu.

Kamanda Malimi alisema boti hiyo ilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 84, aliki ilikuwa na abiria 56 waliookolewa na wananchi waliokuwa nchi kavu, na kuwa wengine waliweza kujiokoa kwa kuogelea majini.

Aliongeza kuwa katika tukio hilo walibainika majeruhi watatu Elizabeth Msiwa (28), Agnes Wiliam(42) mkazi wa Katoro Busesere wilayani Chato mkoani Geita na Mariam Deus (30) ambao walikimbizwa katika hospitali ya Mtakatifu Joseph Kagondo ili kupatiwa matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliwapa pole manusura wa ajali hiyo na kuzungumza na wananchi katika eneo la tukio pamoja na kuwasisitiza kuhakikisha wanazingatia usalama wao wakati wa kusafiri kwa kuvaa majaketi ya kujiokoa.

"Pia na nyinyi wananchi mtusaidie sisi Serikali kwa kuhakikisha mnavikagua vyombo hivi kabla ya safari... mkivitilia shaka toeni taarifa kwa mamlaka husika ili tuweze kudhibiti ajali hizi kabla ya kutokea," alisitiza Gaguti.

Aliwataka wakaguzi wa vyombo vya usafiri majini kuhakikisha wanavikagua kikamilifu kabla ya kuanza safari na pamoja na kutolea taarifa kwa vyombo husika ili kuweza kudhibiti kabla ya kusubilia kutoka.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Ng'ilabuzu Ludigija, wakisaini mkataba wa makubaliano wa mikopo ya uwezeshaji kwa wajasiriamali wamachinga, katika hafla iliyofanyika wilayani Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Sarah Msafiri. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Adaiwa kujirusha Mlima Kilimanjaro na kufariki

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MUONGOZA watalii Thomas Meela (58), mkazi wa Marangu katika Wilaya ya Moshi, anadaiwa kusababisha kifo chake kwa kujirusha kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Hamisi Issah, alithibitisha kuwa Meela alifariki dunia kutokana na kujirusha mlimani baada ya kufikisha wageni katika kilele cha Uhuru.

Wakati Jeshi la Polisi likieleza kwamba uamuzi wa Meela wa kujiua huenda ulitokana na homa ya mlima, kuna taarifa zisizo rasmi kutoka kwa baadhi ya waongoza watalii wenzake, kwamba marehemu alikuwa katika msongo wa mawazo kutokana na masuala ya kimapenzi baina yake na mzazi mwenzie ambaye hawakutaka kutaja jina lake.

Katika taarifa ya Polisi, Kamanda Issah ameeleza kuwa Meela kabla ya kufariki dunia alikuwa ana safari ya siku sita ya kipanda mlimani na wageni.

Alisema alipofika katika kilele cha Uhuru, aliwaacha wageni na kuwaeleza wapagazi aliokuwa nao kwamba yeye hatarudi chini.

Baada ya dakika chache aliwaacha akielekea kama anaenda kuvuta sigara, lakini hawakumuona tena hadi alipopatikana akiwa amefariki dunia.

Mwili wa muongoza watalii hao unadaiwa kuopolewa Septemba 15, mwaka huu na kuhifadhiwa katika Hospitali ya Misheni ya Kilema.

Kwa mujibu wa Kamanda Issah uchunguzi wa kina kuhusiana na tukio hilo bado unaendelea.

**Alipofika katika kilele cha Uhuru, aliwaacha wageni na kuwaeleza wapagazi aliokuwa nao kwamba yeye hatarudi chini.**

# MCF, NMB kukopesha wamiliki hospitali binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kutanua wigo wa wadau wa Sekta ya Afya nchini kukabiliana na changamoto zinazoikabili nyanja hiyo, Benki ya NMB kwa kushirikia na Shirika la Medical Credit Fund (MCF), imezindua huduma maalum ya mikopo nafuu kwa wamiliki wa hospitali binafsi, vituo vya afya na zahanati.

Uzinduzi wa huduma hiyo ya 'NMB Afya Loan,' ulifanyika jana katika Hospitali ya Heameda Medical Clinic, iliyopo Bunju B jijini Dar es Salaam, ambapo NMB itatoa mikopo kuanzia Sh. milioni 2 hadi Sh. bil. 5, wakati MCF inatoa dhamana ya asilimia 50 katika mikopo yote.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Filbert Mponzi, wanufaika wakuu wa Mkopo wa Afya ni hospitali binafsi, vituo vya afya na zahanati, maduka ya dawa na wasambazaji wa dawa ili kuwezesha, kuiinua na kuboresha biashara za huduma za afya nchini.

Mponzi alibainisha kuwa, ushirikiano baina ya NMB na MCF (aliowataja kama wabobevu wa Sekta ya Afya), unaihakikishia jamii ya Watanzania huduma bora za afya kutoka katika vituo, zahanati na hospitali zote zitakazoamua kufanya aina hiyo ya uwekezaji.

Aliongeza kuwa hadi uzinduzi unapofanyika, zaidi ya vituo vya afya, zahanati na hospitali 200 zimeshachukua mikopo ya afya, huku akiwataka wadau walioamua kuwekeza katika sekta ya afya, kuchangamkia Afya Loan ili kujenga misingi ya huduma bora za kitabibu.

"Kuna fursa nyingi katika Sekta ya Afya nchini na NMB, tumeliona hili na tumejikita kuwapa nafasi hospitali, vituo vya afya wasambazaji wa vifaa tiba kujiendeleza. Tuna imani huduma hii itachangia kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa afya za bei nafuu," alisema Mponzi.

Naye Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Elisha Osati (ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo), aliwataka madaktari na wadau wa sekta hiyo kuchangamkia Huduma ya Afya Loan, ili kutanua wigo wa ajira ili kukabiliana na ongezeko la madaktari wapya katika soko la ajira.

Osati alisema kumekuwa na madaktari wengi wapya wanaotokea vyuoni, ambao wanapata wakati mgumu katika soko la ajira na kwamba Afya Loan inaenda kuwapa fursa ya kuajiriwa na wadau watakaotumia mikopo hiyo kuanzisha hospitali, zahanati na vituo vya afya.

Aliitaka NMB kufanya mazingatio makubwa katika riba ya mikopo hiyo, ili kutoa nafasi kwa wadau wengi kujitokeza kukopa na kuboresha sekta ya afya na kujenga Tanzania yenye jamii inayomudu kukabiliana na changamoto za afya kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Mkazi wa MCF, Dk. Heri Marwa, alisema Afya Loan imeboresha Sekta ya Afya katika nchi za Afrika zinazohudumiwa na shirika hilo lenye Makao Makuu nchini Uholanzi, akizitaja kuwa ni Liberia, Nigeria, Ghana, Kenya, Uganda na sasa Tanzania.

Alisema MCF ni shirika linalojiendesha kwa kutotegemea faida, bali kujali afya na ustawi wa jamii na kwamba hiyo ndio siri ya kutoa dhamana ya asilimia 50 ya mikopo yote itakayotolewa na NMB kupitia Afya Loan, ili kwenda kupunguza kama sio kumaliza changamoto za kitiba.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LENYE NYUMBA NDANI LINAUZWA,** Liko eneo la Lumumba Pangani mkoa wa pwani. Lina ukubwa wa heka mbili. Kwa Mawasiliano 0767332830, 0686137871, 0686807366


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

WILBART STANSLAUS NKUBA MKAZI WA KITANGILI SHINYANGA MJINI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 777 BVK AMBAYO ILIPOTEA MWAKA JANA MAENEO YA KISHAPU MKOANI SHINYANGA

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA WILBART STANSLAUS NKUBA

KWA SIMU NAMBA 0762672028

RB NAMBA SHY/RB/TR/3642/ 2018

215422402

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 64 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late DAUDI YOHANA NG'OLO**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by MARIAM LAMECK MASUNGA**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased's estate are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections (if any) to the grant should be filled on or before Day of 25th September, 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 4th THIS day of September, 2019.

215423002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 237 YA 2019**
**BAINA YA**
**PASCAL DANIEL……………………………………MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**YOHANA NKOBOCHE**
**TABU AUGUSTINO MJIMBU ……………………………WADAIWA**

**KWA:-YOHANA NKOBOCHE**
**TABU AUGUSTINO MJIMBU**
**POPOTE MLIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
**Kwa hiyo** mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 03.10.2019 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo mnatakiwa kuleta utetezi wenu kwa maandishi.
**ANGALIZO:-**Kama hamkuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa mmepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yenu.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 5 ya Mwezi wa Septemba,2019.

215422902

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 63 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late EDWARD PASPANOFU MBIDUKA**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by VICTORIA BOYSAFI MBEDUKA**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased's estate are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections (if any) to the grant should be filled on or before Day of 25th September, 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 4th THIS day of September, 2019.

215423202

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**KUMB.NA.TMC/LD/MBG/L/399**


**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA:MARIAM ABDALLAH**
**ARDHI:KIWANJA NA.399 KITALU 'L'**
**ENEO LA MBAGALA MANISPAA YA TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM**

Taarifa imetolewa Kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana,irudishwe kwa :
MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE
S.L.P.46343
DAR ES SALAAM.

P. A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

215423102

## KUPOTEA KWA VYETI



115422202

**Amanyisye Kabuje** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheto cha kidato cha nne chenye index namba **S0153-0010** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007, katika shule ya Sekondari Songea Boys, Cheti cha kidato cha Sita chenye index namba **S0134-0505** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Moshi . yeyote atakaeviona watoe taarifa kituo chchote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **PWA/KIB/RB/303147/2019**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

17/09/2019

**TANGAZO**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 18-09-2019** kampuni ya **BUSINESS TRUST TANZANIA LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA** kupitia **NANGURUKURU.**

1. Gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:
   T 821 BTA / T 143 CBY UREFU 20.0
   UPANA 4.0 KIMO 4.8

   T 908 DGB / T 854 CLY UREFU 20.0
   UPANA 4.0 KIMO 4.8

   T 900 DFZ / T 509 CCB UREFU 20.0
   UPANA 4.0 KIMO 4.8

   T 505 DNJ / T 653 CAE UREFU 20.0
   UPANA 4.0 KIMO 4.8
2. Gari hizo zinatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA kupitia NANGURUKURU.**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115423902





TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AJAX HAJUTII KUWAUZA DE JONG, DE LIGT – TADIC




**AMSTERDAM,** Uholanzi

AJAX itawakosa Frenkie de Jong na Matthijs de Ligt, lakini hawatakuwa na huzuni baada ya wawili hao kuondoka, kwa mujibu wa Dusan Tadic.

Mabingwa hao wa Uholanzi waliachana na nyota hao wawili wakati wa kukaribia kufungwa kwa dirisha la usajili wa msimu uliopita, wakati kiungo De Jong akihamia Barcelona na beki De Ligt akijiunga na Juventus.

Wawili hao walikuwa nguzo kubwa kwa Ajax kuweza kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakianza kwenye mechi 17. Vijana hao wa Erik ten Hag jana walirudi kwenye michuano hiyo ya Ulaya na walicheza dhidi ya miamba ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lille na winga Tadic anaamini kwamba bado wana uwezo wa kufikia mafanikio.

"Hatuna huzuni kwa De Jong na De Ligt kuondoka," alisema Tadic akiliambia Gazeti la Telegraph.

"Tutawakosa wao, lakini ni hatua nyingine kwa upande wao na Ajax inapenda kuwapa sapoti wachezaji ambao wanaona kwamba muda wa kuondoka umefika.

"Wote wamekwenda kwenye klabu kubwa, hakuna aliyeshangazwa. Kitu kizuri ni kwamba, kulikuwa na wachezaji wengine ambao wangeweza kuondoka na kuamua kubaki kwa sababu wana wakati mzuri zaidi hapa. Hilo ndio muhimu.

"Itakuwa ngumu kuwa bila wao wawili, lakini si kwamba haitawezekana. Bado tuna timu nzuri, bado tunaweza kushinda mataji, tunaweza kufanya vizuri Ulaya na kuna wachezaji vijana wanakuja na wataonyesha umuhimu wao.

# Lukaku kazuia Aubameyang kutua United

**LONDON,** England

IMEBAINISHWA kwamba, kuchelewa kwa Romelu Lukaku kuondoka katika Klabu ya Manchester United, ndiko kulikosababisha Pierre-Emerick Aubameyang kushindwa kutua kwa Mashetani Wekundu hao, kwa mjibu wa Daily Mail.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alikuwa na mpango wa kumsajili raia huyo wa Gabon, lakini Lukaku ndiye alikuwa kikwazo kwa kuchelewa kwenda kule Inter Milan.

Man ilikuwa ikimhitaji mshambuliaji wa kati na jina la Aubameyang ndilo lilionekana kukaa zaidi kichwani kwake na anaweza kujaribu kumsajili wakati wa dirisha dogo la usajili Januari mwakani.

Kuwapo kwa uwezekano wa kutokea kwa jambo hilo kunawapa wasiwasi mkubwa mashabiki wa Arsenal, hasa baada ya matokeo ya Jumamosi iliyopita dhidi ya Watford, kwamba yanaweza kumchochea fowadi wao huyo matata kabisa akaamua kuachana na maisha ya kuitumikia timu hiyo.

Mashabiki hao wa Arsenal walimtazama Aubameyang na mwili wake ulionekana kuchoshwa na kile kilichokuwa kikifanywa na wachezaji wenzake, kuruhusu mabao waliyofungwa kurudishwa tu kuzembe.

Arsenal ilipoteza utangulizi wake wa mabao mawili na hivyo kuambulia sare katika mchezo wa Ligi Kuu England uliofanyika juzi Jumapili, huku kukiwa na makosa mengi kwenye safu yao ya mabeki iliyoongozwa na David Luiz yakiwagharimu zaidi.

Aubameyang aliwashutumu wachezaji wenzake kwamba wanafungwa kirahisi sana, kitu ambacho kimewatisha mashabiki na kuona kwamba anaweza kuondoka, huku wakiwaza itakuwaje kama atanyakuliwa na Man United

Baada ya mechi hiyo, Aubameyang, ambaye alifunga mara mbili, alisema: "Naona kama vile tumeamua kuwapa mabao wapinzani kwa makusudi kabisa."





# 'Firmino bora zaidi ya Messi, Ronaldo'

**LONDON,** England

GIWJI Jermaine Jenas anaamini Liverpool hawatakubali kubadilishana Roberto Firmino na mchezaji yeyote yule.

Anaamini Firmino yupo kwenye daraja la juu zaidi kuliko hata nyota wawili wakali duniani, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Nyota huyo wa Brazil alionyesha ubora wake Jumamosi wakati alipotoa pasi za mwisho mbili kuisaidia Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Newcastle United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Na sasa Jenas ameibuka na kusema Firmino amefanya vitu ambavyo hakika hata Messi na Ronaldo hawawezi kuvifanya kwa sasa.

"Vitu ambavyo unaviona kutoka kwake ni vikubwa, vinavutia kuvitazama," alisema Jenas akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

Kiungo wa zamani wa Tottenham na Newcastle aliongeza: "Kwa miaka mingi amekuwa akiheshimika, lakini sasa nadhani ameifanya heshima yake kuwa juu zaidi.

"Tofauti yake na wakali wengine kama Mane au Salah au Origi hawana ule uchawi uliopo kwenye miguu yake. Kuna wachezaji mahiri, lakini huyo Firmino ni zaidi."

## HABARI MICHEZO

# Klopp: Man City ni timu bora duniani

**LIVERPOOPL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema Manchester City ni timu bora duniani.

Liverpool inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya England baada ya kuanza vizuri msimu huu na inaongoza kwa pointi tano kileleni dhidi ya City.

Lakini Klopp anaamini City ambayo imekuwa na wastani wa kubeba pointi 99 katika misimu miwili iliyopita, bado ni bora zaidi ya kikosi chake cha Liverpool.

"Hatuwezi kuwa timu bora Ulaya kwa sababu Manchester City ni timu bora duniani na hiyo ni sayari moja nilivyosikia," amesema Klopp kabla ya mchezo wake wa jana Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli.

"Kuna timu nyingi nzuri na unatakiwa kujithibitishia wewe mwenyewe kwamba ni bora kuliko mwenzako.

"Mwaka jana, tulikuwa wazuri haswa. Nina uhakika tulikuwa bora Ulaya, lakini sisi ni wazuri zaidi kwa wakati huu na ndio maana ni mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Liverpool iliifunga Tottenham mabao 2-0 kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Madrid na kushinda taji la Ulaya ambalo ni kwa mara ya sita kwao, lakini Klopp amesema timu yake haitahisi mzigo wakati wa michuano ya msimu huu kwa sababu ni mabingwa.





# DE GEA AJIFUNGA UNITED HADI 2023

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, amesaini mkataba mpya ambao utamfanya kubakia na klabu hiyo hadi mwaka 2023.

De Gea mwenye umri wa miaka 28, amecheza mechi 367 kwa United tangu Sir Alex Ferguson alipomleta klabuni hapo kutoka Atletico Madrid kwa pauni milioni 18.9 Juni mwaka 2011.

"Sasa majaliwa yamefikiwa, ninachotaka ni kuisaidia timu hii kupata matokeo kitu ambacho naamini tunaweza na kushinda mataji tena, pamoja," alisema kipa huyo raia wa Hispania.

"Umekuwa ni wakati mzuri wa kukaa miaka nane na klabu hii."

De Gea, ameichezea nchi yake ya Hispania mechi 40, pia aliisaidia United kushinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2012-13, Kombe la FA mara tatu na Kombe la Ligi na lile la Europa msimu wa 2016-17.

Mhispania huyo ambaye mara kwa mara alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Real Madrid katika misimu ya hivi karibuni, alikuwa kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake na alikuwa na uwezo wa kuanza mazungumzo na klabu nyingine nje ya Ulaya kwa ajili ya uhamisho wa Januari.

Alikaribia kujiunga na Real kwa pauni milioni 29 Septemba mwaka 2015, lakini mpango huo ulikwama dakika za mwisho.

United na De Gea walikuwa kwenye makubaliano kwa zaidi ya miaka miwili kwa ajili ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo iliongeza ofa yake Julai mwaka huu.

"Nafasi ya kuendelea kucheza soka hapa Manchester United ni nzuri na heshima kwangu," alisema De Gea, ambaye mkataba wake una kipengele cha kuongeza mkataba wake kwa siku za usoni.

# PSG kuivaa Madrid bila ya Mbappe, Edinson Cavani

**PARIS,** Ufaransa

WASHAMBULIAJI Kylian Mbappe na Edinson Cavani hawatokuwa sehemu ya kikosi cha Paris Saint-Germain, ambacho leo Jumatano kitaanza mshikemshike wa kuwania taji la Ulaya kwa kupambana na mabingwa wa kihistoria, Real Madrid.

Mbappe anaendelea kusumbuliwa na maumivu ya misuli ya paja aliyoyapata wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa mwezi uliopita dhidi ya Toulouse, huku Cavani ambaye ni raia wa Uruguay, akisumbuliwa na maumivu ya paja.

Taarifa za wawili hao kuendelea kukaa nje ya uwanja, zimethibitishwa na Kocha wa PSG, Thomas Tuchel na kuchapishwa kwenye tovuti ya klabu hiyo tajiri jijini Paris.

PSG pia watamkosa mshambuliaji wao kutoka nchini Brazil Neymar, ambaye anatumikia adhabu ya kufungiwa michezo mitatu na Shirikisho la Soka barani Ulaya (Uefa), baada ya kumtusi mwamuzi msaidizi, wakati wa mchezo wa hatua ya 16-bora dhidi ya Manchester United, msimu uliopita.

Mbappe, Neymar na Cavani kwa pamoja waliifungia PSG mabao 11 miongoni mwa mabao 20 katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Ulaya msimu uliopita, huku msimu huu wakitarajiwa huenda wakafunga zaidi, kutokana na misingi na malengo yaliyowekwa na uongozi wa klabu hiyo ya kuhakikisha wanafika mbali na ikiwezekana kutwaa taji hilo la Ulaya.



HABARI MICHEZO

# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# HAZARD: CHELSEA, REAL ZINATOFAUTIANA HAPA

## England hamna mashabiki wengi, watu pale wanapenda soka na kila...

**MADRID,** Hispania

BAADA ya mshambuliaji Eden Hazard Jumamosi kuichezea Real Madrid kwenye La Liga kwa mara ya kwanza tangu asajiliwe majira haya ya joto akitokea Chelsea, amezichambua klabu hizo mbili za Ligi Kuu Hispania na England.

**Hazard amekiri kwamba amegundua mashabiki wa Real Madrid wamewekeza zaidi kuliko wale wa klabu yake ya zamani, Chelsea.**

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, alitua Real Madrid akitokea Chelsea kwa pauni milioni 130 majira haya ya joto baada ya kuitumikia miamba hiyo ya Stamford Bridge kwa miaka saba.

"Nadhani mashabiki hapa ni mashabiki wa kweli zaidi," alisema Hazard jana kuelekea mechi yao ya leo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi dhidi ya Paris Saint-Germain.

"England hamna mashabiki wengi, watu pale wanapenda soka na kila mmoja, watu wadogo, wakubwa, makinda, wanavutiwa kweli na soka, lakini hawashangazi juu ya timu zao.

"Wakati huo nilikuwa Chelsea na tulipoteza, tulikatishwa tamaa kama walivyokuwa mashabiki, lakini sikuwahi kuhisi ni janga.

"Wakati unapokuwa Real Madrid, hata kama ni mwaka wangu wa kwanza, kuzungumzia mashabiki, mara zote wanakutarajia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya," aliendelea.

"Hiyo ndiyo maana nadhani kuna matarajio makubwa yaliyowekwa kwenye michuano hii na ndiyo maana klabu imetwaa taji hili mara nyingi zaidi ya timu nyingine."

Hazard alingojea kwa uvumilivu kuondoka Chelsea - kwanza alisema inaweza kuwa wakati wa kuendelea mbele baada ya Kombe la Dunia 2018 - lakini hiyo haikumzuia kusema juu ya hamu yake ya kwenda kuichezea Real wakati bado akiwa 'Bluu'.

"Wakati nilipokuwa Chelsea, tayari nilijua ndoto zangu ilikuwa kuichezea [Real Madrid] siku moja," alisema.

"Sikutarajia kucheza kwa miaka saba Chelsea, lakini mwishowe kila kitu kiliendа vizuri na nilikuwa na nafasi ya kushinda kila kitu kila mwaka. Nadhani ndiyo maana nilibaki pale kwa muda mrefu."

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER BADO ANAYE SANCHO

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ataendelea kumuwinda mchezaji wa Kiingereza anayeichezea Borussia Dortmund, winga Jadon Sancho, 19, na kiungo wa Leicester City, James Maddison, 22, kama kipaumbele chake majira ya joto yajayo. ***(ESPN)***

### MATIC AGOMBEWA ITALIA

AC Milan, Inter Milan, Juventus na Borussia Dortmund zote zinavutiwa na saini ya kiungo wa Manchester United, Nemanja Matic, 31, wakati mkataba wa kiungo huyo Mserbia utakapomalizika mwishoni mwa msimu. ***(Calcio Mercato - in Italian)***

### WANYAMA AWINDWA CELTIC

CELTIC inaweza kumfuata kiungo wa kimataifa wa Kenya asiyehitajika tena Tottenham, Victor Wanyama, 28, katika dirisha la Januari, amesema kocha wa klabu hiyo, Neil Lennon. ***(Team Talk)***

### WILLIAN NJIA PANDA CHELSEA

WINGA wa Chelsea na Brazil, Willian anataka kubaki Stamford Bridge, lakini klabu hiyo bado haijampa ofa ya mkataba mpya. ***(Express)***

### LENO ATETEA MFUMO ARSENAL

KIPA wa Arsenal, Bernd Leno amesema 'Gunners' wataendelea kujaribu kuanzia mpira nyuma, licha ya kufanya makosa na kuiruhusu Watford kupata bao wakati wakiongoza 2-0 Jumapili iliyopita. ***(Mirror)***

### AC MILAN KUPIGWA BEI

TAJIRI wa pili duniani, Bernard Arnault, anaandaa dau la pauni milioni 890 la kuinunua miamba ya Serie A, AC Milan. ***(Mail)***

### KOULIBALY ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ingeweza kumsajili beki wa Napoli, Msenegal Kalidou Koulibaly kama wangeshindwa kumnunua beki wa kati wa Uholanzi Virgil van Dijk, katika dirisha la Januari 2018. ***(Goal)***

### AZIVUTA ARSENAL, CHELSEA

BOURNEMOUTH inajiandaa kumpa mkataba mpya Ryan Fraser wenye thamani ya pauni 100,000 kwa wiki, na Arsenal, Everton, Chelsea na Wolves zote zinavutiwa na huduma ya winga huyo Mscotland mwenye miaka 25. ***(90min.com)***

### KABASELE KUJIFUNGA WATFORD

BEKI wa Watford na Ubelgiji Christian Kabasele, 28, amefunguka kuwa yupo mbioni kutia saini mkataba mpya na wakali hao wa Vicarage Road. ***(Sport Witness)***

### VELTMAN AITAJA WEST HAM

BEKI wa Ajax na Uholanzi, Joel Veltman, 27, amesema anataka kusaini kuichezea West Ham United majira haya ya joto, lakini mabingwa hao wa Uholanzi hawakutaka kumwachia. ***(NOS - in Dutch)***

### SCOTT SASA LULU ENGLAND

EVERTON, Southampton, Bournemouth, Sheffield United, Bristol City, Barnsley na Sunderland zote zimemtupia jicho winga wa Motherwell na Scotland U-21, James Scott, 19. ***(Team Talk)***

HABARI MICHEZO

## Kisiwani mabingwa wapya Kairuki Cup

**Na Mary Mosha,** SAME

MASHINDANO ya Angela Kairuki Cup 2019, yamemalizika rasmi mwishoni mwa wiki kwa timu ya soka ya Kisiwani United kuibuka na zawadi ya Ng'ombe, pikipiki na Sh. milioni 1.5 baada ya kutwaa ubingwa huo kwa kuichapa Ujamaa FC kwa mabao 2-1.

Katika mechi hiyo ya fainali iliyopigwa kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Hedaru, mabao ya washindi yalipachikwa nyavuni na Ally Rajab kunako dakika 35 na Juma Makumbi akipigilia msumari wa pili ulioibebesha timu yake ubingwa.

Kwa upande wa Ujamaa FC iliyokuwa imesheheni wakongwe, bao lao pekee lilitiwa kambani na Ezekiel Ombeni katika dakika ya 40.

Katika mchezo huo uliohudhuriwa na mashabiki lukuki wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angela Kairuki ilishuhudiwa mchezaji Ally Mbaga akitolewa nje ya uwanja kwa kadi nyekundu baada ya kumpiga kichwa mwamuzi wa pembeni wakati akilalamikia maamuzi yake dhidi ya bao lililofungwa na timu ya Ujamaa FC.

Kutokana na kutwaa ubingwa huo, Mgeni Rasmi, Waziri Kairuki aliikabidhi Kisiwani United zawadi ya Ng'ombe, pesa taslimu Sh. milioni 1.5, pikipiki moja, na medali 25 kwa wachezaji hao.

Kwa upande wa mshindi wa pili, Ujamaa fc, walijinyakulia kitita cha Sh. milioni moja, medali na pikipiki huku mshindi wa tatu akiambulia kiasi cha pesa tasilimu shilingi laki tano pamoja na medali. Mashindano hayo yanayofanyika kwa mwaka wa pili sasa na kudhaminiwa na Waziri Kairuki yameshirikisha timu 54 kutoka majimbo mawili ya Same Mashariki na Same Magharibi.

## JKU waanza kujifutua Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

USHINDI wa mabao 2-0 walioupata dhidi ya Selem View katika mechi yao ya ufunguzi wa Ligi Kuu Zanzibar, umeifungua mdomo JKU baada ya kueleza moto huo hautazimika na kwamba wataendelea kutoa vipigo msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa JKU, Saadu Ujudi alisema matumaini hayo yanatokana na timu yake kucheza vizuri na kwamba imempa matumaini ya hata ya kushika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo hadi sasa haina mdhamini.

Alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi na amekuwa akirekebisha makosa yanayojitokeza ili kuweza kutoa changamoto katika ligi hiyo yenye ushindani wa hali ya juu.

"Wachezaji wanajituma na hadi sasa nashukuru hakuna aliyepata majeraha, wote wapo vizuri, na hawana hofu mchezo mmoja ambao nilipata ushindi wa mabao 2-0 umenipa matumaini makubwa ya timu yangu kufanya vizuri zaidi endapo wachezaji wataendelea hivi hadi mwisho," alisema.

Katika ligi hiyo inayojumuisha timu 16, tayari michezo saba imeshachezwa ambayo ilianza kutimua vumbi Septemba 13, mwaka huu katika viwanja vitatu ambavyo ni Mau, Amaan, pamoja na Gombani.

# AZAM KUIWAHI MAPEMA TRIANGLE KWA MAFUNGU

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU wakiwa na deni la bao 1-0 waliloruhusu katika mechi yao ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika, wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Azam FC wataifuata mapema Triangle FC lakini kwa mafungu.

**Katika mechi ya kwanza ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam, Azam ilikubali kipigo hicho licha ya kumiliki mpira kwa kipindi chote, hivyo inahitaji kushinda kuanzia mabao mawili ili kuweza kusonga mbele.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, juzi, Ofisa Habari wa Azam FC, Jafari Maganga, alisema Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mrundi Etienne Ndayiragije, ameshauri waende Zimbabwe mapema ili kuweza kuzoea hali ya hewa na mazingira ya watakapocheza mechi hiyo.

"Kutokana na ushauri huo wa kocha, tutaelekea Zimbabwe Septemba 22 kabla ya mechi hiyo ambayo imepangwa kuchezwa Septemba 28, mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema kutokana na baadhi ya wachezaji wa kikosi hicho kukabiliwa na majukumu ya timu ya Taifa, Taifa Stars ambayo ipo kambini kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Sudan, wataondoka kwa mafungu mawili.

"Kundi la kwanza litaelekea Zimbabwe Septemba 22 kabla ya wachezaji waliopo Stars pamoja na kocha mkuu kuungana na wenzao nchini humo siku moja baadaye," alieleza.

Hata hivyo, Ndayiragije ambaye anakaimu nafasi ya kocha mkuu katika kikosi cha Stars, ameeleza Azam FC inaweza kupindua matokeo hayo kwa kuwa ameshafahamu uchezaji wa wapinzani wao na kuanza kufanyia marekebisho makosa yaliyojitokeza awali.

"Tatizo kubwa wapinzani wetu [Triangle FC], walicheza bila kufunguka na kufanikiwa kupata bao ambalo waliweza kulilinda hadi mpira unamalizika," Ndayiragije alisema.

"Wengi wanaamini kwamba ushindi ni nyumbani, lakini hata ugenini unaweza kupata matokeo kama ilivyokuwa wao na nimewaeleza wachezaji wangu tunaweza kushinda ugenini."




Mshindi wa Jackpot ya Sh. milioni 825, Magabe Marwa, akiwa na familia yake. Kulia ni baba yake, Marwa Maratho, wapili kushoto ni mama yake,Wisiko Warioba akifuatiwa na mke wa mshindi, Elizabeth Wambura. **PICHA: SPORTPESA**

# *Wazazi mshindi mil. 825/- wafunguka*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mwanawe kuwa mmoja kati ya washindi wawili waliojishindia jumla ya Sh. milioni 825.9 kupitia Jackpot ya Sportpesa mwezi uliopita, baba mzazi wa Magabe Marwa, Marwa Maratho, amefunguka kuhusu ushindi huo.

Magabe na mwenzake Kingsley Pascal kutoka Biharamuro, Kagera mwezi uliopita walifanikiwa kushinda kwa pamoja mamilioni hayo kabla ya kugawana na kila mmoja kuibuka na Sh. milioni 412 kufuatia kutabiri kwa usahihi mechi 13 za Jackpot.

Akifungukia ushindi huo wa mwanawe, Maratho alisema hakuamini wakati anampigia simu akimtaarifu ushindi wake akiwa anachunga mifugo yake.

"Wakati ananipigia simu kunitaarifu sikuamini, nilikuwa nachunga lakini alipokuja kunipigia binamu yake ambaye ni mkuu wa wilaya na kunitaarifu kwamba kijana wangu ameshinda na SportPesa, hapo ndio moyo ukaanza kufarijika kwamba na mimi nimeingia kwenye utajiri usiotarajiwa.

"Nilijisikia vizuri kabisa na jasho lilinitoka sehemu zote, ushauri wangu kama baba yake asikurupukie kufanya vitu. Aendelee na kazi yake, hizo hela aziweke na baada ya hapo tutakaa baadaye mimi na mama yake tutatafuta ushauri.

"Mimi sifa ambayo napenda aendelee nayo ni utanashati na upendo kwa watu maana bila upendo hata uwe na pesa ni bure, napenda kuwashukuru SportPesa, pia namuombea kijana wangu aitumie hiyo pesa vizuri na imsaidie yeye na ukoo wetu wote bila ubinafsi.

**HUYU HAPA MAMA YAKE**

Wisiko Waryoba ambaye ni mama wa Magabe, alisema: "Nilikuwa nyumbani nakamua maziwa ndio nikapata simu ya Magabe kuwa ameshinda mamilioni. Kwa kweli nilijisikia vizuri kwa sababu mtoto ameshinda na atanikomboa na maisha yangu magumu niliyoanza nayo.

"Awe ni mtoto mwenye imani na ningemshauri akae kwanza atulie kidogo na ndipo baadaye apange jinsi ya kuzitumia fedha hizo ambazo ni nyingi kwa kweli.

"Kwa ujumla fedha hizo zitatumika kifamilia kwa sababu hiyo hela aliyoshinda itasaidia kutatua changamoto ya maisha tuliyoanza nayo yasiweze kujirudia.

"Nilikuwa sina nyumba ya kuishi kwa hiyo mtoto wangu ameshinda hela hivyo nitapata nyumba ya kuishi na pia nitaendelea kuishi maisha mazuri."

# Michezo

Jumatano Septemba 18, 2019

Nipashe




Hazard: Chelsea, Real zinatofautiana hapa UKURASA 30

MNASTAHILI...



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akimkabidhi zawadi ya Ngao nahodha wa timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Enekia Kasonga, kama kumbukumbu ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa COSAFA mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vita Simba vyaanza, Mexime macho kodo

●●● Apania kubeba tena pointi zote msimu huu huku Aussems akieleza ugumu uliopo wakati...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Mexime akiendelea kutolea tena 'macho kodo' pointi sita za Simba, mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, safu yake ya ushambuliaji imezidi kunoga baada ya vita vya ushindani wa namba kuongezeka kufuatia kurejea kwa Mbrazil Wilker da Silva aliyekuwa majeruhi.

**Msimu uliopita, Kagera Sugar ikiwa katika Uwanja wake wa Kaitaba mjini Bukoba, iliichapa Simba kwa mabao 2-1 kabla ya kuja Uwanja wa Taifa na kuondoka tena na pointi tatu kufuatia kuitandika bao 1-0.**

Hata hivyo, kama ilivyo kwa Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi sita baada ya kushinda mechi zake mbili dhidi ya JKT Tanzania mabao 3-1 na kisha kuichapa Mtibwa Sugar 2-1, Kagera Sugar nayo mambo ni moto.

'Wakulima wa Miwa' hao, nao wameshinda mechi mbili huku milango yake ikiwa migumu hadi sasa kufuatia kushinda 2-0 dhidi ya Biashara United na kisha kuichapa Alliance FC bao 1-0, jambo ambalo Mexime anaamini kikosi chake ni bora msimu huu na kinaweza kuendeleza rekodi yake ya kuifunga Simba.

Mexime amesema anaamini Septemba 26, mwaka huu watakapokutana na Simba katika Uwanja wa Kaitaba, wanaweza kuwafunga tena mabingwa hao watetezi licha ya kuundwa na mastaa wengi wa kigeni.

Hata hivyo, kwa upande wa Simba inazidi kuimarika kufuatia winga wao Miraji Athumani kuandaliwa kuwa 'supa sab' na tayari amefunga katika mechi zote mbili akitokea benchi.

Lakini mbali na Miraji, kurejea kwa mshambuliaji Mbrazil Da Silva kumerejesha matumaini makubwa katika kikosi hicho ambacho bado kina hazina ya wachezaji wengi kwenye benchi lake, akiwamo Ibrahim Ajibu, suala ambalo linaelezwa litaamsha ushindani mkubwa wa namba.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, akizungumza na Nipashe jana baada ya mazoezi yanayoendelea kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam, alisema hali ya wachezaji wake kwa ujumla sasa ni nzuri na kikosi kinazidi kuimarika kila uchao licha ya nahodha wao, John Bocco kuwa mchezaji pekee aliyeko nje akiendelea kuuguza majeraha ya mguu.

"Wachezaji wanaendelea vizuri makosa machache ambayo nimeyaona kwenye mchezo uliopita naendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie tena," alisema Aussems ambaye anatambua vema ugumu wa mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar.

Alisema mchezo ujao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani na kuahidi kutumia nguvu nyingi kwa wachezaji kuhakikisha wanatetea ubingwa wao.

# Yanga wajichimbia Dar kuijadili Zesco

**Na Shufaa Lyimo**

YANGA imeanza mpango mkakati wa kuhakikisha inaitoa Zesco na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa baada ya mwishoni mwa wiki kulazimishwa sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa hivyo kuwa na deni kubwa la kulipa bao hilo la ugenini.

Na ili kuhakikisha wanafanya kama ilivyokuwa dhidi ya Township Rollers ugenini Botswana, leo uongozi wa klabu hiyo umepanga kujichimbia katika kikao kizito cha kuandaa mkakati wa ushindi.

Tayari Yanga ilishaeleza kuwa itawasili nchini Zambia wiki moja kabla ya mechi ili kuyasoma vema mazingira na kuzoea hali ya hewa ya huko, lakini leo watajadili mkakati mzito wa kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri na hatimaye kupata ushindi.

"Hicho kikao kitakuwa na mikakati binafsi ambayo watu hawatakiwi kuifahamu kwa sababu kwenye mpira kuna mambo mengi ambayo mengine yanafanywa kisirisiri," kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo ambacho kiliomba hifadhi ya jina lake.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hamad Islam aliwataka Watanzania wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita na badala yake wazidi kushikamana mpaka mwisho.

Mjumbe huyo alisema, lengo lao ni kuhakikisha timu yao inakwenda kufanya vizuri ugenini na kurudi na matokeo mazuri nyumbani na suala la kuitupa nje Zesco United linawezekana kama walivyoifanyia Township Rollers mjini Gaborone.

Katika mechi ya raundi ya awali ya michuano hiyo, Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa dhidi ya Township Rollers kabla ya kwenda Botswana na kushinda bao 1-0, matokeo ambayo pia wiki iliyopita waliyapata dhidi ya Zesco Uwanja wa Taifa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >